**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Saba – Tarehe 8 Novemba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwathibitishie tu kwamba vazi hili ndilo vazi rasmi la kimwambao kwa mujibu wa Kanuni ya 119. Pili, nilipotembelea Zanzibar tarehe 4/10/2006 Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar wakiongozwa na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji walinipa zawadi ya kanzu hii nzuri na kofia. Nimeona ni jambo la kiungwana kwamba niwaenzi na kuwashukuru kwa kulivaa vazi hili. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):-**

Taarifa ya Mwaka ya Benki ya Posta Tanzania kwa Mwaka 2005 *(The Annual Report of Tanzania Postal Bank for the Year 2005)*

Taarifa ya Mwaka ya *Twiga Bancorp* kwa mwaka 2005 *(The Annual Report of Twiga Bancorp for the Year 2005)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 82

**Serikali Kupeleka Madaraka katika Halmashauri na Miji**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupeleka madaraka zaidi katika Halmashauri za Wilaya na Miji, utekelezaji wake umezitenga Wizara katika usimamiaji wa sera, mafunzo ya wataalam na matumizi ya utaalam nchini:-

(a) Je, Serikali haioni hali hii hasa katika Wizara za Kilimo, Mifugo, Maliasili na kadhalika?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuunganisha pingili za mnyororo wa utaalam ambazo kwa sasa zimekatika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kupeleka madaraka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ulianza pale tulipotunga Sheria zinazoanzisha na kutoa utaratibu wa kuendesha Mamlaka za Serikali hizo. Sheria Na. 7, 8 na 9 za mwaka 1982 zilitungwa ili kutekeleza uamuzi huo wa Serikali.

Aidha, uamuzi huo wa kupeleka madaraka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa umekuwa ukiimarishwa na kuboreshwa kwa kuanzisha progarmu kama ile ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa. Kabla ya utaratibu huo Wizara zilijihusisha moja kwa moja na Sekta zake zilizopo katika Halmashauri, ikiwa ni pamoja na Kilimo, Mifugo na Maliasili.

Katika utaratibu wa kupeleka madaraka kwenye Halmashauri watumishi wa Sekta zote wanawajibika kwa Halmashauri. Wizara za Sekta zimebaki na jukumu la kusimamia sera na kuhakikisha kuwepo kwa viwango vya taaluma. Kwa hiyo, Wizara za Kilimo, Mifugo, Maliasili na nyingine zinasimamia sera, mafunzo ya wataalam na matumizi ya utaalam kwa kuzishusisha Halmashauri. Utaratibu huu umeziunganisha Halmashauri na Wizara pia unatekeleza nia nzuri ya Serikali ya kupeleka madaraka zaidi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kwamba, Wizara zote za kisekta ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo, Maliasili na Utalii zinaendelea kutekeleza sera ya kupeleka madaraka Mikoani bila matatizo yoyote. Wizara zimeendelea kusimamia Vyuo vinavyotoa wataalam na Halmashauri zinaendelea kuwaajiri katika maeneo husika. Hivyo, hakuna pingili za mnyororo ya utaalam uliokatika.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa lengo la maboresho ni kupunguza urasimu na kutoa huduma bora kwa wananchi. Lakini chini ya utaratibu uliopo hivi sasa kwa mfano, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo akitaka kupeleka maagizo kwa Afisa Elimu aliye chini ya Halmashauri ya

Wilaya inabidi apitie utaratibu ufuatao:- Moja, apeleke barua yake kwa TAMISEMI, TAMISEMI ipeleke kwa *RAS, RAS* aipeleke kwa *DAS* na *DAS* aipeleke kwa Mkurugenzi wa Wilaya ndipo imfikie Afisa Elimu. Chini ya dhana ya Kasi Mpya, isingekuwa vizuri baadhi ya maagizo yakatoka moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenda kwa Afisa Elimu wa Wilaya ili kutekeleza nia hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu kuhusiana na mawasiliano ya kati ya *Central Ministries* na Halmashauri zetu upo bayana; na kwa kweli siyo mbaya kama ambavyo Mheshimiwa Jackson Makwetta amejaribu kuliweka. Kimsingi utaratibu unasema yapo masuala ambayo wanaweza wakawasiliana moja kwa moja na Halmashauri zetu *provided* tunapewa nakala sisi kama Sekta *Ministry* lakini vilevile tunaosimamia eneo hili pamoja na Mkoa.

Lakini katika uratatibu wa kawaida yapo mambo ambayo maagizo yake yanatakiwa yafanyiwe usimamizi wa karibu na mzuri zaidi katika mazingira hayo ndipo tunapowasiliana kati yetu pamoja na hizo Wizara za Kisekta ili tuweze kuhakikisha kwamba ufanisi wa maagizo hayo unakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba hatuna mlolongo *bureaucratic* kiasi hicho ni utaratibu ambao ni *flexible* na una-*accommodate* kwa kweli hisia zote za Mheshimiwa Jackson Makwetta.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimwia Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu swali la msingi limesema kwamba kwa kutoa madaraka haya kwenye Halmashauri au Wilaya utekelezaji wake umezitenga Wizara katika usimamiaji wa sera.

Mheshimiwa Spika, utakuta kwa mfano, sera ya elimu inasema kwamba shule za sekondari kwenye Kata hizi ambazo ni shule za sekondari za wananchi, kila Kata ijenge shule ya sekondari moja kwanza na inapomaliza ndiyo ijenge shule ya sekondari ya pili.

Mheshimiwa Spika, lakini utakuta kwenye Halmashauri wanatoa vibali viwili katika Kata moja. Je, Serikali haioni kwamba haya ni matatizo makubwa shule zote mbili katika Kata moja zinakuwa hazina uwezo wa kukamilika wakati muafaka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, sera ya Chama cha Mapinduzi kuhusiana na suala hili la kuendeleza Elimu ya Sekondari inasema katika kipindi cha miaka hii mitano CCM itajitahidi kuhakikisha kwamba kila Kata inajenga angalau shule ya sekondari moja. Hiyo ndiyo lugha iliyotumika kwenye Ilani ya Uchaguzi. Kwa maneno mengine ni programu ya kipindi cha miaka mitano ya ujenzi wa shule za sekondari. Lakini msukumo lazima uwekwe tangu mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kwa suala ambalo Mheshimiwa Anne Malecela amelisema hali hii inategemea kati ya Wilaya na Wilaya na kwa kweli inategemea vilevile Halmashauri yenyewe na mahitaji yake yakoje kwa wakati unaohusika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninadhani isiwe pengine kwamba ni tatizo la jumla hivi, hapana, inategemea *demands* zenyewe za eneo husika na tumeona katika baadhi ya maeneo shule hizo zimejengwa mbili, na katika Mkoa kama Kilimanjaro hata shule za sekondari tatu zinajengwa kwa wakati mmoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwa kujali muda. Nina tatizo na swali linalofuata ningeomba kumwuliza Mheshimiwa Halima Mdee. Taarifa nilizosoma kwenye Vyombo vya Habari ni kwamba mgogoro huu sasa ni shauri ambalo liko Mahakamani na pia Mheshimiwa Halima Mdee ni Wakili wa upande mmoja wa shauri hili. Je, ni kweli?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, siyo kweli.

**SPIKA:** Nakushukuru uulize swali sasa kwa sababu ingekuwa hivyo ulikuwa huna haki ya kuliuza hili swali wala tusingelijadili hapa Bungeni. Lakini kama sivyo basi endelea.

Na. 83

**Mgogoro juu ya Mmiliki Halali wa Uwanja wa Shule wa Kawe B**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumetokea mvutano mkubwa juu ya nani mmiliki halali wa Uwanja wa Shule ya Kawe B, mvutano ambao umetokana na kuuzwa kwa eneo la Uwanja wa Shule ya Msingi Kawe B na Sekondari ya Kawe kwa *ISHIK Foundation*; na kwa kuwa, katika kipindi chote hicho Viongozi wa Serikali za Mitaa wa maeneo husika yaani Diwani, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, na Afisa Mtendaji wa Serikali wamekuwa wakiwakwepa wananchi kwa kutoitisha vikao kuhoji uhalali wa uuzwaji wa eneo hilo:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na mmiliki halali wa uwanja husika?

(b) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kukiuza kiwanja husika; na kwa nini wakazi wa eneo hilo hawakuhusishwa katika maamuzi ya kuuzwa au kutokuuzwa kwa kiwanja husika?

(c) Kwa kuwa, sehemu ya kiwanja cha shule kilichouzwa kilikuwa ni kwa ajili ya kujenga madarasa ya Kidato cha Pili – Cha Nne cha Shule ya Sekondari ya Kawe. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wanatarajia kuingia kidato cha pili mwakani lakini wamekwamishwa kutokana na kiwanja cha shule yao kuuzwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Kinondoni iliongeza idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza baada ya Mpango wa MMEM kufanikiwa. Shule mbili za Sekondari zilizokuwepo hadi kufikia mwaka 2004 hazikutosheleza kuwachukua wanafunzi wote waliofaulu. Kwa hiyo, Halmashauri iliamua kuunda Mfuko wa Elimu ili kupata fedha za kujenga shule za sekondari. Pamoja na jitihada hiyo iliamuliwa pia kutafuta wafadhili ili kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Kawe iliomba kukamilisha kujenga shule ya sekondari kwenye eneo la shule ya Msingi ya Kawe B kwa kutumia mfadhili aitwe "*ISHIK Foundation*." Makubaliano yalikuwa mfadhili aijengee Kata ya Kawe madarasa manne na Ofisi ya Walimu na Mfadhili apewe eneo lililopo jirani na shule ajenge shule yake binafsi. Kwa hiyo, mfadhili alipewa ekari 2.784 na ekari 3.588 zilizobakia zilikuwa kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari ya Kawe.

Maamuzi hayo yamepelekwa kwenye Kikao cha Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa Kinondoni na hatimaye yamepelekwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mamlaka zote mbili ziliidhinisha maamuzi hayo ya Kamati ya Kata ya Kawe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mmiliki halali wa ardhi hapa Tanzania ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999. Mamlaka za Halmashauri zimepewa mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi ambayo iko chini ya himaya zao. Kwa hiyo mmiliki halali wa uwanja wa shule ya msingi Kawe B ni Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni.

(b) Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyotumika kugawa kiwanja cha Kawe ni pamoja na:-

1. Uwezo mdogo wa wananchi wa Kawe katika kuchangia gharama za ujenzi wa shule na wananchi wengi walikuwa hawajachangia.

2. Masharti rahisi ya mfadhili ambaye alihitaji eneo dogo kutoka kwenye eneo kubwa ambalo lilikuwa halitumiki.

3. Eneo lilitengwa kwa ajili ya maendeleo ya shule na malengo hayakubadilishwa.

4. Kutekeleza agizo la Serikali la kujenga shule za sekondari kwa kipindi cha miezi mitatu.

Aidha, wakazi wa Kawe walihusishwa katika maamuzi ya kugawa kiwanja kwa kupitia wawakilishi wao na kwenye Vikao tarehe 5/5/2006, 2/6/2006 na 1/7/2006. Katika kikao cha tarehe 1/7/2006 wananchi walipewa taarifa kamili ya utaratibu uliotumika katika kuwapatia *"ISHIKI Foundation*" eneo la Ardhi.

(C) Mheshimiwa Spika, maendeleo ya shule ya sekondari ya Kawe yamezingatiwa na eneo la ekari 3.588 halijatumika. Manispaa ya Kinondoni inajenga madarasa 4 kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha pili na wanafunzi wa mwaka 2007 kidato cha kwanza. Aidha, ujenzi wa madarasa hayo unagharamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa hiyo uhakika wa kukamilisha madarasa hayo upo na yatakamilika kwa wakati.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo kwa kiasi fulani hayajaniridhisha. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza akakubaliana na mimi kwamba kweli eneo husika halina nafasi na kubadilisha uamuzi wa Serikali kama anavyodai?

Je, tunafahamu kwamba kuna maeneo mengi sana ya *Private Development Schemes.* Kwa nini lile eneo dogo kama ameliona atakuwa ameona kwamba sehemu iliyouzwa ni sehemu ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa *laboratory* ya shule ya sekondari hiyo husika na ilishaanza kujengwa nayo imeuzwa humo ndani. Kwa nini wapewe eneo hilo wakati kuna maeneo mengi na hilo eneo vilevile linaziba nafasi wanafunzi wanashindwa kupita kwenda kwenye hayo madarasa wanayosomea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali mamlaka ya kugawa ardhi yako mikononi mwa Halmashauri husika. Matumizi ya ardhi yako mikononi mwa mamlaka husika na iliona ni vyema kugawa ardhi hiyo na siyo kuuza, ardhi ile haikuuzwa bali wamegawa kiwanja. Sasa lengo la eneo hilo lilikuwa ni kwa

ajili ya elimu na huyo alipewa, amepewa kwa lengo la kujenga shule na hiyo shule ameishaanza kuijenga.

Kwa hiyo, naomba tuziheshimu Mamlaka za Serikali za Mitaa wanapotoa maamuzi yao ya kugawa ardhi kwa mtu yeyote ambaye anahitaji. Tukumbuke kwamba Halmashauri zinapewa maombi mengi kutoka kwa watu mbalimbali kuhusu maombi ya ardhi kwa ajili ya majukumu mbalimbali. Kwa hiyo, na yule mfadhili aliomba kwa lengo nzuri tu na Halmashauri ikaona ni busara kumpa kwa sababu ardhi hiyo waliona kwamba kwao haina matumizi ya zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea majibu ya nyongeza kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema kama nikiwa Mbunge wa Kawe nimetembelea eneo la mgogoro na vilevile nimekagua na kuwasikiliza wananchi wanataka nini. Nilichobaini kikubwa hapo wasiwasi wa wananchi ni kwamba eneo lile halikugawanywa kwa kufuata taratibu zinazopaswa.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba wananchi wanahofia kwamba eneo lililobaki halitatosha kwa ajili ya matumizi ya shule.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwamba eneo lililobaki linatosha kwa ajili ya maabara, linatosha kwa ajili ya matumizi ya shule na tutahakikisha nikiwa kama Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwamba tunawapatia eneo la kuweza kukamilisha mahitaji ya shule ya Kata ya Kawe ambapo mimi nikiwa Mbunge wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya uchunguzi wa kina kabisa kutazama kama kweli eneo hilo liligawa kwa utaratibu unaofaa na mimi binafsi nimehakikisha katika Wizara yangu na katika Manispaa ambako pia mimi ni Diwani kwamba utaratibu ulifuatwa na namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane kwa karibu kama Wabunge ambao tunapenda maslahi ya wananchi kuweza kuwahakikishia wananchi kwamba haki yao itapatikana na shule ya *ISHIKI* iko pale kwa ajili maendeleo ya wananchi wa Kawe vilevile. *(Makofi)*

Na. 84

**Ujenzi wa Daraja la Chitala**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa, daraja la Chitala ni muhimu sana katika Jimbo la Kibakwe na Wilaya ya Mpwapwa kwa ujumla kwa sababu linauganisha Tarafa za Rudi, Kibakwe na Mpwapwa; na kwa kuwa Serikali ilishaahidi kulijenga daraja hilo kwa muda mrefu lakini haijafanya hivyo.

Je, Serikali inaweza kutamka rasmi ni lini itaanza kulijenga daraja hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliahidi muda mrefu kujenga daraja la Chitala kutokana na umuhimu wake kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa daraja hili, Serikali katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 ilitenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, Serikali kwa kupitia Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Dodoma *(TANROADS),* ilitangaza zabuni ya ujenzi wa daraja hili mnamo mwezi Machi, 2006 na Mkandarasi M/S *Bahaj Construction Works* wa Dodoma kuteuliwa mnamo mwezi Mei, 2006 kutekeleza kazi ya ujenzi wa daraja hilo kwa mkataba Na.*TRD/DO/R.472/2005-06/16* wenye thamani ya Sh.97,660,600 kwa muda wa siku 120.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa daraja ilianza tarehe 29/05/2006 na mkandarasi alitarajia kukamilisha kazi hiyo tarehe 25/09/2006, lakini kutokana na matatizo mbalimbali yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mradi, mkandarasi aliongezewa muda wa kukamilisha kazi hadi tarehe 15/10/2006. Hali halisi ya kazi za ujenzi wa daraja la Chitala hadi kufikia tarehe 15/10/2006 zilikuwa zimekamilika kama ilivyokuwa kwenye mkataba. Kuanzia tarehe 16/10/2006 kazi hii imeendelea kuwa chini ya uangalizi wa mkandarasi ikiwa ni kipindi cha matazamio (*defects liability period*) cha miezi sita ambapo Mkandarasi anatarajia kukabidhi mradi tarehe 15/04/2007.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja hili ulijumuisha kazi zifuatazao:-

(a). Kujenga daraja la mfuto la zege lenye urefu wa mita 110

(b) Kujenga barabara zinazounganisha daraja kutoka pande zote mbili katika urefu wa mita 600.

(c) Kusafisha mkondo wa maji ili kuelekeza maji katika daraja.

(d) Kujenga kingo za mto karibu na daraja kwa *gabions* ili kuzuia mmomonyoko.

Ni imani ya Serikali kuwa kukamilika kwa daraja hili kutarahisisha mawasiliano na kutaharakisha maendeleo ya wananchi kiuchumi katika vijiji vya Jimbo la Kibakwe na Wilaya ya Mpwapwa kwa ujumla.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani kwa majibu mazuri, lakini shukrani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuweza kukamilisha daraja hilo. Lakini daraja ni sehemu ya barabara. Ningependa sasa niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, daraja lile sasa limekamilika na barabara bado si nzuri na hasa tunapozungumzia kuanzia Kinusi kuelekea Malolo. Lakini sasa ni muhimu sana kufikiria kutusaidia sehemu inayounganisha kati ya Wilaya ya Kilolo, Kilosa na Jimbo la Kibakwe kwa maana ya Mpwapwa. Kwa utaratibu ule ule ili kuweza kufungua barabara ile ambapo maeneo yale kuna watu wanazalisha sana mazao ya kilimo ambayo yangeweza kusafirishwa na yakasaidia mapambana na umaskini. Naibu Waziri yuko tayari kutusaidia tena maana hili eneo linaunganisha Wilaya ya tatu na hivyo likifunguka litatusaidia. Je yuko tayari kutusaidia kama alivyotusaidia katika hilo daraja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya Kinusi hadi Malolo ni muhimu sana na inaunganisha Wilaya tatu, yaani Kilosa, Kilolo pamoja na Wilaya ya Mpwapwa. Mimi ningesema tu kwamba tutashirikiana na Wizara ya Miundombinu kuangalia hiyo barabara na kuangalia uwezo wetu kifedha kama tunaweza tukaitengeneza.

Na. 85

**Tatizo Sugu la Maji**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Masasi ina tatizo sugu la Maji:-

(a) Je, Mradi wa Maji Mbwinji utakamilika mwaka gani na ni vijiji vingapi vitanufaika na mradi huo?

(b) Kwa kuwa, tatizo hili limeongezeka kwa kiasi kikubwa baada ya Bwawa la Mchema kupasuka, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati bwawa hilo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ili kusaidia kuondoa tatizo hilo kwa haraka zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Mbwinji una lengo la kauwapatia huduma ya maji safi na salama wakazi wa Miji ya Masasi na Nachingwea kwa kutumia chanzo cha maji cha Mto Mbwinji. Vijiji 16 vilivyopo kandokando ya bomba kuu la

maji vitahudumiwa na mradi huu. Mji wa Masasi ambao unaokadiriwa kuwa na watu 83,090 kwa sensa ya mwaka 2004 unapata maji kiasi cha mita za ujazo, 1,384 kwa siku ikilinganishwa na mahitaji ya mita za ujazo 9,000 kwa siku. Ili kupunguza tatizo hilo, Wizara imefanya usanifu wa mradi wa maji ambao utatumia chanzo cha maji cha mto Mbwinji kilichopo kilomita 40 kutoka Masasi. Gharama za ujenzi wa mradi utakaohudumia Miji ya Masasi na Nachingwea zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 34.5. Maombi ya fedha kutekeleza mradi huo tayari yamewasilishwa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika yaani *BADEA* na ujenzi wa mradi huo utaanza baada ya kupata fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, bwawa la Mchema lilibomoka kutokana na miti mikubwa kuota juu ya tuta la bwana na mizizi ya miti hiyo kudhoofisha tuta la bwawa. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imetafuta wataalam wa kufanya tathmini ya ukarabati wa bwawa la Mchema na kazi hiyo itaanza mwezi Novemba, 2006.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.Mradi huu kwa kuwa ni wa muda mrefu na Serikali ya Awamu ya Nne iliweza kupata fedha kwa ajili ya mradi huu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza ni kwa nini fedha hizo hazikuweza kufanya kazi katika mradi huu na zilipelekwa wapi na zimefanya kazi ipi?

Je, Wizara haiwezi kuiwezesha mamlaka ya maji iliyopo Wilayani Masasi angalau basi kusaidia kutengeneza maboma yaliyopo kwenye mradi wa maji Ndanda ili uweze kusaidia kutatua tatizo kubwa lililopo katika Wilaya Masasi ambapo wananchi wa Masasi hasa wanawake wanahangaika usiku kucha kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji mali?

**SPIKA** Mheshimiwa Mariam Kasembe, nimehisi kama swali la nyongeza umelisoma, lakini nimekuvumilia, siku nyingine sitaruhusu hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mbwinji umefanyiwa usanifu na sasa mradi umeshapelekwa maombi yake. Pesa za awali zilizokuwepo zimefanya shughuli za kufanya usanifu. Kama nilivyosema, mradi huu ni mkubwa sana ambao unachukua bilioni 34.5. Pesa hizo kwa Serikali peke yake haiwezi, ndio sababu tumekwenda kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa Ndanda ili maji yaweze kutumika kwa wananchi wa Masasi, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa hivi sasa Halmashauri yake imeleta maombi mbalimbali kwa ajili ya miradi midogo midogo kwa ajili ya kuhudumia Masasi na miradi hiyo naomba niitaje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya Masasi ni kwamba kwa hivi sasa kuna Vijiji ambayo vitapewa miradi hiyo na Vijiji hivyo katika jedwali langu inaonyesha kwamba kwa Masasi peke yake kuna miradi mawili ambayo ni Mradi wa Mraushi na Mradi wa Nambawala. Lakini hata hivyo, kwa hivi sasa Masasi inapata msaada wa maji kutoka

chemichem ya Mwena na pia katika chemichemi nyingine na visima virefu vilivyoko eneo la Magumchila katika Mji wa Masasi.

Na. 86

**Masuala ya Ndoa kwa Askari wa Ulinzi**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania JWTZ linaajiri vijana wa jinsia zote na kwa kuwa Watanzania wanayo haki sawa ndani ya mazingira ya kazi:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazompa fursa askari wa kiume anapooa mtu ambaye sio askari kuruhusiwa kuishi kambini na mkewe na kumnyima fursa hiyo askari wa kike?

(b) Je, Jeshi la Wananchi linapoamua hivyo, linamsaidiaje huyu askari wa kike anapoolewa na mtu ambaye sio askari hasa katika suala zima la makazi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania linaajiri vijana wa jinsia zote na wote wana haki na fursa sawa ndani ya Mkataba wa kila kinachofanyika ikiwa ni pamoja na masuala ya makazi na wanajeshi ili kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Jeshi. Kwa maana hiyo, utaratibu wa kijeshi unaotumika wakati mwanajeshi wa kike anapoamua kuolewa anatakiwa kujaza fomu za maombi ya kuolewa na katika fomu hizo kuna kipengele kinachomtaka yeye mwenyewe kuamua kama anapendelea kuishi nje au ndani ya Kambi akiwa na mume wake ambaye sio mwanajeshi. Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fursa ya kuishi kambini kwa mwanajeshi na familia yake hutolewa kwa wanajeshi wa jinsia zote na hakuna mwanajeshi anayenyimwa fursa hiyo. Kwa askari wa kike, uzoefu unaonyesha kuwa, uamuzi wa pahali pa kuishi mara nyingi hutolewa na wanaume wanaowaoa. Wanaume wengi wa Kitanzania wanapooa, awe anayeolewa ni raia au mwanajeshi hupendelea zaidi kuishi katika nyumba zao badala ya kuishi katika nyumba zinazomilikiwa na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeweka utaratibu wa kuwasaidia wanajeshi katika suala la makazi bila kujali jinsia zao. Kwa wale ambao

wanaishi nje ya Kambi kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuolewa, hupatiwa posho ambayo humsaidia kupangisha nyumba.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kwa kuwa wanawake wote wana haki sawa kwa waume zao kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa kuna baadhi ya askari wameoa mke zaidi ya mmoja lakini anayetambulika kisheria pale Jeshini mwanamke mmoja na watoto wanne: Je, Serikali haioni kwamba inawanyima haki wale wake wengine wa askari huyo na watoto?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Jeshi kama nilivyosema awali, linatoa fursa sawa kwa jinsia zote. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwa wale ambao wameoa wanawake ambao sio wanajeshi, wanajeshi hao wanapewa fursa ya kuishi katika kambi na kama nafasi hakuna, huwa tunawasaidia kuwapa posho kusaidia kukodisha nyumba nje, kama ni mke mmoja au wawili au wanne.

Na. 87

**Fedha kwa Ajili ya Kuongeza Ajira na Mitaji**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana iliyosomwa tarehe 4 Agosti, 2006, pamoja mambo mengine aliahidi kuwa Serikali itatoa Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa kwa ajili ya upatikanaji wa mitaji. Je, hadi hivi sasa ni fedha kiasi gani zimewafikia wananchi na wa Wilaya zipi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka huu wa fedha imetenga kiasi cha Shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati kupata mikopo yenye masharti nafuu. Fedha hizi zinatolewa kupitia mifumo mawili ifuatayo:-

(i) Mfumo wa kwanza ni ule ambao fedha kiasi cha Shilingi bilioni 10.5 zitapitia katika Benki ya *CRDB* na *NMB*. Benki hizi zimechaguliwa kwa sababu zina mtandao mpana hapa nchini na pia zina uzoefu katika kutoa mikopo midogo midogo.

(ii) Mfumo wa pili utatumia Shilingi bilioni 10.5 na utahusika Benki za Wananchi na Asasi nyingine za Fedha zenye uzoefu wa kutoa mikopo ya aina hii. Kutumika kwa asasi

hizi kutaongeza uwezo wa kuwafikia walengwa wengi zaidi. Asasi hizi ni pamoja na Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mikopo *(SCCULT),* Benki ya Posta, *First Adili*, *Akiba Bankcorp,* Benki za Ushirika na kadhalika. Katika mfumo wa kwanza, Serikali imekubaliana na Benki hizi kuwepo kwa masharti nafuu ya ukopeshaji ikiwemo riba isiyozidi asilimia kumi, kufutwa kwa ada za kuombea mikopo, kufutwa kwa ushuru wa kuchukulia fomu za mikopo na kadhalika. Katika mfumo wa pili, bado majadiliano yanaendelea kati ya Serikali na Taasisi za kifedha ili nazo zikubaliane na Serikali kuhusu masharti na taratibu za kutoa mikopo hii. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mfumo wa kwanza yamekamilika baada ya makubaliano *(MOU)* kati ya Benki Kuu na Benki za *CRDB* na *NMB* kutiwa saini tarehe 23 Oktoba, 2006 ambapo sasa kiasi cha Shilingi bilioni 10.5 kwa ajli ya dhamana kwa Benki hizo kimetolewa na hivyo kuziwezesha Benki hizo kuanza kutoa mikopo kwa walengwa wakati wowote kuanzia sasa.Maandalizi ya mfumo wa pili utakaohusisha Benki ndogondogo na asasi nyingine za fedha yanaendelea na mara utakapokamilika, mikopo itaanza kutolewa kwa walengwa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na shukrani kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina shukurani kwa Serikali kwa mpango huu mzuri sana ambao unaendelea. Nikitolea mfano Wilaya yangu ya Kongwa, tayari katika Kata zote 14 zimekwishaundwa *SACCOS* kwa ajili ya maandalizi ya mikopo hii. Kwa kuwa wananchi wanategemea mikopo hii iwasaidie katika msimu wa kilimo unaokuja ambao unaanza katika muda usiozidi wiki tatu hivi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawahakikishia wananchi wa Kongwa kwamba fedha hizi zitaweza kupatikana ndani ya mwezi huu mmoja ili waweze kuwahi msimu huu wa kilimo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kongwa kwa kukamilisha kuunda *SACCOS* katika maeneo yao yote. Pili ili kumthibitishia kwamba Serikali iko makini katika kutekeleza hilo na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameagiza kikao kesho kwa ajili ya kuhakikisha shughuli hii infanyika h araka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA - BANTU:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa fedha hizi zitapelekwa kwa *SACCOS* zaidi na kwa kuwa Majimbo mengine kama lile la kwangu Bukene, *SACCOS* ni kitu kipya, kwa Kinyamwezi wanasema mashikolo mageni na kwa kuwa wananchi wa Jimbo hilo la Bukene wamehamasika katika Kata zote 16 kuunda *SACCOS* lakini Maafisa Ushirika hawajafika kuwatengenezea utaratibu ili wawe-*registered.* Kwa kifupi wako *SACCOS* bila *registration*. Je, Serikali iko tayari kuwapa mikopo hawa *SACCOS* ingawa hawajapata *registration* kwa sababu Ushirika hawajawafikia?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza tunawapongeza

kwa kuwahamasisha wananchi kujiunga na *SACCOS*. Lakini vile vile tunatoa wito kwa Maafisa Ushirika katika Wilaya ambazo hazijasajili na vikundi vipo, wafanye haraka sana kukamilisha zoezi hilo kabla Serikali haijachukua hatua. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la mwisho la nyongeza. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri amelieleza Bunge kwamba Mfumo ule wa pili wa kutumia Benki za Wananchi, Vyama vya Akiba na Mikopo na vikundi vingine vya wakulima ndio utakaouwezesha mpango huu wa fedha kuwafikia wananchi wengi zaidi. Kwa kuwa mpaka sasa hivi mfumo huo wa awamu ya pili ndio bado uko kwenye majadiliano. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atatuhakikishia kwamba na mfumo huo unatakiwa uchukue hatua zinazotakiwa kwa haraka ili uanze kutumika sambamba na huo mfumo wa mabenki ambao umeanza sasa hivi ili wananchi hao wengi waweze kufikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Mfuko huu kwenda haraka ili wananchi waweze kunufaika na Mfuko huu mapema inavyowezekana. Majadiliano yanayoendelea sasa ni kuhakikisha kwamba Mfuko huu utakuwa na masharti nafuu kwa wananchi. Serikali inasimamia kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika badala ya kutozwa riba kubwa pamoja na fedha nyingine nyingi ambazo itakuwa hazina msingi na kuongeza mzigo kwa wananchi. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada ni kubwa na hatulali usingizi mpaka tuhakikishe kazi hii imefanikiwa. *(Makofi)*

Na. 88

**Mikopo kwa Vijana na Jamii ya WafugajiI**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Asasi zote za Mikopo wananchi wa maeneo ya wafugaji hawapati mikopo ya aina yoyote;

(a) Je, Serikali itachukua utaratibu gani kuwasaidia vijana ambao hawana ajira hasa wa jamii ya wafugaji?

(b) Kwa kuwa umaskini ni mkubwa sana kwa vijana wa jamii ya wafugaji na ndiyo maana wamejaa mijini kulinda nyumba za watu. Je, Serikali itachukua hatua gani za kuwapatia mikopo huko huko waliko?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali kuwasaidia vijana wasio na ajira ni pamoja na kuimarisha Mifuko ya Mikopo ifatayo. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa *SELF* na Vyama Vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)* na kuhamasisha Vijana wakiwemo wafugaji kujiunga na kutumia mifuko hiyo. Vile vile Serikali itatumia utaratibu wa Mikopo ya Masharti nafuu utakaotolewa katika mpango wa kuwakopesha wananchi shilingi Bilioni moja kwa kila Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha Mkakati wa kukuza ajira nchini ambapo wadau wote wameshirikishwa. Pamoja na mambo mengine, mkakati huo unafafanua namna bora na endelevu ya kuwafanya vijana wajiajiri sehemu walipo na kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Mkakati huu unawataka vijana kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali, vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* na Asasi mbali mbali zisizo za kiserikali kwa lengo la kuwezeshwa wapate mikopo nafuu kama mitaji ili kukuza ajira na kujipatia elimu ya ujasiriamali.

Lengo kuu la mkakati huu ni kuhakikisha kwamba vijana wanafanya shughuli ambazo zinalingana na mazingira yao ikiwemo ufugaji. Mkakati huo pamoja na mambo mengine unaimarisha namna ya kupata mitaji kupitia vyanzo nilivyovitaja, taarifa mbali mbali muhimu zikiwemo za masoko na huduma za ugani nazo zinapatikana kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati huu utakapoanza, Serikali itahitaji kupata ushirikiano kutoka katika jamii yetu yote ikiwemo sekta binafsi, madhehebu ya dini na viongozi wa ngazi zote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa vijana hawa walinzi pamoja na wamachinga walioko mijini, wamekwenda mijini kwa sababu ya umaskini. Na kwa kuwa Serikali imeona hilo, wakasema watawajengea wamachinga ghorofa 5, na kwa busara hiyo hiyo, Serikali isingeona namna ya kuwasaidia hawa walinzi waliokwenda mijini ili nao wanufaike?

Swali la pili, kwa kuwa vijana hawa wanaweza wakafanya kazi lakini hawana mitaji na wanaweza kunenepesha mifugo na kuuza lakini hawana mitaji. Je, Serikali itachukua hatua gani kuwatengea fungu maalum hawa vijana watoke mijini waende kunenepesha mifugo na kuuza badala ya kukaa mijini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, la kwanza; napenda kulithibitishia Bunge lako kwamba Serikali katika mpango mzima wa kuwawezesha wananchi, imeangalia makundi yote na kila Wilaya tumeweka utaratibu wa Kamati ya Maendeleo ya Wilaya kusimamia mpango wetu wa ukopeshaji.

Kwa hiyo, vijana wa Kimasai au wafugaji ambao wametawanyika maeneo mbali mbali ya nchi, watahudumiwa katika maeneo waliopo kama Watanzania. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni wajumbe wa Kamati za Fedha za Halmashauri wahakikishe pia wanatusaidia kulisimamia hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile namna nyingine ya kuwanufaisha vijana ambao ni walinzi walioenda maeneo mbali mbali, ni kuhakikisha nao wanajiunga katika mfumo wa *SACCOS*. Wakiita *SACCO* ya Walinzi, nayo inakubalika. Halafu na yenyewe itaweza kupata zana bora zaidi badala ya kuendelea kulinda kwa mapanga na mashoka. Ahsante! *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya swali la Msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba zimetengwa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa. Ningependa kufahamu kwamba kwa kuwa shilingi bilioni moja ni kidogo kulingana na mahitaji ya wananchi katika maeneo hayo, na kwa kuwa Mkoa unaundwa na Wilaya mbali mbali, ni vigezo gani vitatumika kuhakikisha kwamba hakuna Wilaya itakayoachwa katika mkopo huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, utaratibu uliowekwa na

Serikali, ni utaratibu mzuri ambapo tumeweka shilingi bilioni moja kwa kila mkoa na katika mgao wa kwanza kama tulivyoeleza awali, kila mkoa utapata shilingi milioni 500 ambazo zitagawanywa sawa kwa Halmashauri zote.

Mgao huo ambao utakuwa sawa kwa sawa ndio utakaotumika kama mtaji wa kwanza kwa wananchi wetu. Napenda kulithibitishia Bunge hili kwamba lengo la Serikali siyo kwamba kwa kutoa bilioni moja kwa kila mkoa ndio tumemaliza kazi, tunajua kwamba huu mpango ni wa muda mrefu, tunataka mpango huu uwe endelevu na kila mwaka tutakapokuwa na uwezo, Serikali itaongeza fedha zaidi.

Lakini tutaomba na Waheshimiwa Wabunge watusaidie kuelimisha wananchi umuhimu wa kulipa fedha hizo ili mtaji uzidi kukua.

Na. 89

**Kunusuru Misitu**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa misitu na wanyamapori ni hazina na maliasili ya kujivunia nchini Tanzania. Misitu inaleta mvua, inaboresha mazingira na inatunza wanyama; na kwa kuwa misitu mingi hapa nchini imepukutika kwa sasa na kusababisha uharibifu wa mazingira:

(a) Je, Serikali imeandaa mkakati upi wa kunusuru misitu asilia katika hali ya kulinda wanyamapori na baadhi ya miti ambayo ni hazina kubwa ya taifa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa hali ya Mazingira Jimbo la Iramba Magharibi ni mbaya sana katika Kata ya Mtoa/Mtekente katika vijiji vya Msai, Msansao, Ujungu na Maghoba?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatvyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina Programu ya Taifa ya Misitu ambayo inabaini mikakati na maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa Sera ya Misitu katika jitihada za kuinusuru Misitu ya Asili.

Mikakati iliyopewa kipaumbele katika Programu ya Taifa ya Misitu ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Kushirikisha Wananchi katika Utekelezaji wa Programu ya Misitu: Kwa kuzingatia Programu ya Misitu, Ushirikishwaji wa wananchi katika

uendelezaji, uhifadhi na ulinzi wa misitu umepewa kipaumbele. Ushirikishwaji huu umelenga katika maeneo mawili ambayo ni ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi wa misitu hasa katika vijiji na ushirikishwaji wa sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali katika usimamizi na uendelezaji wa misitu.

(ii) Mheshimiwa Spika, kusimamia na Kuendeleza Mashamba ya Miti na Misitu ya Asili: Msukumo mkubwa umewekwa katika kuhimiza upandaji wa miti na kuhifadhi misitu kwa kunzisha Siku ya Taifa ya Upandaji Miti. Katika kuadhimisha siku hiyo, jumla ya miti 468,292,942 imepandwa nchini kote kuanzia mwaka 2000 hadi 2004.

(iii)Mheshimiwa Spika, Kuandaa na Kuzingatia Mpango wa Uvunaji katika Misitu ya Asili na Kushirikisha Wadau katika Ngazi ya Wilaya na Vijiji katika kutoa Leseni za Uvunaji katika Misitu hiyo: Katika Mkakati huu wataalam wa misitu wanasimamia uvunaji kwa karibu ili kuhakikisha kuwa aina na umri wa miti itakayovunwa ni ile tu inayoruhusiwa kitaalam.

Hali kadhalika, Kamati maalum za Wilaya husika zimeanzishwa kusimamia mpango wa uvunaji chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya. Matarajio ya Wizara ni kwamba, uvunaji utafanyika chini ya usimamizi madhubuti na endelevu.

(iv) Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Vikosi vya Doria: Katika mkakati huu, Wizara imeunda Vikosi vya kudhibiti uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu. Hadi sasa Wizara imeanzisha Vikosi Vitatu katika Kanda zifuatazo:- Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kusini na Kanda ya Mashariki. Wizara ina lengo la kuwa na Vikosi katika Kanda zote saba. Mwaka huu wa fedha, Wizara imepanga kuanzisha Vikosi Vinne zaidi. Wizara inaimarisha Vikosi hivyo vilivyopo kwa kuongeza watumishi na vitendea kazi ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

(b) Kuhusu hali ya Mazingira ya Jimbo la Iramba Magharibi, Serikali inatambua kuwa maeneo mengi yaliyoko katikati ya nchi yetu pamoja na Jimbo hilo yanakabiliwa na hali ya ukame na hali mbaya ya mazingira. Wizara yangu ikishirikiana na TAMISEMI inawahimiza wananchi kupitia Halmashauri za Wilaya zao kuhifadhi mazingira hususan kuendeleza misitu kwa kuhifadhi uoto wa asili na kupanda miti ya asili inayovumilia ukame. Aidha, Wizara yangu itatumia uzoefu wa kuhifadhi uoto wa asili katika Mkoa wa Shinyanga kupitia Mradi wa Uendelezaji Misitu ya Asili na Kilimo mseto *(NAFRAC)* ambao utashughulikia usambazaji wa uzoefu katika Wilaya kame nchini kote ikiwemo Wilaya ya Iramba.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba maeneo ya Mikoa ya Kati ni kame sana ikiwemo Wilaya ya Iramba, lakini kwa bahati nzuri Wilaya ya Iramba tunayo misitu asilia. Sasa Je, Wizara ipo tayari kwenda kufanya utafiti katika eneo la Kinampanda kuelekea Kinyangili, Msingi na baadae tukashuka Dolomoni ambako kuna misitu asili ili eneo hilo likatengwa kwa ajili ya misitu asilia na kuwa eneo tengefu?

Pili, kwa kuwa wakati nauliza swali la msingi kipengele (b) nilizungumzia Vijiji vya Mtoa, Msai, Mtekente, Ujungu na Maghoba, eneo hilo ni maarufu sana kwa miti iitwayo Mpingo ambayo ina faida kubwa sana, lakini kwa hivi sasa miti hiyo inavunwa hovyo bila utaratibu kwa kukosa elimu. Je, Wizara ipo tayari sasa kuweza kuunusuru mti huo wa Mpingo katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika mapori ambayo Mheshimiwa Juma H. Killimbah ameyataja, mengi ya mapori hayo ni mapori ya wazi. Aidha kutokana na uharibifu mkubwa ambao umefanyika, utafiti uliofanywa na Maafisa Maliasili na Maafisa wa Misitu, umegundua kwamba mapori hayo yamefikia hatua mbaya sana kutokana na wafugaji kufuga katika misitu hiyo na pia wakulima kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo hayo. Hata hivyo, Maafisa wa Maliasili wa Maeneo ya Wilaya ya Iramba na Wilaya zingine za Singida, walikuwa na kikao cha pamoja na katika kikao hicho, waliazimia pamoja na mambo mengine kuinua hadhi ya misitu ambayo ni ya wazi ili iwe misitu tengevu.Lakini hata hivyo, pamoja na kuinua hadhi ya misitu hiyo kuwa misitu tengevu, bado wananchi wanatakiwa kupata elimu ili wasichunge katika misitu na wasilime katika misitu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba katika maeneo mengi ya misitu asilia kuna miti aina ya Mipingo. Aina hii ya miti ina faida sana. Kwanza inatumika katika kutengeneza vinyago na vile vile inatumika katika kutengeneza vifaa vingine vya nyumbani. Miti hii inavunwa baada ya miaka 70. Kwa hivyo, namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itafuatailia na kuhakikisha kwamba mafunzo yanatolewa kwa wananchi wa Iramba Magharibi na Wilaya nzima ya Iramba ili wananchi hawa waweze kufahamu kwamba mipingo ni miti ambayo; kwanza ina faida kubwa lakini vile vile haipaswi kuvunwa kabla ya miaka 70 na ikizidisha sana miaka zaidi ya 80, inaota fangasi na inaharibika. Kwa hiyo watapata elimu hiyo. Namwahidi Mheshimiwa Juma H. Killimbah ajitayarishe tu semina inakuja. *(Makofi)*

Na. 90

**Ufumbuzi Wa Tatizo La Usafiri Kwa Wanafunzi**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya limu na Mafunzo ya Ufundi ina mapngo wa kulitafutia ufumbuzi tatizo la usafiri wa wanafunzi Jijini Dar es Salaam kwa kuwashauri wazazi wanaosomesha watoto wao kwenye shule za Serikali zilizo mbali na maeneo wanayoishi kwamba wawahamishie watoto wao katika maeneo yaliyo karibu na nyumbani kwao au katika Kata wanazoishi, lakini kwenye shule hizo pia zinakuwa zimejaa kabisa kuweza kupokea watoto kutoka shule hizo. Na kwa kuwa katikati ya Jiji la Dar es salaam zipo shule ambazo kwa asilimia kubwa wakazi wa maeneo hayo hawapeleki watoto wao kusoma katika shule hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitumia shule hizo kupunguza mlundikano wa wanafunzi waliozidi kwenye baadhi ya shule za Jiji?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa ziko shule ambazo zimejaa kiasi kwamba haziwezi kupokea wanafunzi zaidi wanaoishi katika maeneo yao. Lakini pia kuna wazazi ambao hawataki kuwaandikisha watoto wao kwenye shule zilizo karibu na wanakoishi hata kama nafasi zipo. Ili kurekebisha hali hiyo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Serikali inatoa wito kwa wazazi/walezi kuwaandikisha watoto wao wa Darasa la Kwanza katika shule zilizopo katika maeneo wanayoishi kuanzia mwezi huu wa Novemba, 2006.

(ii) Kutoa wito kwa wazazi/walezi kuwahamishia wanafunzi kwenye shule zilizo karibu na maeneo wanakoishi watumie kipindi hiki cha likizo.

(iii) Maafaisa Elimu wameagizwa kushirikiana na wazazi kupitia kamati za shule kusimaia zoezi la kuwahamashia watoto kutoka shule zilizojaa kwenda kwenye shule zenye nafasi.

(iv)Maafisa Elimu wameagizwa kurekebisha Ikama ya walimu na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

(v) Wizara imeagiza uchaguzi wa Kidato cha Kwanza kuanzia mwaka 2007 uzingatie maeneo wanayotokea wanafunzi.

(vi) Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hilo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, itatoa fedha kiasi cha shilingi 310,000,000/= kuunga mkono juhudi za Mkoa wa Dar es Salaam, kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa kwa kutumia nguvu za wananchi.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu na ruzuku ya uendeshaji kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii, kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kutuunga mkono katika kuhamasisha wazazi na walezi kuandikisha na kuhamishia wanafunzi katika shule zilizo karibu na wanakoishi, kama njia mojawapo ya kupunguza matatizo ya usafiri kwa wanafunzi.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Wazazi wengi hawapenda kupeleka watoto wao mbali na maeneo kwa kuzingatia watoto wao ni wadogo na ni hatari. Wazazi wengi wangependa watoto wao wasome katika maeneo yao, tatizo lililopo ni kwamba kiwango cha elimu kinachotolewa katika shule ambazo wazazi wengi wanahamisha watoto wao kinatofautiana na shule zingine.

Sasa Serikali itakubaliana nami kwamba sasa imefika wakati kuangalia kwamba kiwango cha elimu kinachotolewa kwa shule zote kiwe cha aina moja na kiwango kimoja ili kupunguza hii dhana ya wazazi kuona shule moja bora zaidi kuliko nyingine pale maeneo wanapoishi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli wazazi hupenda kufuatilia sana kuona elimu inayotolewa katika shule wanazowapeleka watoto wao kuona kama ni bora au siyo bora. Lakini katika agizo letu ndiyo maana tumewaagiza Maafisa Elimu katika kila Wilaya wahakikishe wanafuatilia suala hili ambalo linawakera sana wazazi kuona kwamba elimu inapishana kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge. Ndiyo maana Wizara imeagiza waangalie mahali ambapo pana wanafunzi waliojaa wasipeleke zaidi, wapeleke mahali ambapo hapajaja. Lakini Ikama ya walimu ambayo ndiyo jambo la msingi katika ufundishaji, lizingatiwe. Lakini pia vyumba vya madarasa vijengwa vya kutosha na walimu wapelekwe wa kutosha.

Lakini pia Wizara yetu ndiyo maana imejitolea kutoa fedha kama shilingi milioni 310 ziende zikaboreshe mazingira ya kusomea na ya kujifunzia kwa wanafunzi ili elimu iweze kuondokana na tofauti hizi za ubora. Kumbe Wizara yetu itaendelea kulifuatilia hili suala kwa karibu ili kuhakikisha elimu inakuwa na ubora unaolingana katika maeneo yote ya mijini. (*Makofi*)

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watalaam mbalimbali huwa wanapewa mafunzo ya namna mbalimbali ili kuweza kuboresha taaluma zao na mafunzo haya hutolewa mara kwa mara. Je, kuna mkakati gani wa kuwasaidia walimu wa shule za msingi ambao ndiyo wanaowafundisha watoto wetu elimu ya awali na elimu ya msingi kwa ujumla ili waweze kuwa bora katika ufundishaji wao licha ya ile elimu wanayopata ya cheti.

Je, utaratibu ni kwa kiwango gani ambavyo inawapa mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kuhakikisha kwamba na wao wanakuwa bora katika ufundishaji wao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu ina mpango mzuri sana wa kuwaendeleza walimu katika nyanja za ufundishaji wa masomo yao kwa kuandaa kozi fupi fupi na semina mbalimbali za ufundishaji wa masomo kama ya

hisabati, sayansi na masomo mengine kila nafasi inapopatikana na hasa haja inapoonekana kwamba ipo ili kuweza kubadilisha mfumo namna ya kufundisha masomo hayo. Tunavyo vyuo ambavyo vyote vinaendesha mafunzo ya kuwapandisha daraja walimu ambao wapo katika ngazi ya chini kwenda katika ngazi ya juu. Vyuo hivi ndivyo vinatumika katika kila kanda. Sasa walimu hatuwezi tukawaacha wakabaki na elimu ile waliyoipata pale walipokuwa vyuoni. Ndiyo maana tunaandaa mipango hii ya kila mara ya kuwa na kozi za muda mfupi ili kuweza kupandisha madaraja yao na kufundisha masomo yale ambayo yanahitaji labda pengine ufundi maalum katika kufundisha kulingana na mazingira ya kisasa. Hata *computer* hivi sasa inaanza kufundishwa na walimu wetu wataanza kupata mafunzo katika vyuo vyetu ambavyo tumeshaanza kuvibadilisha na kuviwekea *computer* ili walimu waanze kujifunza taaluma hiyo kwa ajili ya kuwafundisha watoto katika shule zao.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niongezee kidogo kwa yale majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu suala la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Ruth Msafiri kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama alivyosema Naibu Waziri, kwamba Wizara ina mpango wa kuendeleza walimu. Lakini mimi ningependa kutumia nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri, ninavyofahamu mimi kwa kila Wilaya ina *Teachers Resource Center* yaani Kituo cha Walimu ambacho kinahudumia *cluster*. Ni vizuri Halmashauri zikatumia vituo vya walimu kutoa mafunzo ambayo yameandaliwa na Halmashauri husika. Kwa mfano, baada ya matokeo ya darasa la saba ni matumaini kwamba Maafisa Elimu wa Mikoa, kwa kusaidiana na Maafisa Elimu wa Wilaya watakaa na kuangalia maeneo ambayo wanafunzi katika maeneo yao hawakufanya vizuri. Kila Wilaya ina Maafisa Elimu Taaluma, ambao ndiyo kazi yao.

Kwa hiyo, watumie vituo hivyo kuwasaidia walimu katika maeneo ambayo wanafunzi wao hawakufanya vizuri hasa baada ya matokeo ya mtihani wa darasa. Kwa hiyo, mafunzo ya ualimu siyo lazima yatokee Makao Makuu, tu hata Wilaya husika inaweza kuwa na mpango wao wa kusaidia walimu katika maeneo yao. Njia nzuri ya kuhakikisha kwamba vituo vya walimu vinafanyakazi ni Halmashauri kuweka mpango wa kutoa mafunzo katika vituo vyao katika bajeti zao ili mafunzo haya yawe endelevu. Kwa hiyo, tusisubiri tu Wizara ya Elimu, lakini hata Halmashauri katika maeneo yanaweza kuwasaidia walimu katika maeneo ambayo wanafunzi hawafanyi vizuri. Nakushukuru. (*Makofi*)

Na. 91

**Suala la Serikali Kuuza Nyumba zake**

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni nyumba nyingi za Serikali zimeuzwa na kusababisha upungufu wa nyumba na mkanganyiko katika suala zima la wajibu wa Serikali wa kuwapatia nyumba watumishi wake wenye stahili na kwa kuwa kumekuwepo na taarifa za upendeleo na hata matumizi batili ya fedha za umma zilizotumika kujenga au kukarabati baadhi ya nyumba zilizouzwa na kwamba hakukuwa na uwazi wa kutosha na kwa upande mwingine zimejengwa nyumba nyingi hapa Dodoma na Dar es Salaam ambazo hatima yake haieleweki na kwa kuwa kumekuwepo na kauli kadhaa zinazopingana na kwa nyakati tofauti kwamba uuzaji umesimamishwa au utaendelea au zitatumika na taasisi nyingine na mengine kadhaa wa kadhaa, ili mradi hakuna jambo moja linaloeleweka:-

(a) Katika mazingira kama haya, je, Serikali haioni kuwa ni vema kuweka na kueleza msimamo ulio wazi kuhusu suala hilo?

(b) Bila kujali usahihi wa zoezi hilo na ili mradi zoezi lenyewe limetekelezwa au linatekelezwa. Je, kwa wafawidhi wastaafu ambao walishiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa hili kwa hali na mali, nao wasipewe fursa sawa ya kuuziwa nyumba hasa ikizingatiwa kwamba walichangia ujenzi huo kwa kodi zao?

(c) Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba watumishi wanaendelea kupatiwa nyumba kulingana na stahili zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kuanzia mwaka 2001 iliamua kuuza baadhi ya nyumba zake kwa watumisahi wa Umma kwa lengo la kuwawezesha watumishi hao kupata makazi bora wakati wakiwa kazini na baada ya kustaafu.

Aidha, Serikali ilifikia uamuzi huo ili kuondokana na gharama kubwa ya kuzifanyia matengenezo nyumba hizo. Hatua ya kuuza nyumba hizo ilisaidia kuzizungusha fedha zilizopatikana ili ziweze kutumika kujenga nyumba nyingine ambazo pia zingeuzwa au kupangiwa watumishi wengine na hivyo kupunguza tatizo kubwa la makazi kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba kumekuwa na kauli zinazopingana kuhusu suala hili isipokuwani kwamba kwa kuwa ni zaidi ya miaka mitatu sasa tangu zoezi hili lianze. Serikali ya Awamu ya Nne, imeanza kufanya tathmini ya zoezi zima ili kubaini mapungufu yoyote yaliyotokana na utekelezaji wa zoezi hili. Matokeo ya tathmini hiyo yataisaidia Serikali kuboresha mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi hili.

Kubwa katika maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Nne, ni kusisitiza maamuzi ya awali kwamba baada ya nyumba zilizoamuliwa kuuzwa, nyumba zingine zitakazojengwa rasmi au kutengwa rasmi kwa ajili ya Viongozi na watumishi wengine wenye stahili *(tied quarters)* hazitauzwa. Aidha, pale ambapo utaratibu au mantiki haikutumika wakati wa utekelezaji, hatua zitachukuliwa kurekebisha hali hiyo ikiwemo kuzirudisha nyumba kama hizo Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuweka uwazi na kuondoa malalamiko ya upendeleo katika zoezi hili, Serikali ilitoa vigezo kadhaa za mtumishi kuuziwa nyumba, vikiwemo vifuatavyo:-

❖ Mhusika awe mtumishi wa Umma na awe ameipata nyumba hiyo kihalali.

❖ Mtumishi awe anaishi katika nyumba anayokopa.

❖ Mtumishi alipe deni lake la pango kabla ya kupewa mkataba na kuuziwa na pia atoe ahadi ya kulipa mkopo wake kabla hajastaafu au ndani ya kipindi cha miaka 10 ya utumishi wake Serikalini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kuna Watanzania wengi na hasa wazalendo ambao kwa namna moja au nyingine wameisaidia nchi hii pamoja na watu wake katika mambo mengi yenye kuzingatia maslahi ya Taifa letu. Kwa kutambua hilo, Serikali pamoja na kuwa na nyumba chache, imejaribu kuwapangisha nyumba baadhi ya watumishi wa umma waliostaafu muda mfupi tu kabla ya uamuzi wa Serikali wa kuuza nyumba zake kwa watumishi wa umme. Hata hivyo, haikuwezekana kuendelea kufanya hivyo kwa wastaafu wote kwa vile wastaafu hao ni wengi sana lakini nyumba ni chache mno. Aidha, napenda kusisitiza kuwa dhana kubwa ya mpango huu ilikuwa ni kumpa motisha na kumpunguzia mtumishi wa umma ambaye hajastaafu makali ya ukosefu wa makazi na kumwezesha kuongeza ufanisi katika kutekeleza kazi zake kwa umma.

(c) Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kutekeleza mpango huu wa kuuza na kujenga nyumba mpya za Serikali, nyumba zipatazo 967 zimekwisha jengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na zile zilizojengwa Dar es Salaam na Dodoma. Nyingi ya nyumba hizo zimekamilika au zipo katika hatua mbalimbali za kukamilishwa.

Nyumba zote zilizojengwa Dar es Salaam na Dodoma ambazo zimekamilika, zimepangiwa watumishi wa umma wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamepangiwa nyumba za Dodoma na wanalipa kodi. Aidha, nyumba zingine za Dodoma zitapangiwa watumishi wa Chuo Kikuu kipya kinachotarajiwa kujengwa Dodoma.

Kadhalika kuhakikisha kwamba watumishi wenye stahili ya kupewa nyumba na Serikali wanapewa nyumba. Serikali imetenga baadhi ya nyumba na inaendelea kujenga nyumba kwa ajili ya viongozi na watumishi hao. Nyumba hizo zinazotengwa kwa namna hii, kuanzia sasa hazitauzwa. Nyumba hizo ni pamoja na nyumba 91 za Jijini Dar es

Salaam na nyingine 38 za Mikoani na nyumba 42 zinazoendelea kujengwa katika Wilaya 4 mpya za Siha, Nanyumbu, Mkinga na Chato.

Serikali inaendelea kutenga fedha katika bajeti kila mwaka ili kuendelea kujenga nyumba kama hizo kwenye Wilaya zingine. Lakini pale ambapo inathibitika kuwa mtumishi mwenye stahili ya kupewa nyumba ya Serikali hakuweza kupatiwa nyumba, Serikali inao utaratibu wa kuwawezesha kutafuta makazi yao wenyewe kwa kuwalipa posho zinazostahili. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nadhani ni vema nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kutoa kauli aliyotoa kwa kiwango fulani inafafanua suala hili zima ambalo kwa maoni yangu limegubikwa na utata mwingi. Lina mambo mawili sera na utekelezaji. Sera mimi sitahoji kwa sababu sera ina mahali pake siyo hapa. Lakini utekelezaji kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri dhahiri kabisa kuna mapungufu katika utekelezaji. (*Makofi*)

Nikizingatia taarifa za magazeti za hivi karibuni ninadhani kwamba imefika wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa nakuomba uulize swali.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Umefika wakati iundwe Tume itakayobaini ukweli na kuelekeza masahihisho ya yale mapungufu yaliyojitokeza. Je, Waziri atakubaliana nami juu ya hilo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba Serikali ya awamu ya nne inaendelea kutathimini utekelezaji wa sera hii ili kubaini mapungufu ambayo yamejitokeza.

Kama nilivyosema pale ambapo mapungufu yanatokeza tunafanya marekebisho ndani ya Serikali kwa mfano kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekwishasema pale ambapo mantiki haikutumika kwa mfano kuuza nyumba ambayo iko ndani ya Kambi ya Jeshi kwa mfano Jeshi la Polisi au ndani ya hospitali ukamuuzia Mganga Mkuu nyumba ambayo iko ndani ya eneo la hospitali hapo ni kwamba mantiki haikutumika. Sasa kwenye maeneo kama hayo lazima marekebisho yafanyike na Serikali inafanya.

Mimi sidhani kwamba kuna haja ya Tume kufanya marekebisho ya mapungufu kwenye utekelezaji. Serikali imedhamiria kufanya kazi hiyo ya kurekebisha mapungufu na hakuna sababu ya Tume. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la kumuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hoja ya wananchi siyo kuuzwa au kuto kuuzwa nyumba lakini wanacholalamikia labda ni bei haikuridhisha wakati wa mauzo. Je hata hizi nyumba mpya zilizojengwa kwa mfano za Kisasa gharama ya nyumba iliyofikia itujalie ni shilingi milioni 50, akitokea mtu akanunua kwa milioni 100, je, hapo Serikali haitaweza kuuza? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nyumba ambazo ziliuzwa zile za zamani zilifanyiwa tathimini na bei ambazo ziliuziwa ni zile ambazo watalaam walizifanyia tathimini na kwa hiyo, gharama zile zilikuwa halali kulingana na hali ya nyumba zilivyokuwa. Kama ambavyo tumeeleza mara nyingi zile nyumba zilikuwa chakavu za miaka mingi. Lakini nyumba mpya ambazo zimejengwa thamani yake sasa ni milioni 50. Kama inaamua kuuzwa zitauzwa kwa bei ambayo imetumika kwa sasa baada ya kuongeza gharama za kuendesha shughuli yenyewe hiyo, kwa maana ya faida kidogo. Lakini hatuna mpango kwa kweli kuuza nyumba ambazo zimetengwa. Kama zinazungumziwa nyumba ambazo zimetengwa kwa ajili ya watumishi kama tulivyosema hatuna mpango kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi. *(Makofi)*

Na. 92

**Nafasi za Masomo ya Kuongeza Ufanisi wa Kazi kwa Wafanyakazi**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** alijibu:-

Kwa kuwa ni kweli usiopingika kuwa sababu zinazoweza kusababisha mfanyakazi wa taasisi yoyote kutekeleza majukumu aliyonayo kikazi kwa ufanisi zaidi ni pamoja na kuwapa nafasi za kusoma ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, kwa upande wa Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar ni wafanyakazi wangapi wa kike na wa kiume walipelekwa masomoni mwaka 2000 – 2005?

(b) Kati ya wafanyakazi hao, je, kila Mkoa ulitoa wafanyakazi wangapi ukijumuisha na Ofisi Kuu Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kuwa ili mfanyakazi yoyote aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ni budi kupewa mafunzo na kuendelezwa katika fani inayoendana na utendaji wa majukumu yake ya kila siku. Jukumu hili ni la msingi na linatekelezwa ipasavyo na Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2000 – 2005 Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar, imewapeleka wafanyakazi 27 masomoni kwa mchanganuo ufuatao:-

Jumla ya Maafisa Uhamiaji 14 waliopelekwa masomoni wakiwemo wanawake 2 na wanaume 12.

Jumla ya wafanyakazi wengine (*Common Cadre*) 13 walipelekwa masomoni katika kipindi hicho, wakiwemo wafanyakazi 7 wanaume na 6 wanawake.

(b) Mheshimiwa Spika, wafanyakazi waliopelekwa masomoni katika kipindi hicho kwa mchanganuo wa Mikoa wanayotoka ni kama ifuatavyo:-

- Mkoa wa Mjini Magharibi watumishi 3;
- Ofisi Kuu watumishi 19;
- Kaskazini Pemba watumishi 2;
- Kusini Pemba mtumishi 1;
- Kaskazini Unguja mtumishi 1; na
- Kusini Unguja mtumishi 1.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri yeye mwenyewe kwamba ile kumwendeleza mfanyakazi afanye kazi zake kwa ufanisi ni lazima apate masomo na kwa kuwa katika swali langu niliuliza masomo haya ya ndani na nje lakini yeye anayajibu kwa ujumla lakini hata hivyo naomba kuuliza kama Mkoa Kusini Unguja, ambao ndiyo Mkoa wangu ni kweli huko ndiyo kumwendeleza mfanyakazi kipindi cha miaka mitano awe amepelekwa masomoni mfanyakazi mmoja tu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Serikali inaona kabisa umuhimu wa kupeleka wafanyakazi wake kwenda kusoma ili kujiendeleza. Idadi ya wafanyakazi wanaopelekwa inatokana na idadi ya wafanyakazi ambao wako katika eneo hilo na kutokana na Bajeti ambayo Wizara inayo.

Ningependa kumhakikishia kwamba hakuna upendeleo katika Mkoa wowote katika Zanzibar wala hapa Bara na tutaendelea kuwasomesha wafanyakazi wote wa idara ya Uhamiaji kutokana na Bajeti na kutokana na idadi ya watu ambao wako katika maeneo husika. (*Makofi*)

Na. 93

**Uchimbaji Mdogo Mdogo wa Madini na Hifadhi ya Mazingira**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** alijibu:-

Kwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini alituma watalaam wa madini kwenda Jimboni Bumbuli kuainisha maeneo yenye madini yaliyo nje ya misitu ya hifadhi na

vyanzo vya maji ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kuyachimba na kuzingatia azma ya kuhifadhi mazingira:-

Je, ni lini taarifa ya watalaam waliofanyakazi hiyo itapatikana ili kuvunja ukimya uliopo tangu watalaam hao waende jimboni Bumbuli tarehe 23 Machi, 2005?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwezi machi, 2005, Wizara yangu ilituma watalaam kutoka 2005, Wizara yangu ilituma watalaam kutoka *Geological Survey of Tanzania (GST)* hapa Dodoma kwenda kufanya uchunguzi wa awali wa madini katika Wilaya ya Lushoto, likiwemo jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, lengo la uchunguzi huo lilikuwa ni kubaini madini yanayopatikana katika miamba iliyoko kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Lushoto na kisha kutambua maeneo yenye madini, hususan yaliyoko nje ya hifadhi ya misitu, ili kuyatenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Baada ya hapo ulifuatia uchunguzi wa kimaabara wa sampuli za miamba na mchanga wa mito zilizochukuliwa na baadaye taarifa ya kitaalamu kuandaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uchunguzi huo ilikamilika mwezi Agosti 2006. Taarifa hiyo inapatikana katika Ofisi za *Geological Survey of Tanzania (GST)* zilizoko hapa Dodoma na Mheshimiwa Mbunge atapatiwa nakala ya taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Bumbuli kwa jitihada zake anazofanya za kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo katika jimbo lake.

Aidha, Wizara inawashukuru viongozi na wananchi wa Bumbuli kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa watalaam waliokuwa jimboni kwake. Ni matumaini wadogo wadogo wataruhusiwa kuchimba aina mbalimbali za madini yaliyoko katika Jimbo la Bumbuli.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri pamoja na utekelezaji wenye kasi. Taarifa nimeipata ninayo hapa. Ila ningependa tu kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, wengine atufahamishe ni madini ya aina gani ambayo yamepatikana maana yake sijaisoma.

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba Serikali kurekebisha sheria ya madini ili kutoruhusu wawekezaji wakubwa kushiriki katika uchimbaji wa vito, vito vibaki tu kwa wananchi wa hali ya chini wazalendo. Je, hatua gani mpaka sasa hivi imeshachukuliwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa William Shellukindo kama ifuatavyo:-

Aina ya madini ambayo yamebainika kuwepo kwenye miamba iliyopo Lushoto ni kama ifuatavyo:-

Kuna *nickel,* kuna shaba, kuna vito yaani *gemstones*, kuna *marble* kuna *bauxite* na kuna *coals* pamoja na dhahabu.

Kuhusu suala la sera inayowapa wananchi uwezo wa kumiliki *gygemstone* kwa asilimia 100 kwanza ningependa nisema kwamba Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na wachimbaji wadogo wadogo wa madini katika uchumi wa nchi na maendeleo ya wananchi wake.

Lakini pili, Serikali ipo tayari kuangalia upya sera ambayo hadi sasa inawaruhusu wageni wasio wawekezaji kuwekeza katika nchi yetu, kwa sharti kwamba wawekezaji au wananchi wawe wanamiliki asilimia 25 au zaidi.

Serikali itaangalia utaratibu huu ili iweze kuona uwezekano wa wananchi wenyewe kumiliki vito hivyo kwa asilimia 100 kama wafanyavyo wenzetu wa Thailand, Srilanka pamoja na wengine. (*Makofi*)

Na. 94

**Ukamilishaji wa Miradi ya Umeme Vijijini**

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA (k.n.y. MHE. DR RAPHAEL MASUNGA CHEGENI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005 iliahidi kuendelea kukamilisha miradi ya umeme vijijini na kwa kuwa mradi wa umeme wa Lamadi, Kalemela, Nyamikoma, Nyakaboja na Nyashimo ulikuwa ni sehemu ya mpango huo kwa sababu ndicho kipande pekee kilichobaki kuunganishwa umeme kwa njia yote ya Mwanza - Musoma kupitia Bunda na kwa kuwa hata kwenye Bajeti ya 2005/2006 bado Serikali ilisisitiza nia yake ya kukamilisha mradi huo.

(a) Je, Serikali inatamka nini juu ya ukamilishaji wa mradi huo muhimu kwa wananchi wa Jimbo la Busega, hasa ikitiliwa maanani kuwa wananchi wamejenga nyumba bora na za kisasa na vile vile wanajishughulisha na kilimo, biashara na uvuvi kama sehemu ya kuinua uchumi wa nchi?

(b) Je, mpango wa kupeleka umeme kutoka Lamadi kwenda Hospitali ya Mkula na kinu cha kuchambulia Pamba cha Ngasamo, Nyashimo, Shigala na Badugu nao utatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, naomba kutoa maelekezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Lamadi hupata umeme kutoka kwenye kituo cha umeme cha Bunda ambacho kilijengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Hispania. Upelekaji wa umeme kutoka Bunda hadi Lamadi uligharamiwa na fedha za ndani. Mpango wa kupeleka umeme Vijiji vya Kalemela, Nyamikoma, Nyakaboja na Nyashimo ambavyo vipo kando kando ya barabara ya Mwanza - Musoma unalenga kuendeleza njia ya umeme ambayo kwa sasa inaishia kwenye Jineri ya Aquva.

Gharama za kupeleka umeme katika vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja ni takriban shilingi milioni 410.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kuvipatia umeme vijiji nchini, vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya Kalemela, Myamikoma, Nyakaboja na Nyashimo vimejumuishwa kwenye mpango wa upelekaji umeme vijijini ujulikanao kama *Energizing Rural Transformation* chini ya ufadhili wa Benki Kuu ya Dunia kwa kushirikiana na Serikali unaotegemewa kuanza mwaka 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama za upelekaji umeme wa gridi kutoka Lamadi hadi Hospitali ya Mkula na Kinu cha kuchambua Pamba cha Ngasamo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 420. Serikali ya Hispania imeonyesha nia ya kufadhili mradi huu chini ya mpango wa upelekaji umeme vijijini awamu ya *III C (Spanish Phese III C Funding for Rural Electrification)* ambao unategemewa kuanza katika mwaka wa fedha 2006/2007.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba ametuthibitishia kwamba vijiji hivi ambavyo vimebaki kuunganishiwa huduma ya umeme basi vitakamilishiwa huduma hiyo ndani ya kipindi cha fedha cha mwaka huu. Ningependa tu kwa faida ya wananchi wa vijiji hivyo vilivyotajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze ni lini hasa wananchi hawa watakuwa wamepatiwa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi. Wananchi wa vijiji vya Kalemela, Nyamikoma, Nyakaboja, Nanyashimo, vilio vyao vimesikika tangu mwaka 2004 na Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaingizwa kwenye utaratibu ule niliousema wa *Ernegizing Transformation* ili waweze kupatiwa umeme katika kipindi cha mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafidia muda, tulianza na maelezo fulani fulani hapa taarifa. Halafu maelezo kuhusu kanzu. Kwa hiyo, ilikula muda kidogo wa maswali. Pia naona mchangiaji kwa Maazimio ya Wizara ya Miundombinu mchangiaji ni mmoja. Kwa hiyo, hakuna hata haraka sana. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile ahadi za umeme ambazo zimetolewa huko ambako swali limeulizwa maeneo ya Bunga ni sawa na swali la Kilindi, utakumbuka Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuliahidiwa katika Bajeti iliyopita Wilaya ya Kilindi tutapewa umeme kutoka Kwediboma hadi Songe na fedha zimekwishatengwa pamoja na *transformer* katika shule ya Mkuyu.

Je, Waziri anaweza akaniambiaje maana yake hadi sasa wananchi wamekosa imani kwa sababu hata mafundi wa kupita hata gari la *TANESCO* lionekane tu linapita kupima hakuna. Je, Waziri atatuambiaje wananchi wa Kilindi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imepania kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya kuwapatia wananchi katika vijiji vyake, wala asibabaishwe na kutokuona magari yanayopita kucheki kama mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Spika, mipango inafanywa Wizarani na napenda nimhakikishie kwamba katika kipindi cha mwaka 2006/2007 utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi utaonekana kwa vitendo. *(Makofi)*

Na. 95

**Ukosefu wa Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Sikonge**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Sikonge ni moja kati ya Wilaya ambazo mpaka leo haina Kamanda wa Polisi wa Wilaya na kwa maana hiyo haina Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya.

Je, ni lini Wilaya zote nchini zitapatiwa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ili kukabiliana na matatizo mbalimbali ikiwemo lile la ujambazi ambalo wakati mwingine huhitaji huduma ya *OCD* kulikabili tatizo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze kwa vazi rasmi la eneo la pwani, ahsante sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kutaka kujenga Makao Makuu ya Polisi, kwa kila Wilaya na kuwa na uongozi kamili wa polisi akiwemo *OCD* ili kuimarisha usalama wa raia na mali zao katika maeneo yote nchini, lakini azma hiyo njema inashindwa kufikiwa kutokana na uwezo mdogo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo huo mdogo wa kifedha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa vituo hivyo vya ngazi ya Wilaya imeainisha mahitaji hayo katika mpango wa miaka kumi wa Jeshi la Polisi (2003 - 2013) ambapo jumla ya vituo vipya vya polisi 65 vitajengwa ikiwemo Wilaya ya Sikonge. Aidha, ujenzi wa vituo kama hivyo katika baadhi ya Wilaya umeshaanza na vingine vimeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mpango huo wa miaka kumi, Wizara ya Usalama wa Raia kupitia Jeshi la Polisi inaandaa mpango maalum *(Master Plan)* ili kujua mahitaji halisi ya vituo vya polisi hapa nchini kufuatana na vigezo vinavyokubalika kipolisi na mazingira ya sasa. Mara baada ya mpango huo kukamilika utawasilishwa Serikalini ili kuondoa tatizo hili kwa muda mrefu ujao.

Mheshimiwa Spika, kwa zile Wilaya mpya ambazo hazina ofisi za polisi za Wilaya zitaendelea kuhudumiwa na Wilaya mama. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kuboresha huduma katika Wilaya kwa kuongeza askari na vitendea kazi kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Wilaya mpya na kuhakikisha usalama wa raia na mali zao nchini.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri amesema kwamba katika mpango uliowekwa na Serikali kuna vituo 65 ambavyo vitajengwa katika Wilaya mbalimbali. Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kati ya vituo hivyo 65 itakuwa vyema kituo kimoja kikajengwa Wilaya ya Magharibi katika Jimbo la Dimani ambapo kumejitokeza kuwa na ghati ndogo ndogo nyingi na majambazi wanapita sehemu ile?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari Wilaya hizo zimeshaainishwa katika mpango hivyo si rahisi kumhakikishia hapa mbele kwamba na Wilaya ya Magharibi kuingizwa katika mpango huo kwa sasa. Lakini shauri lake tunalichukua tutalifanyia kazi na Serikali inaona umuhimu huo.

Na. 96

**Uhitaji wa Vituo Vidogo vya Polisi**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Vijiji vya Kimara, Kinuni, Pangawe na Kwerekwe havina vituo vidogo vya polisi; na kwa kuwa maeneo hayo yana uhalifu wa mara kwa mara.

Je, Serikali ipo tayari kujenga vituo vidogo vya polisi kwenye vijiji hivyo ili kuwepo na ulinzi wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kujenga vituo vidogo vya Polisi katika vijiji vya Kimara, Kinuni, Pangawe na Kwerekwe, kwa sasa Serikali haina uwezo wa kujenga vituo katika vijiji hivyo. Hata hivyo kwa sasa Vituo vya Mwanakwerekwe na Fuoni vitaendelea kutoa huduma ya polisi kwa vijiji hivyo. Aidha, doria na misako itaimarishwa katika maeneo husika ili kudhibiti uhalifu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali Na. 33 la Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma, nilieleza kwamba kutokana na mahitaji makubwa ya vituo vya polisi nchini na kuimarisha Jeshi la Polisi, Wizara kupitia Jeshi la Polisi wanaandaa mpango maalum *(Master Plan)* ili kujua mahitaji halisi ya vituo vya polisi nchini, kwa mujibu wa vigezo vya kipolisi na mazingira ya sasa. Mara baada ya kukamilika kwa mpango utawasilishwa Serikalini ili kuondoa tatizo hili kwa muda mrefu ujao. Hivyo naomba Waheshimiwa Wabunge, wavute subira wakati tunashughulikia kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala hili.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Pangawe pamoja na vijiji nilivyovitaja viko mbali na kituo cha Fuoni pamoja na Mwanakwerekwe; na kwa kuwa Pangawe ipo katikati ya Kinuni, Kimara, Kwerekwe, je, Naibu Waziri atakuwa tayari walau kupata kituo kimoja tu Pangawe ambacho kiwe katikati ya vijiji hivyo na kurahisisha usalama wa raia?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba uwezo wa Serikali kwa sasa ni mdogo kujenga vituo hivyo. Lakini hata hivyo Serikali inaangalia uwezekano baada ya kukamilisha ule mpango maalum nilioutaja ili kujua mahitaji halisi yanayohitajika katika kila eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu vituo vyote hivyo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, haviko mbali na vituo nilivyovitaja. Hakuna hata kimoja ambacho kitakuwa zaidi ya maili tano kutoka kituo ama cha Fuoni ama cha Mwanakwerekwe. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema tutaimarisha doria na misako katika eneo hilo kuhakikisha wananchi wa eneo hilo wako salama na pale Mheshimiwa Mbunge atakapohamasisha wananchi katika eneo hilo tuko tayari kuunga mkono jitihada hizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Matangazo machache, kwanza ninayo furaha kumtambulisha pale kwenye *Speaker's Gallery* mgeni wangu mimi ambaye ni Diwani kutoka Kata ya Songambele kule Urambo Mashariki. *(Makofi)*

Diwani Kafwenda ni mtu muhimu sana kwangu, kwa sababu nyumba yangu ya kijijini nimeijenga iko pale Songambele. Nakushukuru sana Diwani na karibu tena mara unapofika Dodoma uweze kutuona katika shughuli hizi. Natumaini utawaambia wananchi wa Songambele na Urambo Mashariki kwamba mara nyingine inakuwa vigumu Mbunge wao kufika kwa sababu ndiyo hivyo tena yuko kitini. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Wapo wageni, Madiwani 13 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea wakiongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdallah Mbinga. Ni wageni wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe.

Nawaomba wasimame. Wale pale, ahsante sana. Karibuni sana mmetoka mbali Nachingwea, karibuni hapa Dodoma, tunafurahi mara kwa mara kuwaona wawakilishi wenzetu wa ngazi muhimu sana ya Kata zetu hapa nchini. Ahsante. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Manju Msambya, Mbunge wa Kigoma Kusini, anao wageni wake ambao ni wapigakura kutoka kijiji cha Kalenge, Jimbo la Kigoma Kusini na eneo ambalo linaitwa Maswa. Naomba wasimame wale pale. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gideon Cheyo na Mheshimiwa Richard Nyaulawa wanao wageni wao kutoka Mbeya Vijijini na Ileje, ambao ni Maafisa Watendaji wa Kata mbili hizo za majimbo hayo mawili. Nawaomba wasimame wale wanaotoka kwenye Kata. Wale pale, ahsante sana. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo, yule alikuwa Mheshimiwa Gideon Cheyo yule wa Ileje, huyu sasa ni Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, ameomba niwatambulishe viongozi wa vijana wa *UDP* kutoka Jimboni kwake, Triphone Makoye na Suzan Makoye. Mmoja yupo pale. Karibu sana. *(Makofi)*

Mwisho lakini siyo padogo, tunao wanafunzi 50 na walimu wawili wa Shule ya Msingi ya Amani Mjini Dodoma, wamekuja kujifunza shughuli za Bunge, bila shaka wanao walimu wao. Nawaomba vijana pale mlipo msimame, wale pale. Karibuni sana na tunawapongeza walimu kwa utaratibu huu wa kuiona hali halisi ya uendeshaji wa Bunge

katika nchi yetu. Natoa mwito kwa wenzao hasa zile Wilaya za karibu hapa wafanye hivyo hivyo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wafanyakazi 35 wa Benki ya Posta, *Western Union* nchini wamekuja nao kujionea shughuli za Bunge. Wafanyakazi wa *Western Union* Benki ya Posta. Karibuni sana hapa Ukumbini, tunafurahi ni haki yenu kama raia kuweza kuwa hapa na kuona shughuli za demokrasia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo ya utambulisho lakini Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi au Uchumi na Fedha ameniomba nitangaze kwamba leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 428. Kamati ya Uchumi na Fedha au Kamati ya Fedha na Uchumi chumba namba 428 saa 5.00 asubuhi pale jengo la Utawala.

Pia Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba Wajumbe wake wa Kamati hiyo ya Katiba, Sheria na Utawala wakutane saa 5.00 asubuhi hii katika ukumbi namba 219 jengo la Utawala. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala saa 5.00 asubuhi, ukumbi namba 219. Ahsante sana na huo ni mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**Mkataba wa Kimataifa wa Mwaka 1965 Kuhusu Taratibu za Kuhudumia Meli za Kimataifa Zinazobeba Mizigo na Abiria Zikiwa Bandarini *(International Martime Traffic, 1965)***

**Mkataba wa *ICAO* wa Mwaka 1944 Kuhusu Kuruhusu Ndege za Kimataifa Zenye Ratiba Kupitia Kwenye Anga ya Nchi Nyingine Bila Kutua kwa Sababu zisizo za Kibiashara *(International Air Service Transit Agreement (IASTA) of 1944)***

**Mkataba wa Uzuiaji Uchafuzi wa Bahari kwa Njia ya Utupaji Taka na Bidhaa Nyingine wa Mwaka 1972 *(Ratification of The Conventoin on Previntion of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and other Matters, 1972)***

**Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira na Bahari Kutoka Melini *(International Convention for the Prevention of Pollution from the Ships, (Marpol 1973/1978)***

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maazimio manne kwa madhumuni ya kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mikataba minne ya Kimataifa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

Mkataba wa kwanza ni Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1965 kuhusu Taratibu za Kuhudumia Meli za Kimataifa zinazobeba Mizigo na Abiria zikiwa Bandarini yaani *Internatinal Convention on Facilitation of International Maritime Traffic of 1965.*

Mkataba wa pili, ni Mkataba wa *ICAO* wa mwaka 1944 kuhusu Kuruhusu Ndege za Kimataifa zenye Ratiba Kupita kwenye Anga ya Nchi Nyingine bila Kutua kwa sababu zisizo za Kibiashara yaani *International Air Services Transit Agreement (IASTA) of 1944.*

Mkataba wa tatu, ni Mkataba wa Uzuiaji, Uchafuzi wa Bahari kwa Njia ya Utupaji Taka na Bidhaa nyingine wa mwaka 1972 yaani *The Conventin on Prevention of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and other Matters of 1972.*

Mkataba wa nne na wa mwisho ni Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari kutoka Melini yaani *The International Convention on the Prevention of Pollution from Ships, (Marpol)* ya mwaka 1973 kama ilivyorekebishwa mwaka 1978.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kwanza yaani huu Mkataba wa kuhudumia meli zenye safari za Kimataifa zinazobeba mizigo na abiria zikiwa bandarini uliwekwa saini mwaka 1965 na ulianza kutumika rasmi tarehe 5 Machi, 1967. Makubaliano ya kuwa mkataba huo yalifikiwa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu usafiri wa Kimataifa na utalii uliofanyika mjini Rome mwaka 1963 na kukubaliwa na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia usafiri wa majini yaani *International Maritime Organization (IMO)* mwaka 1965.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya mkataba huu ni kusimamia hudumia zinazotolewa kwa meli zenye safari za Kimataifa zinazobeba mizigo na abiria zikiwa bandarini. Madhumuni ya mkataba huu ni pamoja na kusisitiza ushirikiano wa nchi wanachama wa mkataba huo katika kupunguza urasimu wa kushughulikia meli zenye safari za Kimataifa zinapoingia, kukaa na kuondoka bandarini. Pili, uhuru wa nchi mwanachama kuwa na viwango vya huduma vilivyo juu zaidi ya viwango vilivyokubaliwa kwenye mkataba huu ili mradi vinaboresha dhana na madhumuni ya mkataba huo.

Tatu, mkataba unatoa uhuru kwa nchi mwanachama kutumia kanuni zake kwa manufaa ya nchi yake hususan kama zile zinazohusu maadili, ulinzi na usalama na kuzuia uingizaji na kuenea kwa magonjwa au kuingiza wadudu wanaoathiri afya za binadamu, wanyama na mimea.

Nne, kuweka taratibu za kufuatwa na nchi wanachama ili kutoa mapendekezo yake kwa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia usafiri wa majini *(IMO)* kama kuna ugumu wa kutekeleza viwango vilivyowekwa na mahitaji yaliyomo kwenye mkataba na tano, mkataba unatoa fursa kwa nchi mwanachama wa kujitoa uanachama miaka minne baada ya kuridhia mkataba huo na hatua za kufuatwa katika kujitoa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya viwango vya ubora wa huduma zinazotakiwa kutolewa katika Bandari kwa mujibu wa mkataba huu ni pamoja na bandari kutumia muda mfupi katika kuhudumia meli ili kupunguza gharama na kuongeza tija. Kimsingi meli hutumia gharama kubwa za uendeshaji zikiwa hapo bandarini na kuondoka mapema kwa meli hizo bandarini kunaongeza tija ya kufikisha mizigo na abiria mapema kule meli iendako na hivyo kuendelea kuwa na usafiri unaoaminika na wenye gharama nafuu duniani.

Pili, nahodha wa meli kuwa na nyaraka zote muhimu za abiria au za mizigo zinazoeleweka kwa urahisi na zenye viwango vinavyokubalika ili kuwezesha meli kuhudumiwa haraka.

Tatu, kuwepo na taratibu rahisi zinazopunguza urasimu kwa mujibu wa matakwa na mahitaji ya nchi zenye bandari.

Nne, kuwa na taratibu zinazowezesha meli zenye matatizo au dharura kupata huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu umechelewa kuridhiwa na nchi yetu kwa sababu wakati unaanza kutumika bandari zetu zilikuwa hazitembelewi na meli nyingi kubwa za Kimataifa na hivyo ziliweza kuhudumiwa meli ambazo zilikuwa zinaingia nchini kwenye bandari zetu ziliweza kuhudumiwa kulingana na taratibu zilizokuwepo wakati huo. Hivi sasa bandari zetu zinapokea meli nyingi za Kimataifa na kutokana na utandawazi pamoja na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano duniani hasa kunawezesha mamlaka za bandari kuweza kupata nyaraka za meli mapema kabla meli haijafika bandarini na hivyo kuweza kuhudumia meli haraka, kwa ufanisi mara inapowasili na hapo inaposubiri kuondoka kwenye bandari husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia mkataba huu Tanzania itapata faida zifuatazo:-

(a) Kutumia nyaraka chache na zenye viwango na mahitaji yanayofanana Kimataifa na rahisi kueleweka kwa watumiaji ili kuongeza kasi ya kuhudumia meli na hivyo kupunguza muda wa meli kuingia, kukaa na kuondoka bandarini.

(b) Kuwa na ufanisi na gharama nafuu katika matumizi ya bandari zetu na hivyo kuweza kuvutia nchi nyingi kupitisha mizigo yake katika bandari zetu. Kitu ambacho kitasaidia kuinua uchumi wetu.

(c) Kuwezesha bandari zetu kutumia mawasiliano yenye teknolojia ya kisasa inayowezesha maingiliano na bandari nyingine duniani kwa kutumia mtandao wa mawasiliano na taraklishi kama inavyopendekezwa na *United National Conference on Trade and Development (UNCTD). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya kuridhia na kujiunga na mkataba huu ni kubwa. Serikali inapendekeza kwamba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba huo wa Kimataifa kuhusu taratibu za kuhudumia meli zenye safari za kimataifa

zinazobeba mizigo na abiria zikiwa bandarini wa mwaka 1965 yaani *The Internatinal Convetion on the Infacilitation of International Maritime Traffic of 1965.*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome Azimio la kuliomba Bunge lako Tukufu ili iridhie Mkataba huu.

KWA KUWA nchi wanachama wa Mkataba wa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia usafiri wa majini *(Internatinal Maritime Organization -IMO)* zilikubaliana kuanzisha Mkataba wa Kimataifa unaoweka taratibu za kuhudumia meli za abiria na mizigo zinazofanya safari za Kimataifa zinapokuwa bandarini wa mwaka 1965; na

KWA KUWA madhumuni ya Mkataba huo ni kuboresha huduma zinazotolewa kwa meli za Kimataifa zinazobeba mizigo na abiria zikiwa bandarini; na

KWA KUWA viwango vya ubora wa huduma vinavyotakiwa kutolewa katika bandari kwa mujibu wa mkataba huo ni pamoja na bandari kutumia muda mfupi katika kuhudumia meli ili kupunguza gharama na kuongeza tija. Nahodha wa meli kuwa na nyaraka zote muhimu za abiria au mizigo zinazoeleweka kwa urahisi na zenye viwango vinavyokubalika ili kuwezesha meli kuhudumiwa haraka. Kuwepo taratibu rahisi zinazopunguza ukiritimba na urasimu kwa mujibu wa matakwa na mahitaji ya nchi zenye bandari kuwepo na taratibu zinazowezesha meli zenye matatizo au dharura kupata huduma kwa haraka; na

KWA KUWA faida ya kukubali na kujiunga na mkataba huu ni pamoja na kutumia nyaraka chache na zenye viwango na mahitaji yanayofanana Kimataifa na rahisi kueleweka kwa watumiaji ili kuongeza kasi ya kuhudumia meli kwa kupunguza meli kuingia, kukaa na kuondoka kwenye bandari, kuwa na ufanisi na gharama nafuu katika matumizi ya bandari zetu na hivyo kuweza kuvutia nchi nyingi kupitisha mizigo yake katika bandari zetu hali ambayo itainua uchumi wetu, kuwezesha bandari zetu kutumia mawasiliano yenye teknolojia inayowezesha maingiliano na bandari nyingine duniani kwa kutumia mtandao wa mawasiliano na taraklishi kama inavyopendekezwa na *United Nations Conference and Trade and Development* yaani *UNCTD;* na

KWA KUWA sababu zilizofanya Tanzania kutoridhia mkataba huo sasa hazipo tena; na

KWA KUWA masharti ya Mkataba ni kwa nchi mwanachama wa *IMO* kukubali na kuridhia mkataba huu kwa kutumia taratibu za nchi husika;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia manufaa na faida ya mkataba huu Bunge hili katika Mkutano wa Tano kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaazimia kwamba linaridhia Tanzania kujiunga na Mkataba wa Kimataifa unaohusu Taratibu za Kuhudumia Meli za Kimataifa

zinazobeba Mizigo na Abiria zikiwa Bandarini wa mwaka 1965 yaani *The International Convention on Facilitation of International Maritime Traffic* wa mwaka 1965.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mkataba wa *ICAO* wa Mwaka 1944 Kuhusu Kuruhusu Ndege za Kimataifa Zenye Ratiba Kupitia Kwenye Anga ya Nchi Nyingine Bila Kutua kwa Sababu zisizo za Kibiashara *(International Air Service Transit Agreement (IASTA) of 1944)***

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Mkataba wa pili, ni Mkataba unaohusu *International Service Transit Agreement*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Usalama wa Usafiri wa Anga *the International Civil Aviation Organization (ICAO)*. Shirika hilo ndilo linalosimamia usalama wa usafiri wa anga duniani kwa kuhakikisha kuwa usafiri kwa njia ya anga unaendeshwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Chicago wa mwaka 1944 *the Chigaco Convention of 1944*. Wakati Mkataba wa Kuanzisha *ICAO* uliposainiwa mwaka 1944. Ulisainiwa pia Mkataba mwingine wa kuruhusu ndege zenye safari ya Kimataifa na zenye ratiba *(scheduled airlines)* kupitia kwenye anga la nchi nyingine bila kutua *(International Air Services Transit Agreement, 1994)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya kuanzishwa kwa Mkataba huo ni kuwezesha ndege za safari za Kimataifa kupitia kwenye anga ya nchi nyingine bila ulazima wa kuwepo Makubaliano kati ya nchi mbili husika *(Bilateral Air Service Agreements - BASA)* na hivyo kuimarisha usafiri wa anga. Safari za ndege zinazohusika ni zile za kibiashara zenye na ratiba. Safari nyingine zote za ndege ambazo hazina ratiba zitatumia utaratibu wa kuomba vibali maalum kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, *ICAO* imekuwa ikihimiza nchi wanachama kuridhia Mkataba huo ili kurahisisha usafiri wa anga kati ya Mataifa. Hata hivyo, Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola na zile za uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika *(OAU)* ambazo hazikuridhia au kukubali Mkataba huo kutokana na msimamo wa nchi hizo kuhusu Afrika ya Kusini wakati huo siasa ya ubaguzi na haraka za ukombozi katika eneo la Kusini mwa Afrika.

Hivyo uhuru wa kuruhusu ndege zenye safari za Kimataifa ulisimamiwa na kuruhusiwa kwa kutumia makubaliano kati ya nchi mbili husika kupitia *Bilateral Air Service Agreements (BASA)* kwa nchi zote wananchama wa *ICAO* ambazo zilikuwa hazijaridhia Mkataba huo Kimataifa *IASTA*. Kwa kuwa sababu zilizofanya Tanzania kutoridhia Mkataba huo sasa hazipo tena ni vema sasa Tanzania ikajiunga na Jumuiya ya Kimataifa kwa nchi ambazo zimeridhia Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, Mkataba una maeneo mawili muhimu, sehemu ya kwanza inahusu kubadilishana uhuru wa ndege kupita bila kutua *(over fly)* na sehemu ya pili inahusu kubadilishana uhuru wa ndege kutua kwa sababu zisizo za kibiashara yaani

*for technical reasons* kama vile kujaza mafuta lakini bila kuchukua au kushusha abiria. Faida za kuridhia Mkataba huo ni pamoja na:-

(a) Kurahisisha upangaji wa safari za ndege kwani Mkataba huo unawezesha kuwepo kwa uhakika kwa nchi mwanachama wa *ICAO* kutumia anga ya nchi mwanachama bila hofu ya kukataliwa, baada ya kutoa taarifa za kutosha kufuatana na masharti yaliyowekwa na nchi husika.

(b) Ndege za nchi mwanachama zinapata uhuru wa kuruka juu ya anga la nchi nyingine wanachama zaidi ya mia moja ambao ni wanachama zilizoridhia tayari Mkataba huu na hivyo kuwezesha kurahisisha usafiri wa anga kati ya Mataifa.

(c) Mkataba huu utapunguza muda wa majadiliano kati ya nchi mbili *(bilateral negotiations)* kuhusu safari zenye ratiba za mashirika ya ndege kati ya Serikali mbili kama inavyofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, ili Tanzania iweze kunufaika na Mkataba huu ni sharti iukubali na kuuridhia kupitia Bunge lako Tukufu na hivyo ndivyo Mkataba unavyotaka katika Ibara ya Sita ya Mkataba. Ni kwa msingi huo, Serikali inapendekeza Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisome Azimio linalopendekezwa na Serikali kwa madhumuni haya.

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani yaani *The International Civil Aviation Organization (ICAO),* ambalo shughuli na taratibu zake huendeshwa kwa mujibu wa Mkataba uliosainiwa Chicago, Marekani tarehe 7 Desemba, 1944 ambao ndio Katiba ya Shirika hilo inayodhibiti na kusimamia uwajibikaji wa nchi wanachama wa Shirika hilo katika masuala yahusuyo Usalama wa Usafiri wa Anga;

NA KWA KUWA wakati Mkataba wa kuanzisha *ICAO* uliposainiwa mwaka 1944, ulisainiwa pia Mkataba mwingine wa kuruhusu ndege zinazofanya safari za Kimataifa zenye ratiba *schedules airlines* kupita kwenye anga la nchi nyingine bila kutua *International Air Services Transit Agreement, 1944*;

NA KWA KUWA Tanzania na baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola na zile za uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika *(OAU)* ambazo hazikuridhia au kukubali Mkataba huo kutokana na msimamo wa nchi hizo kuhusu Afrika Kusini na harakati za ukombozi katika eneo la Kusini mwa Afrika, na hivyo uhuru wa kuruhusu ndege zenye safari za Kimataifa ulisimamiwa na kuruhusiwa kwa kutumia Makubaliano kati ya nchi mbili husika *Bilateral Air Service Agreement (BASA);*

NA KWA KUWA sababu zilizofanya Tanzania kutoridhia Mkataba huo sasa hazipo tena;

NA KWA KUWA faida kubwa ya kuridhia Mkataba huo ni pamoja na:-

(a) Kurahisisha upangaji wa safari za ndege zenye safari za Kimataifa.

(b) Nchi mwanachama kupata haki kwa ndege zake zenye safari ya Kimataifa ya kuruka juu ya anga ya nchi zaidi ya mia moja zilizoridhia Mkataba huo na hivyo kuweza kurahisisha usafiri wa anga kati ya Mataifa.

(c) Kupunguza muda wa majadiliano *(bilateral negotiations)* kati ya nchi mbili kuhusu safari zenye ratiba za Mashirika ya Ndege kati ya Serikali mbili husika kama inavyofanyika sasa.

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia manufaa ya Mkataba huu, na faida ya kukubali na kuuridhia, Bunge hili katika Mkutano wa Tano kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kwamba linakubali na kuridhia Tanzania kuwa mwanachama wa Mkataba wa kubadilishana uhuru wa kuruhusu ndege zenye safari za Kimataifa zenye ratiba kupita kwenye anga la Tanzania bila kutua au kutua kwa sababu za kiufundi *(International Air Services Transit Agreement of 1944)* uliosainiwa tarehe 7 Desemba, 1944.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mkataba wa Uzuiaji Uchafuzi wa Bahari kwa Njia ya Utupaji Taka na Bidhaa Nyingine wa Mwaka 1972 *(Ratification of The Conventoin on Previntion of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and other Matters, 1972)***

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Tatu ni Mkataba wa mwaka 1972 unaozuia Uchafuzi wa Bahari kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine yaani *the Convention on Prevention of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and other matters of 1972. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Kimataifa la kusimamia usalama wa usafiri wa majini *(the International Maritime Organization - IMO)* mwaka 1972 liliandaa Mkataba wa Kimataifa wa kuzuia uchafuzi wa bahari kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine. Hatua hii, ilitokana na matukio ya uchafuzi wa bahari unaoleta madhara makubwa kwa viumbe vinavyoishi ndani ya bahari ambavyo ni muhimu kwa manufaa ya uhai wa binadamu.

Mkataba huu uliandaliwa kwa kuzingatia uchafuzi wa majini unaotokana na shughuli mbalimbali za binadamu majini na hewani na hivyo kuona umuhimu wa kila nchi kutumia mbinu zilizo bora ili kuzuia uchafuzi huo. Mkataba huu kwa hivi sasa una wanachama 78 kati ya wanachama 166 wa *IMO.*

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu ya Mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya I inataka kila nchi mwanachama kwa peke yake au kwa pamoja na nchi nyingine wanachama iweke mikakati ya mahsusi ya kuzuia utupaji wa taka baharini ambazo zinaleta madhara kwa afya ya binadamu na viumbe vya baharini na kuharibu mali au kuingilia kati matumizi mengine ya bahari

(ii) Ibara ya II inataka nchi mwanachama, kama ilivyoelekeza katika Ibara ya kwanza, iweke mikakati endelevu ya sayansi na teknolojia itakayosaidia kuzuia uchafuzi wa mazingira wa bahari kwa kutupa taka na kuhakikisha kwamba sera za nchi wanachama zinatilia maanani suala hili.

(iii) Ibara ya IV ya Mkataba inaelezea taratibu na masharti ya kufuata na aina ya taka zinazotakiwa kutupwa baharini kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba. Aidha, Mkataba unaitaka nchi mwanachama kuteua chombo kitakachosimamia utoaji wa vibali maalum vitakavyoruhusu kutupa taka hizo kama ilivyoainishwa katika Ibara ya VI ya Mkataba pamoja na wajibu wa chombo hicho wa kutunza taarifa za aina na idadi ya taka zinazoruhusiwa kutupwa na mahali pa kuzitupa.

(iv) Ibara ya VII inataka nchi mwanachama kuandaa taratibu zitakazofuatwa na meli zote pamoja na ndege zinazoruka katika anga ya nchi mwanachama katika kutekeleza Mkataba huu.

(v) Ibara ya VII(3) inataka kuwepo na utaratibu maalum wa namna ya kuwasiliana baina ya nchi wanachama kuhusu namna ya kudhibiti meli au ndege zitakazogundulika kutupa taka baharini kinyume na Mkataba huu.

(vi) Ibara ya IX inaelezea kwamba katika kutekeleza Mkataba huu nchi mwanachama kwa ushirikiano kupitia Shirika au Mashirika ya Kimataifa inatakiwa kuhamasisha na kushirikiana na nchi nyingine wanachama ili kupata msaada wa mafunzo katika fani ya kisayansi na teknolojia kwa wafanyakazi wao, kupata vifaa vya utafiti na usimamizi wa namna ya kutupa au kuharibu taka na mikakati mingine ya mbinu za kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari unaosababishwa na utupaji taka.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa haijajiunga na Mkataba huu kutokana na kutokuwa na chombo cha kusimamia na kudhibiti usalama wa usafiri wa majini na utunzaji wa mazingira ya bahari. Sasa tunacho chombo cha *SUMATRA* na Serikali inaendelea kukisimamia na kukiimarisha chombo hiki. Aidha, nchi yetu sasa inao wataalam wenye ujuzi, uwezo na uzoefu wa ksimamia utekelezaji wa Mkataba huu na ambapo hatutakuwa na wataalam hao tutaweza kuwapata kokote ambako tunaweza kuwapata ambapo baada ya kuupitia, inaonekana katika hali hiyo kuna umuhimu wa kuuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia Mkataba huu Tanzania itapata faida zifuatazo:-

(a) Kuwa na uwezo wa kisheria wa kuzuia na kudhibiti utupaji hovyo wa taka za mafuta na kemikali ya sumu.

(b) Kuwa na uwezo wa kisheria kuzuia uharibifu wa mazingira na kudhibiti uhai wa viumbe vya baharini katika Pwani ya nchi yetu.

(c) Kupata fidia kutokana na madhara yanayosababishwa na utupaji wa taka za mafuta na kemikali za sumu katika eneo la bahari ya nchi yetu.

(d) Kupata msaada wa kujenga uwezo wa wataalam wa masuala ya utunzaji wa mazingira.

(e) Kupata msaada wa vifaa muhimu na nyenzo za kufanyia utafiti, kuzuia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba sasa nisome Azimio la kuridhia Mkataba huu.

KWA KUWA Shirika la Kimataifa la Kusimamia Usalama wa Usafiri wa Majini *(International Maritime Organization - IMO)* liliandaa Mkataba wa Uzuiaji wa Uchafuzi wa Bahari kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine mwaka 1972, kwa lengo la kukabiliana na matukio ya uchafuzi wa bahari unaoleta madhara makubwa kwa viumbe vinavyoishi ndani ya bahari ambavyo ni muhimu kwa manufaa ya uhai wa binadamu;

NA KWA KUWA Mkataba huu uliandaliwa kwa kuzingatia uchafuzi wa majini unaotokana na shughuli mbalimbali kupitia kwenye maji na kwenye hewa na hivyo kuona umuhimu wa kila nchi kutumia mbinu zilizo bora ili kuzuia uchafuzi huo;

NA KWA KUWA faida ya kukubali kujiunga na Mkataba huo ni pamoja na :-

(a) Kuwa na uwezo wa kisheria kuzuia na kudhibiti utupaji wa taka za mafuta na kemikali ya sumu na bidhaa nyingine.
(b) Kuwa na uwezo wa kisheria kuzuia uharibifu wa mazingira na kudhibiti uhai wa viumbe vya baharini katika pwani ya nchi yetu.

(c) Kupata fidia kutokana na madhara yanayosababishwa na utupaji wa taka za mafuta na kemikali za sumu.

(d) Kupata msaada wa kuweza kuwafundisha wataalamu wetu kwa masuala ya utunzaji wa mazingira.

(e) Kupata msaada wa vifaa muhimu na nyenzo za kufanyia utafiti, kudhibiti na kuzuia uchafuzi wa mazingira.

NA KWA KUWA Tanzania inaona sasa ipo haja na umuhimu wa kujiunga na Mkataba huo.

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia manufaa ya Mkataba huu na faida ya kukubali na kuuridhia Bunge hili katika Mkutano wa Tano kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 sasa linaazimia Tanzania kujiunga na Mkataba wa uzuiaji uchafuzi wa bahari kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine wa mwaka 1972 *the Convention on Prevention of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and other matters 1972.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira na Bahari Kutoka Melini *(International Convention for the Prevention of Pollution from the Ships, (Marpol 1973/1978)***

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Nne na wa mwisho ni Mkataba wa Kimataifa kuhusu Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari kutoka Melini Mwaka 1973 kama ulivyorekebishwa mwaka 1978, *the International Convention for the Prevention of Pollution from Ships Marpol of 1973/1978.*

Mheshimiwa Spika pamekuwepo na matukio mengi duniani ya uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na mafuta yasiyosafishwa, mafuta ya petroli yaliyosafishwa, kemikali za sumu, taka ngumu ya binadamu, hewa kutokana na moshi unatoka kwenye injini za meli, mabaki ya vyakula kutoka kwenye meli kumwagwa baharini na hivyo kuharibu mazingira ya bahari na kudhuru viumbe vya baharini. Ili kukabiliana na tatizo hili, mwanzoni mwa mwaka 1970 , Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Usalama wa Usafiri Majini *(IMO),* iliandaa Mkataba wa Kimataifa kwa madhumuni ya kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari kutoka kwenye meli *(International Convention for the Prevention of Pollution from Ships, 1973/1978).*

Mkataba huu ulisainiwa mwaka 1973 na baadaye ulifanyiwa marekebisho kupitia Itifaki ya Umoja huo ya mwaka 1978. Lengo la Mkataba huo ni kuboresha na kulinda mazingira ya bahari, viumbe na maliasili nyingine zilizoko baharini kutokana na mafuta, kemikali za sumu, karatasi za plastiki, taka ngumu ya binadamu, hewa inayotokana na moshi na mabaki ya vyakula kumwagwa baharini.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu ya Mkataba huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Chini ya Mkataba huo, nchi mwanachama ina jukumu la kuhakikisha kuwa Mkataba huo unatekelezwa ili kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari katika eneo la bahari lililo chini ya mamlaka yake.

(b) Nchi wanachama kushirikiana kwa pamoja ili kubaini matukio ya ukiukwaji wa Mkataba huo na pia kutekeleza Mkataba huo kwa kuweka mikakati ya kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari pamoja na kuweka taratibu za kufuatilia ushahidi wa tukio lolote la uchafuzi wa mazingira baharini.

(c) Mkataba huo unatoa fursa kwa nchi mwanachama kuweza kunufaika na misaada mbalimbali ya kiufundi.

(d) Itifaki ya mwaka 1978 ambayo ilifanya marekebisho kwenye Mkataba mama ina lenga katika kuimarisha juhudi za kuzuia na kudhibiti uchafuzi wa bahari unaotokana na meli kumwaga uchafu baharini hasa kutoka kwenye meli kubwa *(oil tankers)* zinazobeba mafuta ghafi na mafuta ya petroli yaliyosafishwa, kemikali za sumu , hewa chafu inayotokana na moshi wa injini za meli, chupa na makaratasi ya nailoni, plastiki, mabaki ya vyakula na uchafu unaotoka kwenye vyoo vya vyombo hivyo yaani meli na kuweza kuzifanyia kazi kanuni zinazozuia uchafuzi huo.

(e) Nchi mwanachama inapaswa kuwasiliana na *IMO* kuhusu sheria na kanuni zake ambazo zinatumika kudhibiti uchafuzi wa bahari pamoja na vyeti vinavyotolewa kulingana na kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa haijajiunga na Mkataba huu kutokana na gharama kubwa zinazotakiwa katika utekelezaji wa Mkataba huu. Kwa sasa Serikali inaona iko tayari tumeishaunda chombo cha usimamizi na udhibiti wa masuala ya Usalama wa Usafiri Majini *(SUMATRA),* kama nilivyosema Serikali itaendelea kukiimarisha chombo hiki. Sasa hivi tuna wataalam ambao wana ujuzi, uwezo na uzoefu wa kutekeleza Mkataba huo ambao tunaona sasa mazingira ni mazuri ya kuweza kupendekeza kuridhia Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu ni nchi yenye mwambao mrefu wa bahari ambao meli zenye safari za Kimataifa na meli za hapa nchini zinazobeba bidhaa mbalimbali yakiwemo mafuta machafu na mafuta yasiyosafishwa na bidhaa ambazo zinaweza kuleta madhara baharini meli hizo zinapita, hivyo kuwepo uwezekano mkubwa wa uchafuzi wa bahari kutoka melini. Kwa kujiunga na Mkataba huu, Tanzania itapata faida zifuatazo:-

(a) Tanzania itakuwa na mwongozo wa kisheria wa namna ya kukabiliana na meli zinazochafua mazingira ya bahari kwa makusudi au kwa kukiuka taratibu za utupaji wa taka baharini;

(b) Wenye meli watalazimika kuchukua tahadhari zaidi za kuzuia majanga kutokea kwenye eneo la ukanda wa bahari wa nchi yetu na hivyo kulinda mazingira ya bahari kwenye eneo hilo;

(c) Kupata misaada ya mafunzo na misaada kiufundi na ya kisayansi na kiteknolojia na hivyo kujenga uwezo wa kudhibiti na kukabiliana na uchafuzi wa mazingira ya bahari yanayosababishwa na meli kumwaga takataka baharini.

(d) Kupata ushirikiano wa Kimataifa katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya bahari pamoja na wale wanaochafua mazingira ya bahari kwa makusudi;

(e) Kupata ujuzi na utaalam wa namna ya kujiandaa na matukio ya umwagikaji wa mafuta baharini yaani *pollution;* na

(f) Kuwa na chombo au eneo la kuhifadhia uchafu unaotoka kwenye meli *(reception facilities)* badala ya kumwaga uchafu baharini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya kuridhia Mkataba huu ni kubwa, Serikali inaliomba Bunge lako Tukufu likubali Tanzania kujiunga na Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira ya Baharini kutoka Melini wa mwaka 1973 kama ulivyorekebishwa mwaka 1978. *(The International Convention for the Prevention of Pollution from Ships Marpol 1973/1978)*

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako sasa naomba nisome Azimio kwa madhumuni haya.

KWA KUWA pamekuwepo na matukio mengi duniani ya uchafuzi wa mazingira ya bahari unaotokana na uchafu wa mafuta, kemikali ya sumu, uchafu unaotoka kwenye vyoo vya meli hizo, hewa kutokana na moshi, mabaki ya vyakula kutoka kwenye melini na kumwagwa baharini na hivyo kuharibu mazingira ya bahari na kudhuru viumbe vya baharini;

NA KWA KUWA ili kukabiliana na tatizo hili, uliandaliwa Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1973/1978 unaohusu kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari kutoka kwenye meli *(International Convention for the Prevention of Pollution from Ships, 1973/1978),* Mkataba huo ambao ulisainiwa mwaka 1973 na baadaye kurekebishwa kupitia itifaki mwaka 1978;

NA KWA KUWA lengo la Mkataba huu ni kuzuia uchafuzi wa mazingira unaotokana na kumwaga baharini mafuta, kemikali ya sumu, karatasi za plastiki, uchafu wa vyooni, hewa inayotokana na moshi na mbaki ya vyakula;

NA KWA KUWA Tanzania ni nchi yenye mwambao mrefu wa bahari ambao meli za Kimataifa na za hapa nchini zinazobeba bidhaa mbalimbali zikiwemo mafuta machafu na ambazo zinaweza kuleta madhara baharini zinapita, hivyo kuwepo uwezekano wa uchafuzi mkubwa wa bahari kutoka melini;

NA KWA KUWA faida ya kujiunga na Mkataba huu ni pamoja na Tanzania kuwa na mwongozo wa kisheria wa namna ya kukabiliana na meli zinazochafua mazingira ya bahari kwa makusudi au kwa kukiuka taratibu za utupaji wa taka baharini; wenye meli kulazimika kuchukua tahadhari zaidi za kuzuia majanga kutokea kwenye eneo la ukanda wa bahari wa nchi yetu; kupata misaada wa mafunzo ya kisayansi, kiteknolojia na kiujuzi ya kudhibiti na kukabiliana na uchafuzi wa mazingira ya bahari, kupata ushirikiano wa Kimataifa katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya bahari pamoja na wale wanaochafua mazingira ya bahari kwa makusudi; kupata ujuzi na utaalam wa namna ya kujiandaa na matukio ya umwagikaji wa mafuta baharini; na kuwa na vyombo vya kuhifadhia uchafu unaotoka kwenye meli *(reception facilities)* badala ya kumwaga uchafu baharini;

NA KWA KUWA masharti ya kujiunga na Mkataba huu ni kwa nchi wanachama kuuridhia;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia manufaa ya Mkataba huu, na faida ya kukubali na kuuridhia, Bunge hili katika Mkutano wa Tano kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kwamba linaridhia Tanzania kujiunga na Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1973 kama ulivyorekebishwa mwaka 1978 unaohusu Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari kutoka Melini *(The International Convention for the Prevention of Pollution from Ships (MARPOL 1973 as amendmend 1978). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu au mwakilishi wake kwa ajili ya Taarifa ya Kamati kuhusu hoja ya Maazimio haya ya Mikataba, naomba tu kwa taarifa ya Bunge kwa sababu wakati wote linakuwa na viongozi humu ndani wa pande zote mbili, kwamba Mheshimiwa Kingunge Ngambale-Mwiru ndiye anakaimu Uongozi wa Shughuli za Serikali hivi sasa humu ndani na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, anakaimu shughuli za Kambi ya Upinzania humu ndani.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu au mwakilishi wake ili awasilishe taarifa yake. Ni mwakilishi wake. *(Makofi)*

**MHE. MWAKA ABDULRAHMAN RAMADHAN (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, nachukua fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Mikataba ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 63 (3) (e) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinaainisha kuwa Bunge litajadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano, ambayo kwa masharti yake inapaswa kuridhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niitumie nafasi hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa wagombea wa nafasi za Uwakilishi wa Ubunge katika Bunge la Afrika Mashariki walioibuka washindi katika uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, aliyeibuka mshindi katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa kumpata Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ambao pia ulifanyika mwishoni mwa wiki iliyopita hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati yangu nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Andrew John Chenge, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Miundombinu, Kamati yangu inaahidi kumpa ushirikiano katika kusukuma mbele maendeleo ya Taifa hili. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Mawaziri wengine ambao wameteuliwa kushika Wizara mbalimbali katika mabadiliko yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 88 (9) ya mwaka 2004, Kamati ya Bunge ya Miundombinu ilipata fursa ya kuipitia Mikataba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Naibu Waziri wa Miundombinu mbele ya Kamati ili kujadiliwa na kupata maoni na ushauri wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili na kuridhia Mikataba na makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, Mikataba iliyopitiwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

(i) Mkataba wa kubadilishana uhuru wa kuruhusu ndege za Kimataifa zenye ratiba kupita kwenye anga la nchi nyingine bila kutua ama kutua kwa sababu zisizo za kibiashara *(International Air Services Transit Agreement (IASTA) signed on 7 December, 1944).*

(ii) Mkataba wa mwaka 1972 unaohusu uzuiaji uchafuzi wa Bahari kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine *(The Convention on Prevention of Marine Pollution by Dumping of wastes and other matters 1972).*

(iii) Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1973/1978 kuhusu kuzuia uchafuzi wa Mazingira ya Baharini kutoka Melini *(International Convention for the Prevention of Pollution from Ships, MARPOL 1973/1978),* na

(iv) Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1965 unaohusu taratibu za kuhudumia Meli za Kimataifa zinazobeba mizigo na abiria zikiwa Bandarini *(International Convention on Facilitation of International Maritime Traffic, 1965).*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 88(9) ya mwaka 2004, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyowasilishwa na Serikali kama ilivyotajwa hapo juu pamoja na kwamba Kamati imepitia na kujadili Mikataba hiyo minne, mmoja baada ya mwingine, Kamati inawasilisha maoni yanayohusu Mikataba yote minne kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake zilizoleta manufaa makubwa kwa Taifa letu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ifanye kila linalowezekana ili Mikataba kama hii iwe inaridhiwa na Bunge lako Tukufu mapema na kwa wakati unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa Miswada inayoletwa Bungeni ishabihiane na kukidhi mahitaji kulingana na Mikataba inayoiridhia. Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mikataba hii inatekelezeka Serikali inapaswa kufanyia marekebisho sheria zilizopo ambazo bado zina mapungufu au kutunga mpya kwa maeneo ambayo bado hayana sheria husika. *(Makofi)*

Kamati inaishauri Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa Mikataba inayoridhiwa ili kufungua wigo wa ushirikiano wa Kimataifa katika uchumi na uwekezaji. Serikali idumishe ushirikiano na nchi nyingine wanachama katika kutoa mafunzo ya kisayansi na kiteknolojia kwa wafanyakazi wake, kupata vifaa vya utafiti pamoja na kusimamia mikakati ya kuzuia uchafuzi wa mazingira baharini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Mikataba hii katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, kutunza mazingira, kulinda viumbe vya majini, kulinda vyombo vya majini na watumiaji wake, Kamati inashauri Serikali iweke mikakati ya kuwezesha kutekelezwa kwa maazimio hayo.

Kamati inaishauri Serikali kujiandaa katika kukabiliana na majanga kwa kuhakikisha kuwa kuna vitendea kazi na wataalam wa kutosha. Aidha elimu ya kutosha itolewe mara kwa mara kwa wenye vyombo vya angani na majini, ikiwa ni pamoja na watumiaji wake ili kulinda vyombo vya usafiri, watumiaji na viumbe vinavyoishi majini.

Mheshimiwa Spika, Ili kuwepo na utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi wa mazingira ya Baharini kutoka Melini wa mwaka 1973/78 *(International Convention for tha Prevention of Pollution from Ships, MARPOL 1973/78),* Kamati inashauri kuwa Wizara ya Miundombinu iweke utaratibu wa kufuatilia meli zinazopitia nchini ili kuhakikisha kuwa hazimwagi mafuta. Juhudi za makusudi zifanyike kununua rada na boti ziendazo kasi kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imechelewa kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1965 unaohusu taratibu za kuhudumia Meli za Kimataifa zinazobeba mizigo na abiria zikiwa Bandarini *(International Convention on Facilitation of International Maritime Traffic, 1965),* bado umuhimu wake ni mkubwa kwa ajili ya kuboresha huduma za bandarini na kuongeza tija. Kamati inashauri Serikali *(SUMATRA)*

pamoja na vyombo vingine kuweka utaratibu mahsusi wa kufuatilia vyombo vya majini hususan katika Maziwa yetu makuu ili kusiwe na ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wataalamu wake kuiangalia Mikataba yote ya Kimataifa, ambayo Tanzania bado haijaridhia, iwapo ina manufaa kwa maendeleo ya nchi na watu wake, Mikataba hiyo iwasilishwe Bungeni ili Bunge lako Tukufu liweze kuiridhia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Naibu Mawaziri wa Miundombinu, Ndugu John Kijazi, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kuwasilisha Maazimio hayo kwa ufasaha, jambo ambalo limerahisisha kazi kwa Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa kazi waliyoifanya ya kupitia na kujadili Maazimio haya na hatimaye kutoa maoni yatakayosaidia kuyatekeleza. Naomba niwatambue kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Joyce Masunga, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ambao ni Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka Abrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Godfrey Zambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake.

Aidha, napenda kumshukuru Ndugu Justina M. Shauri, Katibu wa Kamati hii pamoja na Makatibu Wasaidizi Ndugu Zainab Issa na Ndugu Patson Sobha, kwa kuweza kuihudumia vema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni na ushauri huo naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Miundombinu imejadili Maazimio yote na kwamba yamezingatia mahitaji ya nchi. Kwa hiyo basi, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kujadili na kuridhia Maazimio na Mikataba hiyo kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, ahsante sana, umewasilisha vizuri sana. *(Makofi)*

Sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala haya.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako wewe na uongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi kuhusu kuridhia maazimio ya mikataba tajwa hapo chini, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(c) na 70(2) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi chote wakati kamati ikipitia maazimio haya, aidha ninatoa shukrani kwa wote walionipa mashirikiano katika uchambuzi wa mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, Mikataba ifuatayo ndiyo iliyopitiwa, na kambi ya Upinzani inayo machache kuhusiana na mikataba hiyo.

(i) Mkataba wa mwaka 1972 unaohusu uzuiaji uchafuzi wa Bahari kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine *(The convention on prevention of marine pollution by dumping of wastes and other matters 1972);*

(ii) Mkataba wa mwaka 1973/1978 unaohusu kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari kutoka melini *(International convention for the prevention of pollution from ships, (MARPOL 1973/78);*

(iii) Mkataba wa mwaka 1965 unaohusu taratibu za kuhudumia meli za kimataifa zinazozeba mizigo na abiria zikiwa bandarini *(International convention of facilitation of international maritime traffic,1965)*; na

(iv) Mkataba wa mwaka 1944 unaohusu uhuru wa kuruhusu ndege za kimataifa zenye ratiba kupita kwenye anga la nchi nyingine bila ya kutua ama kutua kwa sababu zisizo za kibiashara *(International Air service transit agreement (IASTA) signed on 7 December,1944)*

Mheshimiwa Spika, maudhui ya mikataba hii yote isipokuwa mmoja karibu ni sawa kwani lengo lake ni kuweka na kutunza mazingira ya baharini na kuifanya bahari kuwa salama kwa viumbe waishio humo pamoja na mazingira ya kando kando ya bahari.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli uliowazi kuwa madhara ya taka kumwagwa baharini ni makubwa mno kwa viumbe waishio baharini na hata kwa wale wanaojipatia riziki zao za kila siku kwa kutegemea bahari. Mkataba wa uzuiaji wa uchafuzi wa baharini kwa njia ya utupaji taka na bidhaa nyingine wa mwaka 1972 uko chini ya *IMO*. Lakini kitu cha kushangaza ni kuwa kati ya wanachama 168 wa *IMO,* ni wanachama 78 tu ndio wameishauridhia mkataba huu. Kwa hili Kambi ya Upinzani inadhani hapa kuna mapungufu ambayo kwa njia moja au nyingine mkataba unaweza kuwa ni wa kinadharia

mno kwa nchi zinazoendelea kutokana na teknolojia inayohitajika kutumika katika udhibiti huo kutokuwa rahisi kwa mataifa hayo au mataifa yaliyoendelea *(Industrialized countries)* hayakuona umuhimu wa nchi zinazoendelea kuridhia mkataba huo ili yaendelee kupata sehemu ya kumwaga taka bila wahusika kugundua kutokana na kiwango cha teknolojia kilivyokuwa kidogo katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya (i) na (ii) ambapo mkataba unazitaka nchi mwanachama pekee au kwa pamoja kuweka mikakati mahsusi ya kuzuia utupaji taka baharini, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze kwa hili wadau wakuu ambao ni wananchi wote wanaojipatia riziki zao kwa kutumia bahari (wavuvi wadogo na wakubwa) wameshirikishwa vipi? Aidha, Ibara ya (ii) inazungumzia kuweka mikakati inayokwenda sambamba na sayansi na teknolojia na uwezo wa kiuchumi. Tunaweka hilo kama angalizo kwa ukweli kuwa mbali ya vifaa vinavyoendana na sayansi na teknolojia ni lazima kuwepo na vyombo vya doria na pia kwa wadau mbali mbali wawe na uwezo wa kutoa taarifa kwa haraka pindi wanapokuwa na wasiwasi hali isiyo ya kawaida inapojitokeza katika maeneo yao ya uvuvi.

Ibara ya (iv) inaelezea kuhusu taka zilizokubalika, kama ambavyo tumeelezea hapo mwanzo kuwa vifaa vya teknolojia ya kisasa hatuna. Hivyo ni vigumu kuelewa ni taka gani zimekubalika au zipi hazikubaliki kwa kuangalia nyaraka tu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa makini kwa hilo kwani hata madhara yaliyotokea katika nchi ya *Ivory Coast* inawezekana nyaraka zilionyesha kuwa taka hazikuwa na madhara na nchi haikuwa na teknolojia ya kuangalia ukweli kuhusu taka hizo mpaka madhara yalipojitokeza ya vifo vya watu kadhaa kutokea. Jambo lingine ni rushwa, kitu ambacho kimekithiri miongoni mwa wale waliopewa mamlaka kufanya kazi kwa niaba ya wananchi, mvunja nchi ni mwananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba wa pili kama mpangilio wa hotuba hii ulivyo, Kambi ya Upinzani ina maoni yafuatayo, pamoja na uzuri wa mkataba huu, lakini bado utekelezaji wake unaweza kuwa na matatizo kwani, katika faida ambazo nchi itakayoridhia itafaidika nazo, kipengele (f) katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuwa meli zitakuwa na vyombo vya kuhifadhia uchafu unaotoka kwenye meli *(reception facilities)* badala ya kuumwaga baharini. Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi zaidi ni nani hasa atahakikisha kuwa uchafu huo unamwagwa sehemu tofauti na baharini? Aidha, kwa kuwa lengo ni kutunza maeneo ya baharini, Serikali ina sema nini kuhusu mtandao wa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam kuelekezwa baharini? Kwa kuwa Tanzania ilichelewa kujiunga na mkataba huu kutokana na gharama kubwa katika utekelezaji wa mkataba huu, Kambi ya Upinzani ina mwomba Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania, gharama kubwa zilikuwa zinahusisha nini na nini, maana amesema hili limewezekana baada ya Serikali kubadilisha sera zake. Hii inatoa tafsiri kuwa baadhi ya sera za Serikali ni gharama kwa Watanzania? Ni ukweli uliowazi kuwa katika kujiunga na ushirika wowote kuna kupoteza na kupata, je, kama nchi tumepoteza nini?

Mkataba wa tatu kama mpangilio wa hotuba hii ulivyo unaohusu taratibu za kuhudumia meli za kimataifa zinazobeba mizigo na abiria zikiwa bandarini, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa angalizo kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa na bandari.

Kama inavyoeleweka kuwa uharaka wa kupakua na kupakia mizigo ndio ubora wenyewe, lakini hiyo yote inategemea uharaka wa kupatikana kwa nyaraka za mizigo zinazoshushwa na kupakiwa. Ukwamishwaji wa makusudi kwa nyaraka muhimu za mizigo toka katika mamlaka husika,ni jambo ambalo linaongeza gharama kwa wenye meli na wafanyabiashara. Hii husababisha wafanyabiashara kuamua kuhamishia shughuli zao katika bandari za nchi jirani.

Kuhusu mkataba wa mwaka 1944 unaoruhusu ndege za Kimataifa zenye ratiba kupita kwenye anga la nchi nyengine bila ya kutua au kutua kwa sababu zisizo za kibiashara *(International Air Service Transit Agreement (IASTA),* Kambi ya Upinzani inatoa angalizo juu ya usalama wa nchi, tusije tukaridhika tu na maelezo ya nyaraka na taarifa ya kwamba ndege fulani itapita kwenye anga la nchi yetu au kutua kwa sababu za kiufundi. Kwa hivyo tunaitahadharisha Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuwa macho zaidi na hilo kwani adui mara nyingi huwa anatumia mbinu tofauti katika kumshambulia mwenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani na ndiye Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa masuala hayo. Sasa kwa mchakato wa kufikia kuridhia, ninayo majina ya Waheshimiwa Wabunge watano kwa mpangilo ufuatao, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Nitaufuata mpangilio huo huo katika uchangiaji. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya awali ili nichangie machache kuhusu kuridhia kwa hii Mikataba minne mbayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha hivi punde. Napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa nafasi yake hii mpya kwa kutoa ufafanuzi mzuri juu ya Mikataba hii yote. Napenda kuipongeza Ofisi yake vilevile kwa kuandaa Mikataba hii kwa ufasaha. Kamati inayohusika vilevile imejitahidi kutoa ufafanuzi mzuri na kutoa ushauri mzuri kwa Serikali. *(Makofi)*

Nimesimama kuunga mkono Mikataba yote minne kama ilivyotolewa. Lakini kwa sababu ya muda mfupi, nitaomba nijielekeze kwenye Mikataba miwili tu ingawa yote kwa ujumla wake inafanana. Nitazungumzia kwa kifupi Mkataba wa Uzuiaji wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari kwa njia ya utupaji wa taka na bidhaa nyingine wa 1972 na ule Mkataba wa Kimataifa kuhusu kuzuia uchafuzi wa Mazingira ya Bahari kutoka melini wa 1973/1978.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Mikataba yote kwa ujumla wake kama nilivyosema kwa sababu nakubaliana na faida zilizotolewa kama zilivyoainishwa na Mheshimiwa Waziri. Napenda kusema Mikataba hii yote imeletwa kwa wakati muafaka kabisa na naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba na sisi ni wakati muafaka wa kuridhia Mikataba hiyo ingawa imekuja kwa kuchelewa kidogo. Lakini sababu zimetolewa na mimi napenda nikubaliane nazo.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania kukubali kuridhia Mikataba hii, maana yake ni kwamba na sisi wenyewe kama nchi tuko tayari kabisa kusimamia kwa makini na kuhakikisha kwamba tunakuwa mstari wa mbele katika kuona kwamba tunafuata Mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara ya kwanza nilikuwa nina wasiwasi, nilikuwa najiuliza maswali mengi hasa nilipokuwa nayaona maneno katika faida. Katika faida ni kamba tutakuwa na uwezo wa kisheria katika kuzuia masuala mbalimbali ya uchafuzi, lakini vilevile katika kudhibiti. Nikawa najiuliza ni nani atafanya kazi hiyo! Lakini kwa maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, nguvu hiyo kwa Mikataba mingi inapewa *SUMATRA*. Kwa hiyo, napenda kuipongeza Serikali kwa kujiandaa vilivyo, kuhakikisha kwamba kutakuwa na chombo maalum ambacho kitafanya kazi ya ufuatiliaji.

Kwa hiyo, rai yangu ni kuhakikisha kama Serikali kama ilivyoonyesha dhamira, ni kuhakikisha kwamba *SUMATRA* inakuwa na uwezo mkubwa na hasa kwa masuala ya kiutalaam, lakini vile vile kwa masuala ya nyenzo na vifaa. Sina wasi wasi sana kuhusu watalaam, kwasababu nina hakika nchi yetu ina wataalam wengi sana na wasomi wazuri sana ambao wamesomea Sayansi na Teknolojia.

Lakini vilevile tunao watalaam wengi wazuri ambao walibobea katika masuala ya mazingira. Kwa hiyo, katika eneo hili sina wasi wasi, isipokuwa basi tujikite katika kutafuta misaada ya kupata vifaa ambavyo wenzetu watavitumia, *SUMATRA* wasaidiwe hasa katika suala zima la doria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanaotoka katika nchi zilizoendelea wanaokuja katika nchi zetu, tukubali kwamba ni wajanja. Wenzetu wameendelea sana katika mambo ya taaluma na kadhalika. Kwa hiyo, tutahitaji sana udhibiti wa karibu.

Kwa hiyo, kuwa na vyombo vya doria itatusaidia sana na doria hiyo iwe inafanyika mara kwa mara siyo kwa nyakati fulani tu, zifanyike mara kwa mara. Kwa namna hiyo, basi tutahakikisha tumedhibiti vizuri na tumetumia uwezo wetu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naunga mkono kuwa tunahitaji kuwa na vifaa vya utafiti. Nchi yetu katika maeneo mbali mbali suala la utafiti tuko nyuma. Lakini si kwa sababu hatuna watalaam, ni kwa sababu hatuna vifaa au nyenzo ambazo zinatusaidia kufikia maamuzi mazuri kutokana na tafiti tunazozifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyosema Tanzania itakuwa mmoja wa watekelezaji kwa sababu tumeridhia au tutaridhia kwa siku ya leo. Tunazo na sisi *challenges* zetu ambazo lazima tuzisimamie kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue mfano mdogo tu wa namna ya ku-*dispose* takataka zinazoingia baharini. Mimi sioni tatizo la kutupa takataka zinazotokana kinyesi ndani ya bahari. Huwezi ukalaumu ukaishia hapo tu ukasema kwamba kuna tatizo la kutupa

kinyesi ndani ya bahari. Tatizo ni kwamba kinyesi hicho kinatupwa kabla hakijawa *processed*. Kwenye nchi za wenzetu ambao wameendelea hili ni jambo la kawaida tu, utatupa wapi takataka kama hiyo? Kwa wale ambao wako karibu na maji wanatupa huko.

Lakini kwa nchi zilizoendelea wanatumia teknolojia sahihi ya ku-*process* kinyesi hicho na kwa maana hiyo, tungeweza kuona kinachoingia ndani ya maji ni maji safi ambayo unaweza ukanywa yamekuwa *processed*. Kwa hiyo, hamna tatizo hapo na uki-*process* unaongeza hata maji mengine ndani ya bahari. Lakini unakuwa na mabaki ambayo yamesalia kutokana na *procedure* ya ku-*process,* sasa yale mabaki, wenzetu wanayatumia kwa ajili ya samadi. Sasa siyo lazima tutumie mbolea za viwandani. Samadi nyingine ni kama hizi ambazo zinakuwa *processed* kutokana na vinyesi vya binadamu. Kwa hiyo, tatizo hapa mimi silioni, lakini ningeomba, kwa kuwa tunazungumzia suala la kupata misaada ya teknolojia, misaada ya vifaa, basi tuombe misaada kama hii ili tusiwe na tatizo la kutupa taka iliyo mbichi kabla haijawa *processed*.

Nichukue mfano mwingine kwa upande wa Dar es Salaam huko huko. Kule Dar es Salaam au maeneo ya Pwani mengi ambayo watu wanapenda kwenda baharini na kutumia fukwe kwa maana ya kwenda kutembea na kufurahia ufukwe, tumejionea wananchi wa Tanzania hasa wakazi wa Dar es Salaam, wakienda na vifaa ambavyo vinaathiri mazingira. Mfano umetolewa hapa, baadhi ya takataka hizo ni pamoja na mifuko ya *plastic*. Sasa utaona mara nyingi mifuko hiyo inatupwa baharini.

Mheshimiwa Spika, unapotupa takataka kama hizi baharini, kwa vyovyote tukubali kwamba tutaathiri maliasili au viumbe vilivyomo ndani ya bahari. Kwa hiyo, hapo mimi ninachotaka kusisitiza kwamba, yeyote atakayepewa madaraka hayo, basi asimamie suala hili kikamilifu. Kama ni *SUMATRA* yenyewe au Halmashauri za Manispaa lazima waazimie hili na kuhakikisha kwamba taka hazitupwi ovyo katika maeneo ya ufukwe. Ni hatari!

Mimi nimewahi kupita katika maeneo ya ufukwe siku za Jumatatu, utaona kwamba kuna kichefuchefu mtu unakipata. Takataka zimetupwa ovyo ovyo, nyingine baharini, nyingine kando kando ya fukwe ambazo hazina mwenyewe. Wanakuja wanazoa lakini nyingine zinaingia baharini. Kwa nini kusiwepo na utaratibu wa kuweka *dustbins* ambazo zitawekwa katika maeneo hayo ambayo wananchi wanakwenda, basi takataka hizo ziwekwe humo *and then* wanaohusika waende wakazitupe? Kwa nini ziachwe zikizagaa na nyingine zinakwenda baharini na kuharibu viumbe na kuchafua mazingira na kuleta athari kwa binadamu na viumbe ambavyo sisi tunatazamia kwamba ni viumbe vitakavyotuletea uhai katika maisha yetu?

Mheshimiwa Spika, nilifikiri nichangie kwa hayo machache ili kuboresha na kutoa ushauri kwa Wizara na kwa maana hiyo, utekezaji wa Mikataba hii na wenzetu watakapotutembelea waone na sisi tuko mstari wa mbele kwenye utekelezaji. Kwa hiyo, kwa wale ambao hawajaridhia Mkataba na wenyewe basi watakubali kuridhia kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, ninaomba kuunga mkono kuridhia kwa Mikataba hii yote kwa pamoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie angalau kwa machache ambayo ninayo.

Kwanza, nianze kwa kusema kwamba leo nina furaha kubwa kuleta Mikataba hii ya kuridhia hasa ule wa Uchafuzi wa Mazingira Baharini. Jana tulipitisha Azimio la Kuondoa *Visa* baina ya Msumbiji na Tanzania. Waheshimiwa wa Kusini, walifurahi sana kupitishwa kwa Azimio lile na ni kitu ambacho walikifurahia zaidi kuliko sisi wengine tukitazama ule mpangilio.

Sasa na mimi leo niseme kwamba nafurahia sana kuleta maazimio haya kwa sababu ninatoka Visiwani, mazingira niliyokulia ni baharini na mimi uchafuzi wa mazingira baharini unakera mno kwa sababu hizo na mimi leo nina furahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, hii Mikataba Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Msemaji wa Upinzani na mwenzangu aliyetangulia wote wanakubali kwamba imechelewa mno na mimi naungana nao. Mikataba yote minne tukitazama huu wa mwisho una miaka 33 na ukafanyiwa marekebisho ni miaka 28 iliyopita ndiyo tunakubali Tanzania kuridhia leo baada ya miaka 28. Mwingine una miaka 34 ndiyo leo Tanzania tunakubali kuridhia Mkataba huu. Mwingine wa ajabu kabisa huu una miaka 62 wa tangu mwaka 1944 Tanzania ndiyo leo tunaona umuhimu wa kuridhia Mkataba huu. Mwingine una miaka 41, hapa tunapata funzo. Hivi kwa nini miaka yote hii ,ndio leo tunaona umuhimu wa kuridhia Mikataba hii? Hii dosari ni dhahiri kwamba tuione. Sasa hivi Tanzania tujiulize na tuone dosari yetu, kwa nini wenzetu waliona umuhimu wa mambo haya miaka hiyo, lakini Tanzania tunaona leo umuhimu wa masuala haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mikataba hii, naendelea kuongezea kwamba, bado ipo Mikataba mingine ambayo tayari wenzetu wameshairidhia na leo Tanzania bado hatujairidhia. Kwa msemo huu ambapo pengine tuna sababu zetu za msingi, lakini pamoja na sababu hizo baada ya miaka fulani tutakuja kujikuta kwamba kumbe pia ilikuwa na umuhimu wa kuiridhia.

Wito wangu kwa Serikali, Mikataba yote ambayo haijaridhiwa na Tanzania ni vyema kwanza tujulishwe Wabunge, iletwe hapa Bungeni, tuambiwe ni Mikataba gani yote kwa ujumla ambayo Serikali haijaridhia, halafu watueleze kwa muda huu sababu gani zilizopo ambazo Serikali haijaridhia Mikataba hiyo. Kwa hiyo, hilo lilikuwa la kwanza kuhusu mchango huo.

Nakuja sasa kuchangia katika Mikataba mitatu katika hii minne hasa nakijita kwa ile ambayo inahusiana na uchafuzi wa mazingira baharini. Suala la bahari na suala la mazingira ni masuala ambayo yana mifumo miwili. Suala la mazingira lina Waziri wake Tanzania Bara, tuna suala la mazingira lina Waziri wake Tanzania Visiwani. Lakini Ofisi Kuu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye Makamu wa Rais mara nyingi sana

anashughulikia suala la Muungano lakini huku kuna Waziri anayeshughulikia Mazingira Tanzania Bara na Zanzibar.

Lakini suala la bahari, kinakuja kitu hapa cha *(cross cutting)* suala la mtambuka, hasa kwa sababu kuna Sheria ya Bahari Zanzibar mbali na kuna sheria inayohusiana na mambo ya bahari Tanzania mbali. Bahati nzuri Tanzania imejiunga na *IMO* tayari wakati bado Tanzania Visiwani hawajajiunga na *IMO*. Hapa niliuliza swali nikamwomba Waziri wa Miundombinu aisaidie Tanzania Visiwani sasa hivi kujiunga na *IMO* zile *conditions* zote zinazohitajika.

Sasa kwa vile Tanzania imeshajiunga na *IMO* na inakabiliwa na sheria tofauti, lakini suala la uchafuzi wa bahari ni suala mtambuka. Kwa maana hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo inashughulikia masuala pia ya Muungano ilione suala hili la uchafuzi wa bahari, sio suala linalohusu Tanzania Bara tu, bali suala pia linahusu na Tanzania Visiwani. Juhudi zifanywe kwa pamoja kwa sababu bahari ikichafuka aidha ni Tanzania Bara au ni Tanzania Visiwani *effect* itatupata sote.

Kwa maana hiyo, mimi nakiri kwamba mazingira ya bahari yamechafuka tena bahari imechafuliwa sana. Sababu zinawezekana zikawa nyingi mno. Aidha, ni meli hizo za mataifa zinazopita zikachafua mazingira au meli zetu za ndani, ubovu wa meli na moshi unaotoka baharini au sababu nyinginezo lakini uchafuzi umefanyika. Kipimo kikubwa tunachokiona ni upungufu wa samaki, hicho ndiyo kipimo rahisi tunachokiona. Sisi watu wa Pwani tunashuhudia suala hilo kwamba upungufu wa samaki baharini ni mkubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano miaka ya 1960 na 1970 wakati mimi mdogo, ikitoka meli Pemba au Unguja ikipita pale katika *Pemba Channel* utakuta nyuma ya meli wanafuata hawa *dolphins* kwa wingi wanacheza wanafuatana na ile meli. Leo utasafiri Unguja na Pemba, Unguja na Tanzania Bara hukuti *dolphin* yoyote akifuata meli na ni viumbe wa baharini wanaopenda kucheza na vyombo au binadamu. Leo hamna! Wako wapi? *(Makofi)*

Ni sehemu moja tu Zanzibar iko Kizimkazi ndiyo angalau uwafuatilie huko ndiyo utawaona. Hiyo ni sababu moja ya uchafuzi wa mazingira, ndiyo maana viumbe hawa wametoweka kwa wingi. Samaki wametoweka, ndugu zetu wavuvi sasa hivi wanapata taabu, tena wanapata taabu sana. Mtu anakwenda baharini siku tatu/nne pengine hajaambulia chochote, anashindwa na chai yake ya asubuhi kwa sababu samaki hawaonekani. Moja ya sababu ni uchafuzi wa mazingira ya baharini. Kwa maana hiyo, Azimio hili pamoja na kwamba limechelewa, lakini limekuja *time* sasa hivi ambayo nashauri tuliridhie sote kwa ujumla ili mambo haya yaweze kupatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhia Maazimio haya, tunapaswa tujiulize: Je, tumejiandaa kweli? Kwa sababu huu uchafuzi ikiwa hatujajiandaa tutakuwa tunapitisha Azimio hapa Bungeni, lakini utekelezaji wa ufuatiliaji haupo kwa sababu unahitaji nyenzo na vifaa muhimu. Mfano, mwezi wa Julai, niliondoka hapa kwa dharura nikaenda Pemba, tulipita angani tukaikuta Meli ya Mafuta ambayo imeshashusha mafuta sijui wapi inapita katika *Pemba Channel* inapita upande wa bahari kuu ambao anaingia

mpaka *Durban* kupitia upande huu wanasafisha matanki yao na *pilot* wa ile ndege ndogo alibidi azungushe kwanza tuwafuate tuwaangalie, wanasafisha matanki na unaona ile *layer* ya mafuta kwa wingi inamwagika baharini yanakuja huku.

Sasa inategemea *time* aidha maji kuja au maji kutoka. Wakati wanafanya kitendo kile ikiwa ni *high tied,* yaani maji yanajaa utakuwa uchafu wote ule unakuja huku karibu na Wapwa au Pwani ndogo ambapo huku ndiko kwenye miamba ambayo mna vizalia vya samaki na matokeo yake ni kufa kwa viumbe hivi. Je, tumejiandaa vipi kufuatilia meli kama hizo? *(Makofi)*

Ziko meli ambazo hazihusiani na mazingira, lakini zinahusiana na uvuvi ambazo zinakuja vile vile ambazo tunahitaji kuzi- *chase* lakini leo ikiwa Tanzania hatuna chombo au hatuna boti za ufuatiliaji angalau zinazokwenda *speed* za 65 *nods* tutawezaje kufuatilia mambo haya? Kwa maana hiyo, tunahitaji kujiandaa, siyo kupitisha Maazimio haya tu lakini tunahitaji tujiandae.

Tunazo meli zetu hapa hapa nchini. Ukienda Bandari ya Dar es Salaam utaona *wreckage* tele za meli, katika hivyo vyuma chakavu, vyuma vizito meli zimekuwa *dump* zimekaa hapo miaka mingi hakuna mpango wowote. Huo ni uchafuzi mwingine wa mazingira. Ni vitu vilivyopo hapa hapa nchini. Meli nyingine mbovu ambazo zinakuja hapa zipo zinakwenda zinamwaga *oil* baharini, yaani ni vyombo vingine siyo vya nje tu vya hapa hapa nchini. Je, tumejiandaa vipi? Wakati mwingine meli hizo zinatusaidia sisi kwa usafiri na Serikali haina uwezo wa kuleta meli ambazo za uhakika na mwananchi wa kawaida. Ukweli wa mambo, hana uwezo wa kununua meli mpya zilete huduma hapa atakwenda, atapewa hayo hayo mabovu, matokeo yake tunaharibikiwa sisi. Kwa maana hiyo, wakati tunapitisha azimio hili ni vyema Serikali ijiandae vizuri na vyombo vyote vitakavyotusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengine yanachafua mazingira ya bahari na hayatokani kabisa na vyombo vya baharini. Mimi nina mfano mengine yanatokana na mambo ambayo yanatendeka nchi kavu. Mfano halisi unaweza ukapatikana maeneo ya Visiwa vya Zanzibar hasa Ukanda wa Bwejuu mpaka Michamvi ambako kuna wawekezaji katika mahoteli makubwa makubwa wanachukua takataka za hoteli wana-*dump somewhere* juu lakini mvua zikinyesha uchafu ule ule ndiyo unaoingia tena baharini. Ukanda huo mpaka ng'ombe wameshafariki kwenda kuzoga kwenye uchafu ule. Ng'ombe wakafariki maeneo ya Bwejuu. Je, tumejiandaaje? Suala hili la uchafuzi wa mazingira naomba sana Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wizara ya Miundombinu ilichukulie *serious* sana na siyo lifanyike upande mmoja tu wa Jamhuri, linafanyike pande zote kwa sababu ni suala la mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa machache hayo, naomba niunge mkono Azimio hili kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja hizi zilizotolewa na ndugu yetu Waziri wa Miundombinu kwa niaba ya kutaka Bunge lako Tukufu liridhie Mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, nami nirudie kuisifu Wizara hususan Waziri na Naibu kwa kufafanua vizuri tu Mikataba hii ili sote tuweze kuelewa tunachoridhia ni kitu gani. Niwapongeze vile vile hasa Mheshimiwa Andrew Chenge kwa kupewa nafasi hii mpya na tuna mategemeo kabisa kwamba ana uwezo nayo na ataweza kutufanyia kazi yetu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba niseme tangu mapema kabisa kwamba na mimi naunga mkono hoja zote nne kwa sababu naona umuhimu wake ingawaje nyingine zimekuja kwa kuchelewa, lakini bado watalaam wanasema ni vizuri kutekeleza hata kwa kuchelewa kuliko kutotekeleza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamechangia sana na kwa ufasaha mzuri kwenye hoja nyingi zilizoletwa. Lakini mimi kuna sehemu ambazo sina utalaam sana hasa mambo ya anga kwa mfano. Ningependa kuzungumzia zaidi lile Azimio la mwisho ambalo linahusiana na kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu kuzuia uchafuzi wa mazingira kutokana na meli. Ingawaje kidogo nitazungumzia hata kwa kupitia ule Mkataba unaohusu *dumping*. Nitazungumzia katika vipengele vitatu.

Kipengele cha kwanza nitakachopenda kuzungumzia kinahusiana na athari zinazoweza kutokana na uchafu ambao ni kwa bahati mbaya tunaita *accidental spills* kwa Kiingereza. Ya pili, nitapenda kuzungumzia athari zinazoweza kutokana na uchafuzi wa makusudi na tatu, nitapenda kuzungumzia, kuhusiana na kipengele kwamba tunazungumzia hasa suala la bahari. Lakini kwa kweli kwa vile tumezungukwa na maziwa makubwa sana ambayo ni makubwa hapa duniani, ni vyema hata haya tukayaangalia na kuona ni vipi tunaweza tukawa na Mikataba inayoweza kusaidia kuzuia uharibifu wa mazingira kwenye haya maziwa makubwa.

Nianze na ile ya kwanza ambayo inatokana na bahati mbaya *(accidental spills). Accidental Spills* zinaweza kutokana na meli zinazopita katika mwambao au katika bahari yetu na meli ile ikagonga mwamba kwa mfano na ikamwaga Kemikali au mafuta au takataka au Kemikali yoyote ambayo inaweza ikawa imebeba. Lakini *Accidental Spills* nyingine zinaweza kutokana na *leakages* ambazo meli inaweza kuwa inakwenda lakini hawana taarifa kwamba kwa bahati kwamba labda meli imetoboka kwa hiyo, mafuta au Kemikali inamwagika kwa bahati mbaya bila kujua au bila kutarajia.

Mheshimiwa Spika, ni hatari sana vitendo vya namna hiyo ambavyo havitegemewi na siyo vya makusudi, ni hatari sana kwa sababu madhara yake mara nyingi huwa ni makubwa kwa sababu yanaathiri eneo kubwa la bahari na huweza kuathiri viumbe wengi wa majini ikiwa ni pamoja na mimea, wanyama na samaki, lakini baadaye hutuathiri sisi tutakaotumia viumbe hao kama samaki au mimea hiyo. Tatizo langu ni kwamba, licha ya kuridhia Mikataba hii, ni ile tunayoita *preparedness* na wenzangu wengi wamezungumzia hili kujiweka tayari iwapo kwa bahati mbaya mafuta yanamwagika kwa uwingi kutoka kwenye meli au kemikali yoyote inayomwagika kwa wingi kutokana na meli inayopita kwenye mwambao wa bahari yetu tutafanya nini?

Hii *preparedness* inayozungumzwa hapa ni ile *rapid deployment* au mikakati ya kuichukua kwenda kupambana na mafuta au *chemically* ile itakayokuwa imemwagika ili isiathiri eneo kubwa la bahari au isiathiri viumbe wengi wa bahari. Ni kweli inahitaji vifaa/vyombo vya kuweza kwenda haraka. Lakini kikubwa itakuwa ni namna ya kuondoa mafuta yale au kemikali zile angalau kuzipunguza zisiwe nyingi zikaathiri viumbe wa majini. Ile ni kazi ngumu, ni gharama na hata huo uwezo wa kwenda kufanya hivyo unaweza ukawa ni mdogo au hatuna kabisa. Kwa hiyo, nilidhani tunapozungumzia kuridhia Mkataba huu, vyombo vyetu hivi *SUMATRA* Idara ya Mazingira, *NEMC* au Wizara yoyote inayoshughulika na mazingira wakawa na vyombo hata vichache badala ya kungojea kwamba tutaomba msaada kwa nchi zilizoendelea au kwa wenzetu wenye vyombo lakini lazima na sisi tuwe na vitu vichache ambavyo vinaweza kuanza kutumika katika kupooza/kupunguza hali mbaya ambayo inaweza kujitokeza. Hilo ni muhimu kuliko kuridhia mkataba lakini hakuna chochote kinachofanyika. Mimi sijui kama *SUMATRA, NEMC* au Wizara inayohusika na mazingira kweli ina vifaa, imejiandaa kweli na kuweza hata kufanya kile kidogo cha kuanzia wakati tunasubiri msaada kutoka kwenye nchi ambazo wana vifaa vya kuweza kutusaidia. Nilidhania hii ni muhimu sana. *(Makofi)*

Lakini linaloendana na hapo kwa kawaida tunazungumzia juu ya *risk assessment* kwa sababu ni madhara yanayotokea bila kutegemea ni lazima tufanye *assessment* tuainishe uharibifu utakaokuwa umetokea ili hatua zichukuliwe. Vyombo na utaalam unaotakiwa ni wa gharama sana na hapa kwetu tunaweza tukawa na watalaam, lakini vyombo hatuna. Lakini hata utalaam wa kufanya *risk assessment,* tuseme ukweli mimi najua maeneo hayo na namna ya kuweza kufanya kazi hizo *risk assessment.* Lakini watalaam hapa nchini wenye uwezo wa kufanya hizo kazi ni wachache sana.

Kwa hiyo, kuna haja wakati tunaporidhia Mikataba kama hii kuweka msisitizo katika *(ku-train)* kupeleka kwenye mafunzo watalaam wengi zaidi Vyuo Vikuu wanaoweza kutusaidia kuainisha au kufanya *risk assessment* kwa sababu ni masuala ya kitalaam yanahitaji teknolojia ya hali ya juu na vyombo na vifaa vya gharama sana kuweza kufanya *assessment* hizo ili kuweza kujua madhara yaliyotokea baharini yametokea kiasi gani na ni kitu gani kimeathirika.

Lakini haiishii hapo, mara nyingi kuna ufuatiliaji *(monitory)* ili kuweza kuona ni vipi athari ile inaanza kupungua na itachukua muda gani kupungua kufuatilia viumbe vilivyoathirika kama vimeanza kurudia hali yake *recovering* hiyo yote inahitaji fedha ya kuwa na vifaa hivyo kwenda kupima, kwenda kufuatilia na kadhalika. Kwa hiyo, tunaporidhia Mikataba hii tunajiingiza katika suala ambalo ni gumu, sisi hatuna uwezo nalo. Kwa hiyo, nilikuwa nasema, lazima tujiweka tayari hasa katika vyombo vyetu tulivyonavyo *NEMC*, Idara ya Mazingira, Vyuo vyetu vikuu, *SUMATRA* wenyewe kuhakikisha kwamba tunakuwa na watalaam wachache au vyombo vichache vya kutuwezesha haya yanapotokea tukaenda haraka sana kuanza angalau kushughulikia masuala hayo badala ya kungojea mpaka watalaam au vyombe vije kutoka nchi za nje au kwa wenzetu walioendelea. Hilo la kwanza.

La pili, nililotaka kuzungumzia ni uchafuzi huo wa makusudi. Nikisema makusudi ni pamoja na wenzangu wameelezea kutupa takataka *plastics,* makopo baharini tunapovuka kwenda labda Zanzibar au kuja *Main land* kutoka Zanzibar na wanaopita kando kando ya bahari kutupa hizi takataka pamoja na kinyesi tumeambiwa hapa. Hivi ni vitu ambavyo huwa vinafanywa kwa makusudi tu. Suala hapa ni kuwa na tabia ya kupitia, kufanya usafi angalau mara moja kwa mwaka. Kupitia maeneo haya kuona kuna uchafuzi kiasi gani. Inaudhi sana unaposafiri kwa vyombo vya maji unaona makopo yanaelea kwenye maji, hata kandokando wanaokwenda *beach* unaona makopo, *plastics* kandokando ya bahari hasa maeneo ya utalii.

Kwa hiyo, ni vyema kufanya *regular cleaning* kwenye maeneo haya ili kuweka maeneo yetu ya maji ya bahari yakae katika hali ya usafi. Hii tabia Waswahili hatunayo, tunaambiwa kwamba Waswahili tumezaliwa siyo watu tunaopenda sana usafi. Ile *culture* ya usafi hatunayo. Kwa hiyo, hata ukiona kopo unaliacha hivyo hivyo. Lakini ikiwa kwenye nchi za wenzetu ukimwona mtu anatupa kopo unaokota kopo unakwenda kumbwagia kwenye gari lake. *Plastic* mtu anadondosha nje unaliokota unamtupia yeye kwamba bwana hilo usitupe. Lakini sisi tuna kawaida ya kuacha tu, uchafu ule haukuhusu. Lakini kwa kweli tunachafua mazingira yetu.

Kwa hiyo, nilitaka kuainisha hilo tu kwamba *SUMATRA* na vyombo vyetu vingine, Idara nyingine zitakazohusika kuwa na tabia ya kufanya *regular cleaning up* ya maeneo yetu ili kuyaweka katika hali ya usafi. Suala la utupaji wa vinyesi na kadhalika, Mama Ngoye amelizungumza vizuri tu. Nataka kumtambua yeye kama Mwenyekiti wa *NEMC.* Kwa hiyo, anajua kazi ya *NEMC* mojawapo ni kuhakikisha kwamba mazingira ya majini na ardhi kwa kweli yanakaa katika hali ya usafi.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni hili la maziwa makuu. Ingawaje Mikataba hii haihusiani na maziwa makuu, lakini pengine ni wakati muafaka kuanza kufikiria ni nini tunaweza tukafanya au tukawa na Mikataba gani kati ya nchi zinazotumia maziwa haya. Katika vikao vilivyopita tuliambiwa katika Ziwa Nyasa wenzetu wanalisha samaki, humwaga vyakula wakiwa na meli au boti kusudi kuwanenepesha samaki wale.

Lakini kinachotokea pale ni kwamba, unabadilisha biolojia, unabadilisha *chemistry,* kemia ya maji, unaweza ukaongeza bionuwai, ukabadilisha bionuwai ya maji, lakini hata *chemistry* ya maji ikabadilika na ukaharibu mazingira ya majini. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na mikataba katika nchi zinazozunguka maziwa haya, hasa Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, kwa sababu nataka kuamini kwamba Ziwa Victoria angalau kuna *East African Community* na taratibu zinaweza kuwa zimewekwa katika kuainisha masuala ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Lakini katika maziwa haya mawili yaliyobaki, pengine kuna haja ya kuhakikisha kwamba nako tunakuwa na mikataba ya kuweza kuzuia na kuhakikisha kwamba taka, kemikali, sumu hazimwagwi, aidha kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Lakini vile vile kuhakikisha kwamba inapotokea hivyo tunakuwa na utaratibu wa kwenda mara moja haraka kufanya angalau juhudi za awali za kurekebisha mazingira yasiharibike zaidi wakati tunasubiri sheria zichukue mkondo wake wa kuhakikisha kwamba tunapata aidha

fidia au wataalam au vifaa kutoka nje vya kutuwezesha kumudu mazingira yaliyoharibika.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuchangia kwenye maeneo hayo matatu. Naomba kurudia kwamba na mimi naunga hoja hizi nne mkono na kwamba Bunge lako Tukufu liridhie. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nami sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia machache katika Mkutano huu wa Tano. Kwa kuwa ni mara yangu ya mwanzo katika Mkutano huu wa Tano, sina budi kwanza nitoe shukrani na kuwapongeza wale wote waliobadilishwa *positions* na kuwekwa *positions* nyingine ili tuweze kufunga magoli vizuri. *(Makofi)*

Nawapongeza wote wale Mawaziri na Manaibu Waziri. Nampongeza zaidi rafiki yangu Chenge kwa sababu yeye amekuwa sasa anataka kumpa cheo awe yeye ndiyo *Field Marshal* na awe yeye ndiyo *Air Marshal* na awe yeye ndiyo *Admiral of the fleet.* Maana yeye amechukua nafasi zote hizo za anga za bahari na za nchi kavu. Nakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naanza kuchangia, lakini kabla ya kuchangia, nataka kuunga mkono hoja hizi kwa yote haya ambayo yamejumuisha vifungu vinne vyote hivi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaunga mkono na tunaomba hoja hii iridhiwe.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanzia kwenye kifungu cha nne ambacho wenzangu wengi wamechangia. Naachia hicho kwa sababu hiki ndicho kinachotupa mashaka zaidi katika maeneo yetu ya mwambao na bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna bahati, tuna bahati kwa sababu tuna mwambao mrefu sana wa bahari. Kuanzia mipakani Cabodelgado Msumbiji mpaka Moa Kenya, ni maeneo marefu sana. Ukija kwa upande wa Mashariki ya Tanzania, tuna maeneo marefu hata *sea notice* za bahari 200 tunaweza tukacheza huko ni maeneo yetu bado.

Mheshimiwa Spika, tunataka kuridhia hili suala la mazingira ya bahari, lakini naomba sana kumshauri Waziri na kuishauri Serikali tuangalie sana kwa sababu tunaridhia. Lakini tumejipanga vipi katika kuridhia huku? *(Makofi)*

Tunaweza tukaridhia lakini yanayotendeka huko hatuyajui. Wenzangu wengi wameanza kuchangia hapa, wametoa hofu zao kwamba tunakubali kwa sababu ndiyo mambo ya kimataifa na tunakubali kwa sababu Waziri amechambua kwa kirefu hapa faida ambazo zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, meli nyingi sana ni kongwe na nyingi sana zina kawaida hiyo. Nasema hayo kwa sababu mimi mwenyewe ni Kepteni katika *Coastal Lines,* nimekuwa baharini miaka mingi sana na nimefanya kazi ambayo naelewa vizuri na nimetoka na meli mbali kutoka nchi za Ulaya mpaka Afrika, nayaona huko baharini mazongo yaliyoko.

Naeleza haya kwa sababu tumeshayakuta matatizo ambayo wenzetu bado hawana njia ya kuyafuatilia na kuyaona. Kuna hizi *tanker* ndiyo zenye matatizo makubwa zaidi, maana ndiyo zinazokuwa na ma-*chemical* mengi na mafuta ambayo wanachanganya katika zile meli. Mengi yanakuwa mabovu na yana *leakage*. Tukijipanga vizuri na faida zake tunaweza kuzipata vizuri. Tukiwa hatukujipanga vizuri bado tutakuwa ni eneo tulilokubali hoja, tulizoziunga mkono hoja, tulizoziridhia lakini maridhio haya yatakuwa hayana ufuatiliaji wa kweli na sisi tunafaidika katika haya?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa kama *SMATRA* au chombo kingine chochote hasa vyombo vya ulinzi kuwa na vyombo vinavyoweza kufuatilia, basi angalau tungepata helikopta moja au mbili tukawa kweli tunafanya ule ulinzi mle kuona au tukapata *speed boats* na tupate pia *research boat* ambayo pia nayo inaweza ikawa inafanya uchunguzi wa kuona kweli hapajamwagwa vitu vya aina hii. Kuna kule kuona kwa kawaida, lakini kuna kitu cha kuona katika vyombo vya kitaalam.

Mheshimiwa Spika, tunaiunga mkono hoja hii na tunaikubali. Lakini bado tunaomba tujipange katika kutafuta vyombo vya kisasa vitakavyoweza kusaidia kuhakikisha kwamba tuko katika hali nzuri Tanzania.

Mheheshimiwa Spika, baada ya hayo mimi niseme tu kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaunga mkono hoja zote nne zilizojipanga hapa na tunasema tunautakia kila la kheri na mafanikio mema Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni na hasa kutanabahisha kwamba wewe ni baharia.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika mjadala huu wa kupitisha Maazimio haya. Awali ya yote nimpongeze na mimi Mheshimiwa Chenge kwa kuwa Waziri wa Wizara ya Miundombinu. Mimi binafsi nilifarijika sana kwa sababu awali alikokuwa kwa kweli nilikuwa naona kwa uwezo wake mkubwa alikuwa hatumiki ipasavyo. Ila hapa naamini kwamba atatumika ipasavyo. Nataka nimhakikishie kwamba Kilindi tunamhitaji kuliko sehemu nyingine nyingi. Kwa hiyo, ninashukuru. *(Makofi)*

Lakini pili, nashukuru kwamba kwa kweli ameibua maazimio kama haya ambayo ni ya muda mrefu sana. Lakini naomba nimweleze tu kwamba najua yapo mengi ambayo utayaibua tena kwa muda mfupi tu ujao kutokana na uwezo wako.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi nataka kujikita zaidi kwenye kuridhia mkataba wa kubadilishana uhuru kuruhusu ndege za kimataifa zenye ratiba kupita kwenye anga za nchi nyingine bila kutua ama kutua kwa sababu sio za kibiashara, *Internatinal Air Services Transit Agreement.* Mimi zaidi nitajikita kwenye eneo hilo kwa sababu naona kwenye upande wa bahari yameshasemwa mengi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme tu, inasikitisha sana mimi kama Mjumbe wa Kamati wa Mambo ya Nchi za Nje na Wajumbe wenzangu mambo kama haya ambayo yanahusu masuala ya kimataifa, tulidhani kabisa kwamba pamoja na kwamba Kamati ya Miundombinu watahusishwa, lakini na sisi nadhani tulikuwa na kila sababu ya kuhusishwa kwenye kuangalia Mikataba hii. Tayari Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wetu Mama Anna Abdallah, tumeomba Wizara itupatie orodha ya Mikataba yote ambayo ipo ambayo tuliridhia, ambayo haijaridhiwa na sababu na kadhalika na kadhalika na kadhalika, lakini hatujapewa bado.

Lakini kwa kweli inasikitisha unapoiona inaletwa Bungeni na Kamati yetu haijaweza kuipitia ili na sisi tuione, lakini tuweze kutoa maoni yetu kama Kamati. Kamati ya Mambo ya Nje inaonekana kutokuwa na kazi. Ni kwa sababu mambo mengi yanakwenda kwingine ikisahaulika kwamba kuna Kamati kama hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa natoa wito kwa Mawaziri husika kwamba wakumbuke kuna Kamati kama hii ambayo pia ina majukumu katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini namba mbili, Tanzania tunakubali Mikataba mingi sana. Mimi najiuliza, huko nyuma nikisoma nikiwa Mbunge wa Afrika Mashariki nilikuwa nikipenda sana kusoma *Hansard* za Bunge hili masuala ya mikataba, mingapi. Ilikuwa inaulizwa mara kwa mara, utakuta tuko kwenye Mikataba mingi, tunaridhia na nini lakini ukiangalia tunanufaika nini, hakuna. Tunakwenda kama *fashion* wakati mwingine.

Sasa mimi nadhani katika Bunge hili la Awamu ya Nne la ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, ni vyema sasa tukaenda kwa undani zaidi kwenye hii Mikataba tukaona kwa kweli inatusaidia hususan Mkataba huu tunaotaka kuupitisha. Kwa sababu nilipouangalia kwa haraka nimeona tu kwamba kwa kweli labda tunazungumzia kwa sababu wengine wenzetu nchi za wakubwa zimesaini na wameridhia. Lakini sisi binafsi tutafaidika nini hasa ukitaka kuona undani wa faida zenyewe? Ukizisoma kwa undani utaona kwa kweli *as Tanzania,* hakuna kitu ambacho tunafaidika *as such.* Kwa sababu sisi kwa mfano, kama tukizungumzia ndege ya Tanzania, labda hiyo ya *ATC* ambayo iko, lakini kwenye mabano ni ya kwetu. Hii inaweza ikaruka wapi? Ukizingatia vyombo vyenyewe ni chakavu kupita kiasi, ukiangalia huduma hafifu na mambo mengine mengi, menejimenti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli nilikuwa nasema kwamba ni vyema tukubaliane kwamba tunafanya hivyo tu labda ili kunufaisha ndege nyingine, kwa sababu mimi kwa kweli sijaona labda baadaye Mheshimiwa Waziri ataweza tena kueleza vizuri faida hasa kama Mtanzania wa kawaida hususan wa Kilindi utamweleza kwamba nchi yako itafaidika hiki akaweza kukubali. Kwa kweli mimi binafsi sijaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nilitaka kuuliza: Je, ni jitihada gani basi endapo tunafikiria kuridhia Mkataba huu? Je, ni jitihada gani ambazo Serikali inaweka ili na sisi basi tuwe na chombo angalau kitaweza nacho ukiingia mahali tukasema na sisi tumefaidika. Yaani *Air Tanzania* inafanyiwa nini? Mambo ni mengi, utata ni mwingi, havieleweki, vinapanda, vinashuka. Lakini je, Serikali inafanya jitihada gani?

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli sasa hivi ni ulimwengu wa biashara huria. Labda sisi tukaribishe sasa madege mengine kwenda yakishuka, maana yake hawatakosa sababu ya kutua. Lakini vile vile niseme tu tahadhari. Hapa nimeangalia kwenye hii *agreement* ambayo tumepewa kwa haraka, sasa hivi naangalia nchi nyingi ambazo ziko kama sisi pia bado hazijaridhia: Je, wao hawaoni umuhimu wa huu Mkataba? Kwa mfano, Kenya, Uganda, hawa ni wenzetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Msumbiji, *Congo DRC*, wote hawa hawajaridhia, bila kutaja wengine wengi. Je, sababu ni ipi?

Papo hapo tunaona kwenye hiyo *document* inaonyesha nadhani *extract agreement,* unaonyesha kwamba Canada walijiunga mwaka 1945 wakajitoa mwaka 1988. Je, tumekwenda kwenye utafiti? Kwa nini walijitoa hawa? Maana yake tusijiingize tu halafu baadaye tunaanza kuulizana maswali aah! Ilikuwa tunaanza kupeleka kwenye Mahakama za Kimataifa. Mimi nilikuwa nafikiria ni vyema kabisa tuwe waangalifu, tujue pia na wenzetu kwa nini hawajasaini ambao wako kama sisi, kuna nini? Sidhani kama wote wameliacha bure.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu, nakwenda haraka haraka kwa ajili ya muda. Nilikuwa nasema ni vyema tukapata hii Mikataba mapema tukaweza kusoma kwa sababu sisi kama Wabunge sidhani kama sisi ni wataalam. Mimi mara nyingi hupata hii Mikataba halafu nikaenda kwa wataalam nikaomba ushauri ili kujua kwamba mambo yanakwenda vipi. Vinginevyo, hata wataalam pia tukawafuata na wananchi kwa ujumla ambao wana uelewa wa masuala mbalimbali. Lakini sasa unapoipata ukiwa ndani tena tayari imeshaanza kusomwa Azimio, kwa kweli ni ngumu kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati huo huo ukajaribu ku-*catch up* na yaliyoandikwa hapa. *(Makofi)*

Lakini nilikuwa najiuliza, Mkataba wa mwaka 1944, haujawa na marekebisho hata kidogo kwa kweli ndugu zangu! Maana yake lazima tuangalie hali halisi ya mwaka 1944 na hali iliyoko sasa hivi. Huu Mkataba upoje? Hatujaelezwa mahali kwamba labda uliwahi kuhuishwa mahali ukawa hivi ukawa vile. Tangu mwaka 1944, mambo ni yale yale? Mimi nadhani ni vyema tukaingia ndani tukaangalia na kwa kuangalia hii *extra* maana hata ile *convention* yenyewe hatujapewa, lakini kwa kuangalia kwa mfano pale *section* ya tatu, labda kama mimi sijaelewa maana yake, nacho Kiingereza cha kisheria siyo Kiingereza cha kawaida, lakini unasoma katika ile p*aragrap*h ya mwisho ya *sectin three,* inasema: *"A contracting State granting to the airlines of other contracting State the privilage to stop for non traffic purposes may require such airlines to offer reasonable commercial service at the points at which such stops abide."*

Sasa mimi nilipoiangalia kwa haraka ina maana pia wanaweza wakaruhusiwa *commercially.* Sasa kama wakiruhusiwa kibiashara mimi sielewi tena inakuwaje. Sasa tusije tukasaini huu Mkataba baadaye, wanakuja wanatubana na Mkataba kwamba jamani *commercially* mbona Mkataba umesema na nyinyi mmesaini? Hivyo ni vitu vya kuangalia. Lakini vile vile ukiangalia *Section two* ukurasa unaofuatia Na. 5 kwenye ile *extract* maana yake imetolewa vipengelepengele. Kwa hiyo, ni vigumu kufuatilia, kama nitakosea mtaniwia radhi. Inasema *paragraph* ya kwanza: *"If any disagreement between two or more contracting states relating to the interpretation or application of this*

*agreement can not be settled by negotiation, the provisions of chapter 18 of the above mensioned Convention shall be applicable."*

Sasa hiyo *Chapter 18* jamani inasemaje juu ya *Convention?* Tusije tukajifunga! Maana yake hapa imeelezwa tu *one sentence* tunasaini tunakuta mambo mengine magumu, jamaa wanafika na kuondoka wanavyotaka na itakuwa ni *too late* kama ambavyo tumeona mikataba mingi inakuwa ni ya ajabu ajabu. Tusije tukajikuta tumejifunga jamani! Hivyo nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri, labda baadaye utatuelimisha vizuri ili tunapopitisha kama Bunge la Awamu ya Nne nililosema la mtazamo huo ambao nimeutaja, tuwe tunafanya kitu cha uhakika.

**SPIKA:** Ni kitu gani hicho tena. Ni *alarm?* Naona ni makosa ya kiufundi tu. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo unaweza kuendelea.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Lakini mwisho kabisa, kwa kweli mimi nilikuwa nasema ninaona kwamba kuna kila haja ya kuangalia hii mikataba ambayo tunaridhia, kwa sababu kama hapa kuna msemaji mmoja alizungumza akasema tuwe waangalifu hasa kwenye mambo ya usalama.

Ni hivi karibuni tu tumeambiwa mbuga nyingi za wanyama zina vituo vya ndege. Vina viwanja vya ndege. Siyo hivyo tu, hata kwenye madini, tunajua kuna wachimbaji fulani fulani wana viwanja vya ndege ambapo ndege hutua kutoka nje zikafika na zikaondoka kwenda nje hata bila kufika kwetu. Sasa mimi naingiwa na hofu sana ikiwa tutakubali na baadhi ya hizo nchi nimeziangalia zimeridhia mkataba huu tutaweza kuwasimamia. Maana yake hata sasa hivi, usimamizi ni mgumu tu. Nitoe mfano mdogo, kumradhi. Kwa mfano kuna ndege mimi nazikuta kule, zinatoka nje, zinafika zinapaki pale KIA. Kuna ndege nyingine kama aina ya kijeshi ambayo imetoka huko huko ilitangulia kufika, vitu vinatolewa kwenye ndege moja vinaingizwa kwenye ile ndege bila *immigration* kusema lolote na halafu tena watu wote wapo walinzi, vinatolewa vinaingizwa mle ndani na ile ndege inaondoka inakwenda mbugani. Tunajua tumefanya nini? Hilo tu linatushinda kulisimamia.

Mheshimiwa Spika, nia yangu na kusudio langu hapa kusema, sidhani kama tuko tayari kuweza kusimamia mambo kama haya. Nadhani labda tungemaliza kwanza mambo yetu ya ndani, uchafu uchafu huu mdogo mdogo tukausafisha, tukawa na usimamizi madhubuti na wataalam kama wasemaji wengine walivyosema wataalam wa uhakika wa kuweza kusimamia mambo haya, kabla hatujaridhia mikataba mikubwa mikubwa ambayo baadaye itatushinda halafu tutaanza kunyosheana vidole.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, binafsi ninasema ninaunga mkono, lakini ninatumaini kwamba hilo halitamzuia Mheshimiwa Waziri kutoa majibu ambayo yatawezesha Bunge hili ili baadaye lisiweze kuaibika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaona ule muda uliosalia hautoshelezi Mheshimiwa Waziri kuweza kujibu hoja zilizojitokeza na nadhani ni vizuri tu tufikie hapo. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11 jioni.

*(Saa 6.54 Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa kwa kipindi cha asubuhi tumemaliza kuwasikiliza wale wote waliokuwa wanachangia haya Maazimio. Kwa hiyo sasa ni zamu ya Mtoa Hoja, kwa hiyo ataaanza kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri ambaye ndiye mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kabla ya hapo na mimi nijiunge na wenzangu ambao wamewapongeza wale wenzetu ambao tumewachagua kuingia katika Bunge la Afrika ya Mashariki katika wiki iliyopita. Nami bila shaka wengi wenu mnajua furaha gani niliyonayo kwa uchaguzi ule. Lakini vile vile nimpongeze Katibu mpya wa Kamati ya Wabunge wa CCM aliyechaguliwa katika hii *week-end* iliyopita, Mheshimiwa Ameir, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kueleza wazi wazi kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, hoja zote nne ambazo ni Maazimio ya Mkataba ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu, nitajaribu kujibu baadhi tu ya hoja za Wabunge na Mheshimiwa Waziri ambaye ndiye mtoa hoja atakamilisha kwa kujibu hoja nyingine ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe - Mbunge wa Kyela, alipokuwa akichangia kwa maandishi alitoa maoni yake na mapendekezo yake. Kubwa alitaka kujua *financial implications* za uanachama wetu, kwa maana kwamba je, ni ada gani tutakazokuwa tunalipa kwa mwaka na matakwa mengine yanayohitaji fedha?

Labda niseme tu kwamba kujiunga kwetu katika kuridhia maazimio haya, kwanza tutahitajika kugharamia ujenzi wa *reception facilities*, lakini vile vile gharama za mafunzo kwa wataalam kama ambavyo wengi walitoa hoja na wachangiaji walivyoulizia na kusisitiza kuhusu umuhimu wa mafunzo kwa wataalam. Lakini kama mnavyojua, nchi yetu kwa sababu ni mwanachama wa *IMO,* tunalipia *Pound* 3,500 kila mwaka ingawa hii ni kwa ajili ya kujiunga kwetu na *IMO* na faida zote tunazipata kutokana na kujiunga huko na siyo tu kwa ajili ya mikataba hii minne.

Lakini vile vile kama ambavyo Wabunge wengi walivyosema, kuna gharama za ununuzi wa vifaa vya kufanyia doria na hili lazima kama Serikali itabidi tugharamie. Lakini Mheshimiwa Mwakyembe vile vile akichangia ule Mkataba wa *BASA* aliliuliza ni faida gani ambazo zitapatikana?

Sasa moja ya faida ambayo Serikali yetu itapata kwa kuridhia Mkataba wa *BASA*, ni kupunguza usumbufu na muda wa kuruhusu ndege za kimataifa zenye ratiba maalum kupita kwenye anga la nchi nyingine. Kama hatukuridhia, italazimika kila mara tuwe tunakaa na nchi hizo chini ya *Bilateral Air Service Agreements.* Utaratibu wa *BASA* unachukua muda, na pia ni gharama kwa wataalam. Lakini pia pamoja na kwamba Tanzania haina ndege nyingi zenye ratiba, *scheduled airlines,* lakini tutafaidika kwa ndege za nchi nyingine kupita kwenye anga letu, kwani ndege za namna hiyo zinatozwa ada kwa kupitia kwenye anga letu. Ada hizo ni: *Air Navigation Services,* pamoja na *over flight services* ambazo hutozwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga *TCAA.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Mwalyosyi - Mbunge wa Ludewa, akichangia kwa maandishi na vile vile kwa kuzungumza, alizungumzia, kwamba kunahitajika kuwa na *benchmark* au *base line conditions* ili kujua tofauti kati ya kabla ya na baada ya uchafuzi. Vile vile alizungumzia kwamba kuna haja ya kuainisha hali ya mazingira ya maeneo yetu. Ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi tunaupokea na tutauzingatia.

Aidha, katika kukamilisha mpango wa kushughulikia mpango wa uchafuzi wa mafuzi wa mafuta, yaani *oil polution respons*e *and preparedness,* Serikali kupitia *SUMATRA* inaandaa na kufanya *sensitivity maping* ya mwambao wetu. Zoezi hili litabainisha hali ya Mwambao wetu na kuonyesha hali ilivyo kabla ya uchafuzi. Mawasiliano yameanza ikiwa ni pamoja na wataam na wafadhili wa nje *IMO* kuwezesha zoezi hili kufanyika mapema na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, naye alichangia kwa maandishi na aliulizia kama *SUMATRA* inao uwezo wa kulinda doria ya bahari zetu kwa kutumia ndege, maboti na maboti yaendayo kwa kasi na akauliza kama kuna *disaster management* ya kutosha na vile vile kwamba tukiridhia Mikataba hii, tutapata nafasi ya kupata huduma na misaada ya kimataifa? Labda tujibu tu kwamba, Jeshi la *Navy* kwa kushirikikiana na *TPA,* hufanya doria hiyo kwa kutumia boti chache zilizopo. Lakini suala hili litazingatiwa wakati tunaimarisha uwezo wetu wa kufanya doria kwa ajili ya kusimamia mikataba hii.

Lakini nchi ikiridhia mikataba hii inakuwa mwanachama wa *IMO,* hivyo inapata *technical assistance* kutoka *IMO* kama kutoa mafunzo kwa wataalam, kuendesha semina na warsha zinazohusu mikataba ili kuwaelimisha wadau wote, watumiaji wa miongozo ya mikataba na pia kusaidia katika vifaa na nyenzo za kusaidia kutekeleza mikataba hiyo. Pia, nchi ikipata janga hilo itasaidiwa na nchi jirani ambayo ni mwanachama kusaidia kuondoa uchafu baharini ikiwa nchi inayohusika haina vifaa au nyenzo za kutosha kuondoa uchafu huo. *IMO* pia hutuma wataalam wa kusaidia kuondoa uchafu huo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mwingine aliyechangia kwa maandishi alikuwa ni Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, ambaye aliulizia kwamba, kwa Serikali ya Tanzania kuridhia Mkataba wa *BASA,* baadhi ya mataifa makubwa yanaweza kutumia mwanya huu kwa kufanya uchunguzi wa kiharamia, yaani *spying activities* na kwa kweli hili liliulizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Sasa akauliza kwamba, Serikali

iwe na utaratibu wa kufuatilia safari hizo ili anga letu lisije likatumiwa kwa shughuli za kijasusi. Kwa kweli ni mawazo au maoni mazuri na sisi tunasema kwamba Wizara inachukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

Hata hivyo kama tulivyoeleza, Mkataba wa *BASA* unahusu ndege za kiraia na zenye safari za kibiashara tu. Kwa hiyo, ndege za kijeshi hazihusiki na hili anga letu kama kawaida litalindwa vile vile na Jeshi letu la Wananchi kama ambavyo tumeeleza katika sehemu nyingine. Lakini pili, ndege nyingine zote zikiwemo ndege za kijeshi zina taratibu zake kama nilivyosema. Kwa kawaida, ndege za aina hiyo zinaratibiwa na Wizara hiyo ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa Wizara ya Miundombinu inashirikiana kwa karibu na vyombo vya Ulinzi na Usalama na itaendelea kufanya hivyo ili anga letu liendelee kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi ya yale ambayo yalizungumzwa kama mchango wa Wabunge wakati wakichangia hoja hii. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Waziri atakuja kutoa maelezo ya baadhi ya michango ya Wabunge wengine waliobaki ingawa kama Naibu Waziri wa Wizara ya Miundombinu. Nilivyosema kwa kweli mengi yalikuwa yanajirudia na sisi tumeyachukua yote ambayo yametolewa kama maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, ninaomba nieleze kwamba ninaunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ninamwita Mtoa Hoja, Waziri wa Miundombinu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshmiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya pili mchana huu ili niweze kuhitimisha hoja yangu iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwanza na mimi nikupongeze sana kwa vazi lako la mwambao. Nami nadhani nitajitahidi nitembelee Zanzibar mara kwa mara ikiwezekana nitapata na mimi, labda na vitu vingine zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri katika kuwapongeza viongozi mbalimbali ambao wamebahatika kupata nyadhifa kama Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki. Ninawapongeza na tunawakia kazi njema katika kujenga Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na pia nimshukuru sana na kumpongeza Katibu wetu wa Chama cha Mapainduzi, Mheshimiwa Ameir kwa bahati aliyoipata. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, niliwasilisha maazimio manne kuhusiana na Mikataba ya Kimataifa minne, ambayo tunaomba Bunge lako Tukufu liweze kukubali hoja ya Serikali ya kuridhia Mikataba hii. Ina umuhimu wa kipekee, katika mazingira tuliyonayo hivi sasa. Lakini kabla ya kujibu hoja za Wabunge, nianze tena kuwatambua Wabunge waliochangia hoja hii.

Nianze kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi, nao ni kama wafuatao:- Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Guido G.

Sigonda, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosyi na mwisho kwa kutajwa lakini siyo kwa umuhimu, Mheshimiwa Ibrahim Sanya. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kutoa kauli humu Bungeni ni Waheshimiwa wafutao:- Mheshimiwa Mwaka Ramadhani, ambaye aliwasilisha Taarifa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif - Msemaji wa Upinzani kwa hoja hii humu Bungeni. Mwingine ni Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Col. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, na mwisho Dr. Milton M. Mahanga, Mbunge na Naibu Waziri wa Miundombinu. Wote hao ninawashukuru sana kwa michango yao mizuri, wametupatia ushauri, mwongozo na maangalizo ambayo ninadhani ni muhimu katika kutekeleza mikataba hii. *(Makofi)*

Ninashukuru wote wametuunga mkono, pamoja na maangalizo ambayo wengi wametoa, lakini sio wengi wote wamesema tunaunga mkono, lakini yapo haya ambayo ni vizuri tukayafanyia kazi. Tunawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge.

Lakini pia niwasshukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi ambazo wamenipa, wale waliosimama na kutoa kauli humu Bungeni na wale ambao wameniletea kwa maandishi salamu za pongezi tangu niteuliwe kuwa Waziri wa Miundombinu. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na hasa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwamba nitahakikisha kwamba tunafanya kazi kwa karibu, kwa sababu lengo letu ni moja.

Kamati ya Miundombinu kusema kweli ni jicho la karibu sana kwa Wizara hii na ndiyo maana tutajitahidi sana inapowezekana, tuwe na muono mmoja. Lakini pale ambapo tutafoutiana kidogo naamini itakuwa ni kwa sababu za msingi ambazo Serikali itaeleza kwa nini tunatofautiana kidogo na nyinyi. Lakini kwa ujumla, mimi nimefarijika sana tangu nilipoanza kukutana na nyinyi kwenye Kamati kule Dar es Salaam na haya ambayo mnaendelea kunisaidia nathamini sana ushauri wenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Kama nilivyosema, wameunga mkono lakini kulikuwa na maeneo ambayo wametoa ushauri. Nikianza na la kwanza, Serikali itenge Bajeti ya kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa Mikataba iliyoridhiwa. Amelisema Mhehsimiwa Naibu Waziri na sisi tunakubali, mnatusemea, tutakapokuwa kwenye Bajeti mtusemee. Lakini yote haya yataweza kufanyika kwa kutegemea uwezo wa uchumi wa nchi yetu. Ninaamini kadri uchumi unavyokua, ndivyo Serikali itakavyozidi kutenga fedha za kutosha katika bajeti yake ili kuwezesha kutekeleza hii Mikataba ambayo Bunge lako tunaliomba likubali kuridhia. Imetolewa hoja kwamba Serikali ifanye kila linalowezekana ili Mikataba kama hii iwe inaridhiwa na Bunge mapema na kwa wakati. Mimi ninakubalina sana na hoja hii. Tunalizingatia sana hili. Katika kuwasilisha Mikataba hii leo. Sisi Wizarani tunaamini kuwa ni hatua ya utekelezaji wa ushauri huu. Lakini tutajitahidi kwa Mikataba ambayo inaangukia chini ya usimamizi wa Wizara hii tuweze kwenda kwa kasi kidogo ili iweze kufika humu Bungeni.

Serikali iweke mikakati ya kuwezesha kutekelezwa kwa Maazimio hayo. Ni kweli tunakubali na ndiyo maana hata katika maelezo yangu nilisema kwa nini hatukuridhia Mikataba hii huko nyuma. Ukiondoa ule wa *BASA,* ukiangalia ile miwili ya *Polution,* kama mlivyosema na nyinyi inashabihiana sana. Ile ya kuruhusu kupita anga la nchi Mwanachama, tulieleza sababu, kwa sababu kila nchi inaangalia maslahi yake. Lakini kubwa zaidi tulisema ambalo ndiyo hoja yetu Waheshimiwa Wabunge, kwamba mmejiandaa vipi?

Mheshimiwa Spika, ndio tukasema wakati ule shughuli hizi, kama unavyokumbuka zilikuwa zinaendeshwa kutoka Wizarani. Waziri mwenye dhamana ya masuala haya ndiye alikuwa *Regulator,* ndiye alikuwa mdhibiti. Sasa kimeundwa chombo mahususi cha kusimamia masuala haya na ndio tukasema Serikali itaendelea kukiimarisha chombo hiki kwa kukipatia wataalam, kwa kukipatia nyenzo za kufanyia kazi na vyombo vingine ambavyo vitaleta tija katika utendaji kazi wa chombo hiki. Kwa hiyo, hilo tunalikubali, tutakwenda nalo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasema, Serikali izifanyie marekebisho Sheria zilizopo ambazo zina mapungufu au kutunga sheria mpya kwa maeneo ambayo yanahusishwa na mikataba hii. Hii ni sahihi kabisa, tunakubaliana na ushauri huo. Kwa kusema kweli, tulishaanza kazi hii.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika sheria yetu ya *Merchant Shipping,* Sheria Na.21 ya mwaka 2003, suala hili tuliliongea sana na tuliingiza kifungu kinachomwezesha Waziri mwenye dhamana ya masuala haya kutayarisha Kanuni na Sheria za kutekeleza Mikataba ya Kimataifa inayohusu masuala ya Bahari ambayo sasa leo ndio tunaliomba Bunge lako hili Tukufu liridhie.

Kwa maana hiyo, hiyo ni lazima tufanye na Sheria nyingine ambazo zipo lazima tutekeleze Mikataba hii kwa kuzifanyia ile *fine tuning* ili ziendane na matakwa haya ya mikataba ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sasa inakuwa mwanachama katika Jumuiya za kimataifa kuhusiana na hiyo. Hilo tutaendelea kulifanya.

Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye amegusia Mikataba miwili, yaani uharibifu wa Mazingira kwa makusudi kabisa mtu anatupa taka, ile *polution by dumping of waste and other materials.* Halafu kuna ile uchafuzi tu wa mazingira unatokana na Meli. Ameielezea vizuri. Sisi cha kusema ni kwamba tunakubaliana naye kwa ushauri mzuri alioutoa na tutauzingatia kwa kadri tutakavyoweza maana Bajeti kama ulivyosema ndiyo hiyo inavyoturuhusu kwa sasa.

*SUMATRA* iwe na uwezo mkubwa, ameshauri kwa upande wa wataalam na nyenzo. Kwa upande wa wataalam na nyenzo tutafute misaada ya vifaa hasa kwenye Doria. Yote haya sisi hatuna tatizo nalo. Kwa kusema kweli, ukiliangalia suala katika upana wake, ndiyo maana tumesema baadhi ya faida ambayo Tanzania itapata katika kuwa mwanachama wa vyombo hivi ni ile misaada ya kiufundi ambayo tunapata. Misaada ya Mafunzo na vifaa.

Lakini lile la Doria la vifaa vile ambavyo ninafahamu, vile vifaa vikubwa ni jukumu la Serikali yenyewe. Naamini kwa sababu tunashirikiana, Serikali ni moja, lakini imegawa majukumu. Lakini eneo hili unalifanikisha zaidi kama Jeshi lako kwa upande wa wanamaji unaliimarisha. Kwa hiyo, haya ndiyo tunayoyasema vizuri. Nitoe mfano mmoja. Wakati fulani nikiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tuliletewa Taarifa kwamba katika Ukanda wa Uchumi kulikuwa na Meli tatu zimeingia tu, wanavua. Walikuwa wame-*camp* pale kwa karibu ya wiki moja.

Tuliviarifu vyombo, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Sasa ndio tunaongelea mambo ya *preparedness*. Tulijitahidi sana lakini katika kipindi ambacho wale walikuwa na ndege ya kutelekeza mpaka tufike karibu na eneo hilo, tulipoteza kama saa mbili na nusu hivi tunatafuta mafuta. Huo ndio ukweli.

Mnaposema *preparedness,* maana yake ndiyo hiyo, wakati wowote ukisikia taarifa, unaondoka. Kwa hiyo, ndege ile ambayo tulikuwa tumepewa, tulikwenda kwenye eneo hilo, tukakuta ndiyo wanaanza jamaa wameshatoka nje ya maji yetu, wako sasa wanaingia kwenye bahari kuu. Hayo yalikuwa ni mambo ya uvuvi haramu, waliingia kuvamia. Lakini ingelikuwa sasa ni katika masuala kama alivyoeleza Mheshimiwa Habib Mnyaa, kwamba waliona *tanker* linasafishwa wanamwaga takataka. Kama una vyombo vyako na kwa *technology* ya leo, ukisha *record* tu *registration* ya ile meli, mnaanza ile *process,* mchakato wa kuanza kuwasilisha madai kwamba wajue mliingia katika eneo letu na mmefanya yale ambayo hairuhusiwi na Mkataba huo.

Kwa hiyo, hayo aliyoyasema Mheshimiwa Hilda Ngoye sisi tunakubaliana naye kabisa. Nisema tunayafanya, niunganishe na hoja ya Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, kwa Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Ni kweli kwa upande wa Ziwa Victoria tumekwenda mbali sana, kwa sababu ya mashirikiano yetu katika Afrika ya Mashariki, kazi nzuri sana inaendelea kwa *aspect* hii ya uharibifu wa mazingira.

Tunaamini kwa upande wa Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, kutokana na uanachama wetu, pamoja na kwamba Shirika la Kimataifa linashughulikia usalama wa usafiri wa majini, halijishughulishi na maziwa haya, kwa maana ya *internal waters.* Lakini kwa umuhimu wa kipekee wa Maziwa haya, Serikali imewahi kufanya warsha nchini kwa msaada wa shirika hilo la kimataifa kuhisiana na matatizo yaliyopo Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Ndiyo maana tunaona tufanufaika zaidi iwapo Tanzania itakuwa Mwanachama wa Mikataba ambayo tunapendekeza tuwe. Lakini hizi ni sehemu za *challenges,* tutafanikiwa hapa na pale, kuna maeneo mengine hatufanyi vizuri lakini kama Serikali tunasema tumedhamiria kabisa kuhakisha kwamba Mikataba hii tunaisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, alieleza Mikataba imechelewa. Ni afadhali kuchelewa kuliko kutokufika kabisa, tumefika sasa. *SUMATRA* ipo sasa, wataalam wale wapo, tutaendelea kuimarisha kama inavyosema na Mikataba ambayo haijaridhiwa tuilete, sisi tutaendelea kuileta ile ambayo inaangukia chini ya *potfolio* ya Wizara yangu, lakini Serikali ni moja, Mwanasheria Mkuu yupo atakuwa anawahimiza.

*Foreign Affairs* wapo, watakuwa wanatukumbusha tuyafanye haya, ni mema. Kwa sababu nchi ime-*sign* Mkataba, walikuwa na sababu kwa nini Rais walimshauri akubali. Sasa tunakuja kulieleza Bunge kuwaeleza wananchi kwamba tuliyafanya haya kwa nia njema, tunaomba sasa tufikishe hatua ya mwisho ili tunufaike na matunda haya.

Ulitolewa ushauri ya kuwa tufuatilie meli zinazochafua mazingira kwa makusudi. Kama ilivyoelezwa kuhusu ma-*tank,* yanayofanya uchafuzi huo. Ni kweli doria inaendelea kufanyika na tunashukuru pale ambapo mnatupatia taarifa za haraka ili hatua mahususi zichuliwe. Uchafuzi wa mazingira ya bahari kutoka nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli Mikataba hii haihusiani na uchafuzi unaofanywa wa mazingira kuelekea baharini kutoka nchi kavu. Lakini tuna sheria kama mnavyofahamu ya masuala haya na suala hili linashughulikiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kama alivyosema hata yeye mwenyewe Mheshimiwa Mohamed Mnyaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tanzania kusaidia Zanzibar kujiunga na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Usafiri Majini, Tanzania maana yake ni Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ninavyoelewa mimi. Kwa vile chombo hiki ni cha Kimataifa na ni Taifa pekee ambalo linaweza kuwa mwanachama kule, sasa fursa zinazopatikana na uanachama wetu kama Jamhuri ya Muungano, faida hizo ndiyo tungependa tunufaike wote. Hiyo hoja mnanielewa. Mimi nataka tunufaike wote. Mafunzo haya, juzi tuliambiwa zipo nafasi za mafunzo. Sasa tukipata nafasi ya *scholarship* kumi, kwa nini tatu au nne zisitoke Zanzibar na hayo ndiyo matunda ya uanachama wetu katika vyombo hivi vya Kimataifa ambapo Jamhuri ya Muungano ndiyo mwanachama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *SUMATRA* maoni ya Kamati ya Bunge, samahani niliiruka tu lakini ni yale yale ya kuimarisha chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema kuwepo na teknolojia ya vyombo vya doria na uwezo wa kutoa taarifa kuhusu uchafuzi wa mazingira baharini. Nimelielezea, lakini niseme tu kwamba Serikali inaendelea kuimarisha vyombo vya doria na pia Kituo cha Mawasiliano, yaani *Maritime Tour* ambacho kitakuwa na *less communications*.

Pale unapoingia karibu na mlango wa bahari, pale Dar es Salaam karibu na Ofisi ya Rais, Utumishi, unaona kuna *tour* ndefu hivi ambayo inajengwa, ni kwa msaada wa *IMO* ambapo tunajenga huo mnara ambao utakuwa na vifaa vya kisasa kweli kweli vya mawasiliano na kugundua vyombo kwa uhakika kabisa kwamba chombo hicho ni cha nchi gani. *Registration* yake ndiyo yale nilikuwa nawaelezeni tutakuwa navyo sasa kutokana na msaada huo, lakini pia na sisi katika kujiandaa katika mkao ambao unawezesha nchi yetu kunufaika na uanachama wetu.

Mheshimiwa Spika, *SUMATRA* itambue athari za taka zinazotupwa baharini kwa kutumia *TBS* na Mkemia Mkuu, Serikali inafanya shughuli hizi kuchukua *samples* hizo kabla ya *SUMATRA* haija *move in*. *Reception facilities* zitajengwa wapi? Kwa sababu haya yanaletwa na Meli. Kwa *hiyo, naturally* inakuwa rahisi sana. Kama mnataka eneo bandarini, eneo ambalo mtakubaliana nalo, sasa hili ni la kitaalamu sana lakini lazima

iwe mahali ambapo pawekwa hapo. Kusema kweli ukisoma ile Mikataba kwa ukaribu unaelewa. Waheshimiwa Wabunge mna kazi nyingi sana hamna nafasi ya kuisoma vizuri. Lakini hata pale ambapo mnakubali kwamba kata hii hairuhusiwi sufuli huwezi kuileta hapa, unaifahamu vipi, mmesema wataalam.

Lakini hata katika kundi la pili, ambapo unahitaji kibali maalum na kundi la tatu, kibali cha ujumla kuna miongozo ambayo imewekwa kabisa ya kufuatwa kama ni *radio active materials,* kuna *guidelines* ambazo zimetolewa na *International Atomic Energy Agency* hizi ni za Kimataifa na unataka uzizingatie. Kwa hiyo, yote haya yanahitaji tukayazingatie kama nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni ameuliza tumejiandaa vipi? Ni haya niliyoelezea , ile *maritime tour* ambayo tunajenga. Kwanza, niseme nampongeza sana rafiki yangu Mheshimiwa Feteh Mgeni. Katika Bunge lililopita nilimwona ni mtu makini sana, anapenda sana haya mambo. Siku moja nikamwuliza, wewe rafiki yangu mbona mambo ya majini unayaelewa sana? Akaseme ndiyo, akanipa *background* yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Feteh Mgeni ni mtu mahiri sana na amenieleza mengi ambayo mimi kwa shughuli za baharini nilikuwa sifahamu ndiyo utajiri wa Bunge hili. Namshukuru Mheshimiwa Feteh Mgeni kwa mchango wake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi ndiye mwenyewe huyu wa mazingira, lakini ameelezea vizuri sana. Naibu Waziri wangu wakati anajibu hayo aliyoyaeleza upande wa *accidental spills* na ile ya makusudi, lakini sisi tunakubaliana naye kabisa hata hizi *accidental spills,* ni hatari sana. Maana inakwenda pole pole, lakini athari yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, ndiyo maana sisi katika maandalizi yetu tunataka tuzamie kidogo kupitia *SUMATRA*, wengine tujenge uwezo wa ndani wa vyombo vya Serikali. Mnafahamu hatuwezi tukafanya shughuli hizi kama mganga wa kienyeji.

Mheshimiwa Spika, unajua mganga wa kienyeji, yeye ana dawa zake, hataki afahamishwe mtu mwingine jinsi ya kuzichanganya zile dawa labda amwonyeshe mtoto wake anayempenda sana, lakini hamwonyeshi dawa zote, ni yeye tu. Sasa sisi hatuwezi kufanya shughuli hii kwa namna hiyo. Ndiyo maana katika kujenga uwezo ndani ya nchi yetu *SUMATRA* ni chombo kimojawapo tu. Lakini tungelipenda vyombo vikuu vyetu hivi *NEMC* na wengine kwamba tujione kama kitu kimoja katika eneo hilo. Kwa sababu kufanikiwa kwa eneo moja ni kufanikisha pia eneo lingine. Kwa hiyo, hili sisi tunaliona katika mtazamo mpana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr Harrison Mwakyembe namshukuru, lakini sitarudi kwa sababu Naibu Waziri wangu amelisemea vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ibrahim Sanya aliuliza: Je, *SMZ* inayo Sheria ya Anga au inasimamiwa na *DCA*? *Of course DCA* sasa hivi inaitwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga *TCAA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina sheria yake yenyewe kuhusu udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga. Sheria inayotumika ni *the*

*Tanzania Civil Aviation Act* ya mwaka 1977 pamoja na Tanzania *Civil Aviation Authority* ya mwaka 2003. Sheria hizi mbili ni za Muungano. Kwa hiyo, zinatumika na Zanzibar. Aliuliza pia je, ndege zinazopita kwenye Anga letu huwa zinafanya malipo yoyote? Hili amelieleza vizuri sana Naibu Waziri wangu.

Lakini napenda nirudie ndiyo *over fly* hii siyo ya bure. Lakini ili malipo hayo tuweze kunufaika nayo ambayo katika mwaka 2005/2006 Serikali ilikusanya kama Shilingi bilioni tano kutokana na shughuli hizi. Sasa aliuliza je, tunajuaje ndege hizi zipitazo angani wakati hatuna *coverage* ya *satellite* kwa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, ndege zote za kiraia zinazopita kwenye anga la Tanzania zinafahamika. Kwa sasa hivi nchi yetu najivuna kusema kwamba uwezo wa kutambua ndege hizo tunao. Hilo wala lisitutie wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ndege ambazo sio za kiraia za kijeshi kwa mfano, tuna utaratibu mwingine ndio maana nimesema ni mgawanyo tu wa majukumu, lakini Serikali ni moja. Kwa hiyo, kwa kundi hilo la ndege Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga la Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndizo zinazofanya kazi ku-*clear* huyo anayetaka kupita kwenye anga yetu.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukajaribu kupita kama unadhani wewe ni mjanja, lakini hatari ya kutunguliwa ni kubwa sana na ndiyo maana wengi wanaogopa haya, lazima tu utoe taarifa mapema. Kwa hiyo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inapokea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakishirikiana sasa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ndiyo wanasema sawa au hapana. Wakisema hapana, basi ni hapana, ukijaribu basi yatakayokupata itakuwa ni ya kwao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Dr. Guido Sigonda naye aliuliza kwa maneno yake mwenyewe lakini hayo hayo. Lakini niseme tunauchukua ushauri wake, lakini kama tulivyoeleza Mkataba wa *International Aviation Service Transit Agreement* unahusu ndege za kiraia na siyo zenye safari hizo za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba haya ndiyo maelekezo ambayo Wizara imepewa na Serikali wakati inaidhinisha kuridhiwa kwa Mkataba huu na Serikali imeelekeza wazi kabisa kwamba wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu Mamlaka zinazohusika ikiwemo Wizara yangu zilijidhatiti ipasavyo hasa katika usimamizi wa ndege hizo ambazo Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda na wengine ambazo zinaweza kupita juu ya anga yetu bila taarifa au kupita bila kupata kibali kwa kisingizio cha Mkataba huu wa BASA.

Mheshimiwa Spika, sasa suala hili la Usalama wa Anga tunapenda kabisa tuwahakikishie kwamba tunalisimamia kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo amesema kuna ndege zinazofika toka nje kwenda kwenye Mbuga za wanyama na migodi na kuondoka bila udhibiti. Kwa mfano, Kilimanjaro *Airport* kuna ndege kama za kivita zinashusha mizigo

na kuingiza katika ndege ndogo na kuondoka bila kuwepo Maafisa wa Uhamiaji na wa Forodha.

Mheshimiwa Spika, napenda tu nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Anga ya mwaka 1997 ambayo nimeitaja, ndege yoyote kutoka nje haiwezi kutua katika kiwanja ambacho hakiruhusiwi, yaani siyo *designated entry or exit point* ambako wanakuwepo Maafisa wa Uhamiaji na Forodha. Pale ambapo wanataka kwenda moja kwa moja bila kupitia katika hizi *entry or exit point* kiwanja kilichoombewa maombi kwamba wanakwenda kule au kuondokea kule, basi utaratibu wa kutoa idhini unafanywa baada ya *TCAA* kuthibitisha kuwa Maafisa wa Forodha na Uhamiaji watakuwepo kama hawatakuwepo kibali hakitolewi ng'o. Huo ndiyo utaratibu.

Sasa tungependa sana sisi tuelezwe kama Serikali kama kuna mahali ambapo utaratibu huu ambao upo wazi wa kisheria hauzingatiwi. Pale *KIA* mimi ninafahamu utaratibu huu unazingatiwa. Sasa kama kuna ushahidi kamili, sisi kama Serikali tungelipenda sana tupewe hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ameendelea kusema, baadhi ya nchi zikiwemo Kenya, Uganda, Jamhuri ya Demokrasi ya Kongo hazijaridhia Mkataba wa BASA kwa nini sisi tunakwenda kichwa kichwa?

Mheshimiwa Spika, nimeelezea kwa nini hatukuuridhia Mkataba huu huko nyuma na nimjibu pia Mheshimiwa Mohamed Mnyaa hapa Mkataba wa mwaka 1944 mlikuwa wapi? Mwaka 1944 mimi nilikuwa sijazaliwa hata nchi hii ya Tanganyika na ya Zanzibar zilikuwa hazijazaliwa kama nchi huru. Kwa hiyo, yule aliyekuwa anatutawala, ukisoma rekodi, yeye ndiye aliandika akasema anayafanya haya kwa niaba yake na makoloni yake.

Tanganyika ilipopata uhuru ilitoa taarifa kwa Jumuiya ya Kimataifa kwamba Mikataba yote hatuitambui. Lakini ikaendelea kusema hivi, ndani ya kipindi cha miaka miwili tutapenda kufanya mazungumzo na nchi ambazo ni sehemu ya Mikataba ambayo Waingereza walikuwa wametia saini kwa niaba ya Tanganyika. Mmojawapo ulikuwa ni Mkataba huu, kwa vile wao walikuwa wamesaini, sisi tukasema hii tutakwenda nayo, lakini tuliutambua kwa maana kwamba upo, lakini kwa sababu ya harakati za mapambano ya Kusini mwa Afrika ndiyo maana tulisema sisi hatukushabikia sana kuuridhia wakati huo Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Mikataba yote ile ambayo Waingereza walikuwa wameweka saini kwa niaba ya wananchi wa Tanganyika tulikuja tukaikubali isipokuwa Mikataba miwili tu. Nilieleza *last time,* ni mikataba ile ya Nile *Water Agreements* pamoja *Belbes Agreement* kwa Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Kigoma. Mikataba miwili hiyo tulisema tutaongea na wahusika kama wanataka, lakini kwa masharti ya kuleta *equitable benefit* kwa pande zote.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo sura. Lakini kwa sasa hivi tunasema kila nchi inaangalia maslahi yake, siwezi kuzisemea Uganda, Kenya na *DRC*. Lakini hiyo ndiyo sura kwa

upande wa Tanzania. Ameuliza pia kuhusu Ibara ya 14 ya Mkataba Mkuu wa *ICAO*. Ibara hiyo ni ya namna ya kutatua migogoro. Amesema mbona hatuoni ina-*make reference* hapa, lakini utaratibu utakaofuatwa ni ule uliotajwa katika Ibara hiyo. Sasa Ibara hiyo inasema nini? *Chapter* hiyo inasema nini?

Mheshimiwa Spika, kusema kweli ni kwa sababu niliyoeleza hatukuweza kuyaleta yote yale maana yalikuwa mengi. Lakini Mikataba hii kama ilivyo Mikataba yote ya Kimataifa, hatua ya kwanza ya mgogoro ni kutatua mgogoro, unaanza na utaratibu wa usuluhishi mwone kama tofauti ambazo zinawafanya mwende *apart*, je, hamwezi mkazimaliza kwa mazungumzo tu?. Ikishindakana ndiyo sasa kila upande unapewa haki ya kwenda kwenye *arbitration*. Sasa *arbitration* ina utaratibu wake. *Mediation* hii inaweza ikakubali yaliyosemwa na huyo *mediator* au ikakataa.

Kwenye *arbitration* unafungwa, lazima uyakubali hayo na Mkataba huu unasema wazi maana hata kwenye *arbitration* mnataka mteue watu ambao watawasaidia kumaliza mzozo wenu, aidha, mmoja na mara nyingi mnakuwa watatu. Lakini pia unaweza kukuta nchi imekaidi tu inasema muda wa kuteua huyo mmoja wa wasuluhishi ni siku 30, zinapita siku 30 hawateui, unafanya nini? Wewe usubiri tena huku unaumia.

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mwanasheria huwezi ukakubali. Kwa hiyo, ndiyo maana Mikataba hii inasema kama nchi itakaidi kuteua Mjumbe wake atakayekaa kwenye *panel* hiyo ya kuamua *dispute* hiyo basi Mkataba huu unatamka jinsi huyo atakavyopatikana, atateuliwa huyo mtu na chombo kingine, akipatikana yule ambaye wewe ulikataa kumteua, basi hao wawili wanatafuta mtu mwingine wa watatu ili awe miongoni mwao na ndiye anakuwa Mwenyekiti. Huo ndio utaratibu uliopo katika Mkataba huu. Ni taratibu za kawaida tu.

Mheshimiwa Spika, lakini hizo ndizo zilikuwa hoja za jumla ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Lakini nimalizie kama nilivyoanza kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha haya Maazimio manne ili nchi yetu iridhie Mikataba hii muhimu katika kuendeleza maendeleo ya nchi yetu, ulinzi na usalama wa nchi yetu, lakini pia kuwa sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa maelezo hayo fasaha.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefikia hatua ambayo ni kuridhia hayo Maazimio mbalimbali. Mtakumbuka kwamba utaratibu hadi hatua hii umekuwa ni kwamba mtoa hoja aliyewasilisha Maazimio yote kwa pamoja.

Mwenyekiti au Msemaji wa Kamati ya Miundombinu naye alitoa maoni ya Kamati yake kwa pamoja. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani hivyo hivyo maoni yalikuwa kwa pamoja. Hatimaye michango pia ilikuwa katika sura hiyo hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia walikuwa wanachagua pale wanapotaka katika Maazimio yote manne na ndiyo basi Naibu Waziri wa Miundombinu pamoja na Mtoa Hoja nao wamewajibu hivyo hivyo kwa kupitia Maazimio yote.

Lakini sasa kwenye hatua hii hatuwezi kupitisha Maazimio manne kwa pamoja, itabidi niwahoji kwa Azimio moja baada ya lingine. Kwa hiyo, kila Azimio kwenye *Hansard* linakaa pekee yake.

Kwa madhumuni hayo basi, sasa nitamwita Katibu asome Azimio moja tulishughulikie, asome Azimio la pili tulishughulikie, asome Azimio la tatu tulishughulikie na hatimaye tumalizie na lile Azimio la nne.

Kwa hiyo, sasa namwomba Katibu aweze kutusomea Azimio la kwanza kwa mpangilio uliopo kwenye *Order Paper.* Baada ya hapo ndipo nitawahoji kuhusu Azimio sasa la kuridhia Mkataba moja baada ya mwingine.

**Mkataba wa Kimataifa wa Mwaka 1965 Kuhusu Taratibu za Kuhudumia Meli za Kimataifa Zinazobeba Mizigo na Abiria Zikiwa *Bandarini (International Maritime Traffic, 1965)***

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja zote zilishawasilishwa na kuungwa mkono. Azimio hili sasa limesomwa na sasa ni wakati ambapo nitawahoji ili kuweza kuridhia huo Mkataba kwanza kama ulivyosomwa na Katibu.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuhudumia Meli za Kimataifa Zinazobeba Mizigo na Abiria Zikiwa Bandarini liliridhiwa na Bunge)*

**Mkataba wa ICAO wa mwaka 1944 Kuhusu kuruhusu Ndege za Kimataifa Zenye Ratiba Kupita kwenye Anga ya Nchi Nyingine bila Kutua kwa Sababu zisizo za Kibiashara *(International Air Service Transit Agreement (IASTA) of 1944.***

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la kuruhusu Ndege za Kimataifa Zenye Ratiba Kupita kwenye Anga ya Nchi Nyingine bila Kutua kwa Sababu zisizo za* Kibiashara *liliridhiwa na Bunge)*

**Mkataba wa Uzuiaji Uchafuzi wa Bahari kwa Njia ya Utupaji Taka na Bidhaa Nyingine wa Mwaka 1972 (*Ratification othe Convention on Prevention of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and other Matters, 1972)***

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Uzuiaji Uchafuzi wa Bahari kwa Njia ya Utupaji Taka na Bidhaa Nyingine wa mwaka 1972 liliridhiwa na Bunge)*

**Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira na Bahari kutoka Melini *(International Convention for the Prevention of Pollution from the Ships, (Marpol 1973/1978)***

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio manne yaliyotajwa hapo juu yaliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa shughuli zote zilizoorodheshwa katika shughuli za leo.

Ninalo tu tangazo hapa kwamba kesho baada ya kipindi cha maswali nitamwita Waziri wa Miundombinu kwa ajili ya Muswada wa *the Universal Communication Access Services Bill, 2006* ili uweze kusomwa mara ya pili. Kwa hiyo, huo ndio Muswada tutakaoendelea nao. Natangaza sasa ili wale ambao wanajiandaa kuchangia waweze kujua Muswada utakaojadiliwa kesho.

Pia Ofisi ya Bunge imeandaa nakala za kutosha za Muswada. Kwa wale ambao kwa bahati mbaya labda wamesahau Muswada huo nyumbani, Miswada inapatikana kwa Katibu wa Bunge na hata jioni hii mnaweza kuipiatia kutoka kwa Maafisa hapa ili muweze kuwa tayari kwa ajili ya kesho.

Baada ya tangazo hilo na kwa kuzingatia kwamba sasa hakuna tena shughuli nyingine ya kuendelea nayo, naahirisha Bunge hadi kesho Saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.01 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Novemba, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*